SUPA JACKPOT
TZS. 1,062,078,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 3

**ACT-Wazalendo kuja kivingine mwaka 2023**


ama
ALHAMISI DESEMBA 29, 2022
AFYA NA MAZINGIRA

SHULENI HADI MAJUMBANI... Simulizi zenye ukakasi, madhila jinsia yanavyowaangukia watoto kila waliko (Ukurasa 15)

Ugonjwa wa mtu anawehuka kihisia, anashindwa kuizuia dhamira ngono (Ukurasa 16)

**Akerwa uharibifu mazingira, anuia kupanda miti milioni tano kijijini**

• Kila mwezi 2,700; azama mfukoni Mil. 11/-

Na Mwandishi Wetu

NI kwamba ameamua kujitosa kuimaliza kazia kuwa mwanamazingira wa ukweli, tena kwa vitendo, Adama Diémé (48), mwanaume raia wa Senegal, amejiwekea dhamira kupanda miti milioni tano katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kwa lugha rahisi ni ajenda ya kupanda miti milioni moja kila mwaka, au kila mwezi miti 2,740, hali kadhalika wastani wa miti isiyopungua 90 kila siku.

Ni wazo la mradi uliomjia pale aliporudi nyumbani eneo la Casamance mwaka 2020, baada ya kufanya kazi barani Ulaya.

...kutegemea na hali ya ardhi na mahitaji ya jamii. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, alishapanda zaidi ya miche 142,000 imetunzwa na kuota mizizi.

Mshirika wake, Yolanda Pereñiguez, anayefanya kazi ya ufundi cherehani kijijini, amekuwa muhimu katika kusaidia kupanga fedha kwa kubuni fulana inayouzwa nje ya nchi kwa dola 15 (Sh. 35,000), akiwa na Raymonde Coly, anayefanya kazi katika karakana ndogo yenye cherehani mbili ili kuzitengeneza kutoka kwa nguo za kienyeji, zenye picha ya kipekee ya mbuyu. Kila moja inayouzwa inaweza kulipia miche 15 ya miti.

"Nilichagua mbuyu kwani ni alama ya mti wa Kiafrika," anasema Periniguiz, akifafanua: "Inapendeza kujua kwamba fulana hizi zinakwenda duniani kote, Ulaya na hata Canada kusaidia mradi wa miti."

Miaka 10 iliyopita, viwango vya ukingo wa maji ulikuwa mbali zaidi na kufika kijijini hapo ambako...

Alhamisi Desemba 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581174

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 13

# Daktari ataja mbinu za kuepusha mauaji

UKURASA 2



## Askari anayedaiwa kutoroka na meno ya tembo akamatwa

UKURASA 2

UKURASA WA 3

### SAMIA AMWOMBEA AFYA NJEMA LOWASSA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwakilisha Dk. Samia Suluhu Hassan kumjulia hali Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, anayeendelea na matibabu...

UKURASA WA 4

### DK. MWINYI AIPA JUKUMU SUZA KUANDAA VIJANA KUTUMIKIA TAIFA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema bado Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kina wajibu wa kuwaandaa vijana kuwa mahiri, weledi kitaaluma wenye ubunifu kwa...

UKURASA WA 5

### 'MARUFUKU KULIPUA FATAKI BILA KIBALI MAALUM'

JESHI la Polisi mkoani Tanga limepiga marufuku ufyatuaji fataki ovyo na kuchoma matairi barabarani siku ya mkesha wa mwaka mpya.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkoa wa Tanga, Leopard Fungu, alitangaza marufuku hiyo wakati...

## Mke amshtaki mumewe kisa kuchukua mkopo benki kinyemela

UKURASA 9

MICHEZO YANGA, FEITOTO, MOSHI MWEUSI UK. 32

KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimtunuku Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili, Nunuu Abdalla Mohammed, katika mahafali ya 18 ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) yaliyofanyika Wilaya ya Kati Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Daktari ataja mbinu kuepusha mauaji

**Na Christina Mwakangale**

KUDHIBITI hasira, mihemko, kutoa elimu kwa jamii pamoja na kuondoka eneo na mazingira yanayochochea kutenda mambo mabaya, vimetajwa kuwa ndiyo dawa inayoweza kudhibiti au kupunguza matukio ya watu kujiua au kuua.

Daktari Bingwa katika Idara ya Afya ya Akili ya Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Raymond Mgeni, alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu ongezeko la matukio ya mauaji, ikiwamo watu kujiua au kutekeleza mauaji.

Alisema jamii inapaswa kudhibiti msukumo wa hasira unaochochewa na sababu yoyote, ikiwamo kuudhiwa ama kusingiziwa jambo lolote, akisema kati ya sababu za ongezeko la matukio ya mauaji nchini ni ukosefu wa kudhibiti hali hiyo.

Kauli hiyo ya Dk. Mgeni inakwenda sambamba na takwimu zilizotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mwaka juzi kuhusu haki za binadamu kwamba watu wanne kati ya 10 waliojiua, walikuwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 35.

Alisema ili kudhibiti matukio ya watu kujiua au kuua, jamii inapaswa ijenge mazoea na utaratibu wa kujifunza na kuwafundisha watoto, kutoruhusu kuchukua hatua wapatwapo na msukumo huo, badala yake waondoke eneo au mazingira yanayosababishia hasira.

"Rafiki wa aina yeyote, ndugu yako anapokutukana utatafsiri na kuwa chanzo cha sababu ya msukumo wa hasira. Tuache kutafsiri kila neno wakati wa hasira. Ukidhibiti mihemko, misukumo au vitendo ambavyo vimeleta madhara, ingepunguza vifo ambavyo kila siku tunaona na kusikia kwenye vyombo vya habari.

"Ukiwa na hasira unatakiwa kuwa na uwezo wa kuvuta pumzi unapokutwa na msukumo huo. Pia usitoe tafsiri ya kile ambacho umefanyiwa au mtu amekutukana. Utakuta mtu ambaye amenitukana akiwa hana utimamu wa akili utaona ni jambo la kawaida, ila kama mtu aliyetimamu itakuumiza, usijipe muda kutafsiri haya," alisema Dk. Mgeni.

Aidha, alibainisha kwamba matukio yanayoongezeka ya watu kijiua hutokana na kuchochewa na misukumo isiyodhibitiwa kutokana na hasira, ikiwamo mazingira yanayowazunguka watu huku kusababisha mtu kuamua jambo pasipo kutarajia na kufahamu athari zake baadaye.

"Kuna wakati mwingine unaongea na mtu anakuudhi, kuna wengine hawana udhibiti, wengine wanaoudhiwa wanapoambiwa jambo ambalo hawajalitenda wanajikuta wakipatwa na hasira, akipandwa na hasira anaweza kuchukua kitu ajichome au anywe sumu.

"Kuna wakati sababu fulani inaweza kuchangia kisasi na matukio mengi, mtu alikuwa kwenye mazungumzo wakapishana kauli utakuta ananyanyua jiwe au chupa na kumrushia mwenzake. Idhibiti hali hayo na iwe ni utaratibu kwenye maisha yetu kila siku," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) akisoma muhtasari wa ripoti kuhusu haki za binadamu kwa mwaka 2021/22, alisema haki ya kuishi inakiukwa kutokana na matukio kadhaa hasa ongezeko la mauaji yatokanayo na wivu wa kimapenzi.

Alisema kwamba wanawake ndiyo waathiriwa wakuu wa matukio ya ukatili wa kijinsia, wanauawa na wapenzi wao kwa sababu wivu wa mapenzi, ingawa takwimu zinabainisha pia wanaume ambao wanaongoza kwa kuchukua maamuzi magumu ya kujiua. Kadhalika, takwimu za Shirika la Afya Dunani (WHO) zinaonyesha kwamba Watanzania milioni saba, wana tatizo la afya ya akili, wengi wao wakiishi Dar es Salaam.

Pia zinabainisha kuwa mtu mmoja hufariki dunia katika kila sekunde 40 kutokana na kujiua.

Aidha, takwimu za LHRC kuhusu haki za binadamu mwaka 2021, inabainisha kwamba watu wanne kati ya 10 waliojiua mwaka jana walikuwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

# Askari anayedaiwa kutoroka na meno ya tembo akamatwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

ASKARI polisi anayetuhumiwa kuhusika katika tukio la kuomba rushwa ya Sh. milioni 100 kwa mfanyabiashara maarufu wa mji wa Usa River, Prof. Justine Maeda, ambaye alitoroka na ushahidi wa meno ya tembo, amekamatwa.

Askari huyo kwa sasa anashikiliwa katika Kituo cha Polisi Usa River kilichoko Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi (ACP) Justine Masejo, alipoulizwa juu ya taarifa za kushikiliwa kwa Kostebo Zakhayo, alisema jambo hilo liko chini ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

"Haliko kwetu liko TAKUKURU, ila nafuatilia hivi sasa kuona taarifa hizo zina ukweli kiasi gani. Kwa mara ya mwisho suala hili lilikuwa linashughulikiwa na TAKUKURU wenyewe, hivyo sikujua kinachoendelea ila nitafuatilia kujua ukweli wa tukio hilo," alisema.

Alipotafutwa kuzungumzia taarifa hizo, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha, Zawadi Ngailo, alithibitisha kukamatwa kwa askari polisi huyo ambaye alikutwa akiwa amejificha kwa mwanamke mmoja eneo la Kimandolu, jijini Arusha.

"Kostebo Zahkayo, alikamatwa jijini Arusha na uchunguzi zaidi unaendelea na baadaye atafikishwa mahakamani," alisema Ngailo.

Akizungumza kwa njia ya simu, mwathiriwa wa tukio hilo, Prof. Maeda, alisema amesikia kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo akieleza kuwa ni miongoni mwa askari waliogawana fedha zake, ambaye alitoroka pia na kidhibiti cha meno ya tembo na mgawo wa Sh. milioni 31 kati ya Sh. milioni 100 walizochukua.

"Mimi pia nimesikia askari huyo amekamatwa mimi ninachotaka ni fedha zangu tu wanirudishie mpaka sasa sijapata chochote," alisema Prof. Maeda.

Habari kutoka vyanzo vya ndani ya Jeshi la Polisi Usa River zilisema Konstebo Zakhayo alikamatwa Kijenge Juu, Kata ya Kimandolu jijini Arusha, nyumbani kwa mke wake, alikoamua kurudi na kujificha baada ya kutokomea mafichoni.

Kostebo Zahkayo na askari wenzake saba walifanya tukio hilo Machi, mwaka jana na askari waliokamatwa (majina tunahifadhi kwa sasa) ni pamoja wakaguzi wasaidizi wawili, Koplo mmoja na Konstebo (PC) wanne wawili ni wa kituo Kikuu cha Polisi Arusha ambao walitoroka lindo na kwenda kufanya uhalifu huo wakiwa na silaha.

Ilidaiwa kuwa mmoja wa raia watatu waliokamatwa (jina tunalihifadhi) aliwahi kuwa mfanyakazi katika shamba la Prof. Maeda katika Mji wa Usa River na alifukuzwa kazi muda mrefu na ndiye aliyeshawishi polisi waombe rushwa kwa bosi wake wa zamani kwa madai kwamba ana mali nyingi na ni mwoga wa polisi.

Mtuhumiwa huyo, anadaiwa kuwa aliwaeleza polisi watafute meno ya tembo wayaweke kwenye moja ya mizinga ya nyuki shambani kwa mafanyabiashara huyo ili wamtuhumu kuwa anafanya biashara haramu na kwa kuwa ni mwoga, atakubali kutoa rushwa ya kiasi chochote cha fedha.

Ilidaiwa kuwa Polisi wa Usa River kwa kushirikiana na raia hao walitekeleza mpango huo na siku ya upekuzi, polisi wawili wenye silaha kutoka Arusha mjini walikwenda kwenye eneo la tukio ili kumwaminisha mfanyabiashara huyo kuwa upekuzi ni halali na viongozi wa polisi Usa na Kituo Kikuu Arusha wanajua jambo ambalo si kweli.

Taarifa zinadai kuwa shamba la mfanyabiashara huyo lina mizinga mingi ya nyuki, lakini katika upekuzi huo, polisi walikwenda moja kwa moja katika mzinga walikoficha meno ya tembo na kumwonesha mfanyabiashara huyo kuwa anafanya biashara haramu, hivyo anastahili kushtakiwa kwa uhujumu uchumi.

Inadaiwa kuwa wakati wa upekuzi hakukuwa na kiongozi yeyote wa serikali wa mtaa wala mjumbe wa nyumba 10 na hata ndugu wa karibu wa mtuhumiwa.

Vyanzo vya habari hizi vya Usa river na Arusha mjini vinadai kuwa mfanyabiashara huyo aliwauliza polisi wanahitaji kiasi gani ili kumaliza kesi hiyo, wakasema walihitaji Sh. milioni 100.

Inadaiwa kuwa mfanyabiashara huyo aliwapa Sh. milioni 74 alizokwenda kuchukua katika Benki ya NMB na CRDB zilizoko katika Mji wa Usa River na kiasi kingine cha fedha cha Sh. milioni 26 aliomba kwa ndugu zake na kukamilisha kiasi cha Sh. milioni 100 walizoomba askari hao.

"Baada ya kunikamatisha meno ya tembo kwa kujiwekea kwenye mizinga yangu ya nyuki, walitaka niwapatie Sh. milioni 100 ili wasiende kunifungulia kesi ya uhujumu uchumi, ndipo nilipoamua kuwapatia fedha hizo," alisema.

Prof. Maeda aliongeza kuwa askari hao baada ya kuona ameenda kulalamika kituo cha polisi cha Usa River, waliamua kumrudishia Sh. milioni 26 huku wakisema kuwa fedha nyingine wamepeleka kwa wakubwa wao ambazo ni Sh. milioni 50.

HABARI KITAIFA

# Samia amwombea afya njema Lowassa

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwakilisha Dk. Samia Suluhu Hassan kumjulia hali Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, anayeendelea na matibabu Afrika Kusini.

Akizungumza na wanafamilia kwa niaba ya Rais Samia, Waziri Mkuu amewasilisha salamu za pole kutoka kwa Rais Samia na kusema anafuatilia hali ya Lowassa kwa ukaribu na anamwombea afya njema.

Alitoa salamu hizo jana, jijini Johannesburg, Afrika Kusini ambako aliienda kumjulia hali Lowassa.

Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Mama Regina Lowassa, amemshukuru Rais kwa jinsi ambavyo amekuwa karibu na wanafamilia na namna ambavyo anafuatilia matibabu ya mpendwa wao.

Naye mtoto mkubwa wa Lowassa na Mbunge wa Monduli, Fredrick Lowassa, amewashukuru Watanzania kwa maombi yao ya kumtakia afya njema baba yao.



Mhifadhi Mkuu katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Neema Mollel (kulia), akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea hifadhi hiyo kuhusu vivutio mbalimbali vilivyoko katika hifadhi hiyo kikiwamo cha uwepo wa Simba wanaopanda juu ya miti. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# ACT-Wazalendo kuja kivingine 2023

Na Maulid Mmbaga

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kitaendelea kufuatilia, kupaza sauti na kutoa mapendekezo ya masuala yenye tija kwa wananchi na taifa ikiwamo kupanda kwa bei za bidhaa, kanuni za kikokotoo cha uzeeni na Bima ya Afya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri Mkuu Kivuli wa chama hicho, Doroth Semu, alisema wamekuwa wakimulika, kufuatilia, kukosoa na kutoa mapendekezo ya kimtazamo, kifikra na kisera kuhusu uamuzi na utendaji wa serikali na vyombo vyake tanzu.

Alisema wataendelea kusimama kidete kuishauri serikali kukabiliana na majanga yanayoathiri maisha ya watu, kutoa msimamo na mapendekezo ya kukabiliana na changamoto ili kuleta unafuu wa maisha kwa wananchi.

Alibainisha kuwa kilio cha wananchi kuhusu mfumuko wa bei za bidhaa muhimu kama petroli, dizeli na mafuta ya taa ni jambo lililosababisha kupanda kwa gharama za maisha.

"Bidhaa zingine ni za chakula kama maharagwe, mafuta ya kula, sukari, unga na mchele vimepanda zaidi ndani ya mwaka mmoja na pembejeo za kilimo na mbolea, baada ya kupaza sauti na kutoa mapendekezo kwa serikali kuweka ruzuku kidogo imeshuka," alisema.

Kadhalika, alisema katika kuisimamia serikali ipasavyo, ACT-Wazalendo kupitia kamati ya wasemaji wa kisekta itaendelea kufuatilia, kuchambua, kukosoa na kutoa mapendekezo yao kuhusu miswada kadhaa iliyowasilishwa bungeni na serikali.

Alikumbusha kuwa serikali iliwasilisha bungeni Muswada wa Bima ya Afya kwa wote Septemba, mwaka huu na kwamba pamoja na nia yake njema ya kutaka kupanua wigo wa watu walio kwenye sekta isiyo rasmi kuingizwa kwenye mifumo ya bima, alidai kuwa maudhui ya muswada huo yalikuwa na upungufu.

Alibainisha kuwa tatizo waliloliona ni kuwa sehemu ya wananchi walio sekta isiyo rasmi wasingeweza kumudu gharama za bima hiyo kutokana na viwango vya juu vilivyowekwa.

"Tuliwaeleza tatizo la afya ya Watanzania halitokani na kukosa matibabu tu bali ni mazingira hatarishi ya kazi, watu kukosa vipato vya kueleweka, maskini kuendelea kuwa maskini zaidi, wazee kutopatiwa mahitaji yao ya msingi, umaskini wa chakula na kipato," alisema.

"Mfumo utakaoimarisha afya ya Watanzania na kuwezesha kugharamia matibabu kwa watu wote nchini ndio jawabu la kuimarisha afya na kukabiliana na changamoto za gharama za matibabu," alisema.

"Sisi tulipendekeza mfumo wa hifadhi ya jamii kwa watu wote ambao ndani yake ungetoa fao la Bima ya Afya kwa watu wote. Hatimaye muswada uliondolewa rasmi bungeni, tunatumai sasa kama wadau tutasikilizana ili kuboresha zaidi," alisema.

**KIKOKOTOO**

Alisema serikali ilirejesha kanuni ya mafao iliyopigiwa kelele 2019 na kuifanyia marekebisho madogo, akieleza kuwa walipambana kuhakikisha kanuni hizo zisipitishwe na Bunge kwa kutoa mapendekezo mbadala.

Alisema kuwa uamuzi wa serikali kutangaza kanuni mpya uliweka kikokotoo cha 1/580 badala ya 1540, pia malipo ya mkupuo ya mafao ya mtumishi aliyestaafu atalipwa kwa asilimia 33 badala ya 50 iliyokuwa inatumika kabla, umri wa kuhudumiwa mstaafu ni miaka 12.5 badala ya miaka 15.5.

"Tulionyesha uchambuzi wa athari za kutumia kikokotoo kipya chenye marekebisho madogo kutoka asilimia 25 hadi 33 na kuacha maeneo mengine kama yalivyo, namna yatakavyoenda kumpunja mstaafu.

"Kutokana na matatizo ya kanuni za mafao tulizipinga, kwa kuwa tunaamini mfumo wa hifadhi ya jamii unapaswa kusaidia kulinda maisha ya watu na kutoa uhakika wa kuishi vizuri unapokutwa na majanga au kupoteza uwezo wa kufanya kazi kwa namna yoyote ile," alisema.

**UTAWALA BORA**

Alisema wataendelea kuwa mstari wa mbele kupigania mageuzi ya Sheria ya Jeshi la Polisi ili kulifanya kuwa linalotumia weledi na kujali wananchi badala ya jeshi la mabavu dhidi ya raia.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**29.12.2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Ijumaa tarehe 30-12-2022 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji**, gari hizo zina namba za usajili:

**T 275CZS / T 568EAZ**
**T 515BKC / T 572EAZ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 20.00
Upana - mita 5.50
Kimo - mita 4.60

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti**, gari zitasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

17208402

# Dk. Mwinyi aipa jukumu SUZA kuandaa vijana kutumikia taifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema bado Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kina wajibu wa kuwaandaa vijana kuwa mahiri, weledi kitaaluma wenye ubunifu kwa kutambua fursa na kuzitumia ipasavyo.

Dk. Mwinyi ambaye ni Mkuu wa SUZA, alisema hayo jana katika mahafali ya 18 ya chuo hicho yaliyofanyika katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Tunguu mjini Zanzibar.

Alisema ni lazima chuo hicho kitoe wahitimu wenye uwezo wa kuhimili ushindani uliopo katika soko la ajira ili vijana hao wanaajirika na kutumia elimu waliyopata kujiajiri.

Pia alisema ili nchi kuendelea, inahitaji watu wenye uwezo wa kujifunza kwa haraka, wenye kujituma, wachapakazi, waaminifu, waadilifu na wenye uwezo wa kuwashawishi wengine kuwa hivyo.

Alisema chuo hicho kimekuwa kikitoa idadi kubwa ya wahitimu katika programu mbalimbali kila mwaka na wamekuwa wakiongezeka na hata katika programu mpya tatu ambazo zinakwenda sambamba na mahitaji ya taifa yaliyoko hivi sasa.

Rais Mwinyi alisema programu hizo zilianzishwa maalum kwa lengo la kuwa na wataalamu wa fani hizo ikiwamo shahada ya uzamili ya elimu ya lugha, shahada ya sayansi ya kilimo mjumuisho na shahada ya sayansi ya uuguzi.

Alisema hicho ni kigezo kimojawapo muhimu cha kubainisha kuwa tasisi hiyo ya elimu ya juu Zanzibar inatekeleza kwa mafanikio jukumu la kuzalisha wasomi wa fani mbalimbali ambao ni nguvu kazi na chachu ya kusukuma mbele maendeleo ya nchi.

Dk. Mwinyi alisema mageuzi makubwa waliyodhamiria hivi sasa katika kuimarisha elimu inayotolewa Zanzibar hayawezi kupata ufanisi ikiwa hakuna ushirikiano kati ya wizara, SUZA na wadau wengine wa sekta ya elimu wa ndani na nje ya nchi.

Akizungumzia changamoto zinazokabili chuo hicho, Dk. Mwinyi aliwataka wanajumuiya wa chuo kutoa ushirikiano wa uongozi kufanya kazi kwa pamoja ili kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo.

Alisema ni lazima kila mmoja kuwa mzalendo na kutambua umuhimu wa kutekeleza wajibu wake katika maendeleo ya chuo huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazokabili chuo hicho na msaada wa hali na mali.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema chuo hicho ni pekee kinachomilikiwa na serikali na anaamini kitaendelea kuimarika na kutoa huduma bora katika taasisi husika ili kupata vijana waliobobea kitaaluma.

Aliiomba SUZA kuhakikisha vijana waotoka katika chuo hicho taaluma wanazopatiwa ziwawezeshe kujiajiri ili wasiwe mzigo kwa familia zao.


Hata hivyo, alisema ni lazima kama vyuo vikuu kuwekeza kutoa wataalamu watakaoendana na Sera ya Maendeleo ya 2050 kwa kuanzisha fani ambazo zitaendana na mahitaji ya sasa.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Ali Makame Ussi, akitoa nasaha kwa wahitimu aliwasisitiza kukumbuka kuwa kutafuta elimu ni wajibu uliokuwa endelevu kwani kumaliza kwao katika ngazi mbalimbali za taaluma iwe ni mwanzo wa ngazi inayofuata kujiendeleza kwani elimu haina mwisho.

Alisema kwa wale wanaorejea kazini baada ya kumaliza masomo na wale watakaobahatika kuajiriwa ni vyema wakaonesha kwamba wameongeza uwezo mkubwa wa kufanya kazi kutokana na taaluma waliyoipata chuoni na wale watakaokosa ajira basi anaamini taaluma itawasaidia katika shughuli za ujasiriamali na kujiajiri.

Dk. Ussi aliwasisitiza wahitimu hao kuwa na uthubutu wa kutimiza malengo waliojiwekea na kutumia uwezo walionao kwa kutenda yale yaliyobora kwao na jamii iliyowazunguka kwa kuwa wawajibikaji, wachapakazi na wazalendo wa nchi yao.

Wanafunzi 1,913 wakiwamo wanaume 810 na wanawake 1,103 walitunukiwa astashahada, stashahada, shahada, shahada za uzamili na shahada ya uzamivu.



Mafundi wa Kampuni ya Pindoria Construction Ltd wakiendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa madarasa kwenye Shule mpya ya Sekondari ya Liwiti iliyoko Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu 80 shule za sekondari, msingi wapata mafunzo ya kompyuta, ubunifu

**Na Gwamaka Alipipi**

WALIMU 80 kutoka shule za sekondari na msingi jijini Dar es Salaam, wamepatiwa mafunzo ya programu za kompyuta na ubunifu ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

Mafunzo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na Kodi Atamizi ya Ubunifu Dar es Salaam (DTBI), iliyo chini ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH).

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mafunzo hayo, Ofisa kutoka COSTECH, Michael Thomas, alisema mafunzo hayo ni ya siku mbili na yalilenga kuwapatia ujuzi na ubunifu walimu wa shule za msingi na sekondari za jijini Dar es Salaam.

Alisema walimu hao wakihitimu mafunzo watakwenda kuwafundisha wanafunzi na kuwawezesha kutatua matatizo mbalimbali pamoja na kuwa na ujuzi wa matumizi ya kompyuta.

"Tumekuwa tukizifikia shule nyingi za msingi na sekondari, hapa Kijitonyama kuna sehemu ya kutolea hayo mafunzo na ndiyo maana tumewakusanya walimu wote wa Jiji la Dar es Salaam. Lakini lengo letu ni kuzifikia shule zote nchini," alisema Thomas.

Alisema walianza kutoa mafunzo hayo mwaka 2017 kwa mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Zanzibar, lengo kuu likiwa ni kuwafundisha walimu masuala ya kompyuta na ubunifu, hadi sasa wamewafikia walimu zaidi ya 3,000.

"Walimu wakishapata mafunzo na kwenda kuwafundisha wanafunzi, hao wanafunzi tunawakutanisha katika shindano liitwalo 'Africa Code Challenge' na kuwapima uelewa wao katika masuala ya ubunifu na kompyuta," alisema.

Mmoja wa walimu waliopata mafunzo hayo kutoka Shule ya Msingi Libaman, Flora Saimon, alisema: "Hii programu inamsaidia mwalimu kujiamini, pia inamsaidia mwalimu kwenda na uchumi wa viwanda. Kwa siku mbili tulizokuwa hapa tumefundishwa namna ya kumjenga mwanafunzi awe mbunifu."

Mwalimu kutoka Shule ya Sekondari Kambangwa, Omary Mhina, aliahidi atakaporudi shuleni atawafundisha wanafunzi namna ya kuiendesha kompyuta.

Alisema kupitia programu hiyo wanafunzi wataweza kutatua matatizo kwa mifumo iliyoandaliwa.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Nuru Juba, alisema baada ya kutoa mafunzo hayo kwa walimu, wanafunzi hushiriki katika mafunzo yaitwayo Afrika Code Challenge.

## Barabara ya Makete-Mbeya kufunguka kwa lami

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema serikali itaendelea na ujenzi wa barabara za lami katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ili kuunganisha vyema ukanda huo na bandari ya Mtwara na kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji, kukuza uzalishaji wa mazao ya kilimo, misitu na utalii.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini ujenzi wa barabara ya Isyonje-Kikondo hadi Makete kilomita 96.2 sehemu ya Kitulo hadi Iniho kilomita 36.3 inayojengwa kwa kiwango cha lami, Waziri Prof. Mbarawa alisema serikali itahakikisha inaunganisha kwa njia fupi mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Njombe hadi Mbeya kupitia Makete ili kukuza fursa za kiuchumi zilizoko katika ushoroba huo.

"Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia imejikita kwenye kuboresha miundombinu hususani maeneo yenye uzalishaji mkubwa hivyo niwahakikishie kuwa ongezeni uzalishaji miundombinu bora inakuja," amesisitiza Waziri Prof. Mbarawa.

Aliitaka Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), kumsimamia kikamilifu mkandarasi anayejenga barabara hiyo M/S China National Aero-Technology Egineering Corporation ili mradi huo ukamilike kwa wakati na viwango.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, amesema ujenzi wa barabara hiyo utahusisha ujenzi wa mizani katika Kijiji cha Igalala ili kudhibiti magari yanayozidisha uzito na kuwataka wananchi kuzingatia sheria na kulinda miundombinu yote ya barabara.

Mbunge wa Makete, Festo Sanga, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi huo kwa kuwa kukamilika kwake kutaunganisha wilaya hiyo na Mkoa wa Mbeya kwa njia fupi, kukuza utalii wa hifadhi ya taifa Kitulo na kupandisha thamani ya mazao mbalimbali yanayozalishwa mkoani Njombe.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthon Mtaka, aliwataka wakazi wa Wilaya ya Makete nchini kutumia maendeleo ya ujenzi wa miundombinu kuwekeza wilayani humo.

Zaidi ya Sh. bilioni 69.7 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi huo unaotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miezi 36.



Mwonekano wa kituo cha mabasi yaendayo haraka katika barabara ya Kawawa, Magomeni Mikumi, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 'Marufuku kulipua fataki, matairi bila kibali maalum'

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga limepiga marufuku ufyatuaji fataki ovyo na kuchoma matairi barabarani siku ya mkesha wa mwaka mpya.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkoa wa Tanga, Leopard Fungu, alitangaza marufuku hiyo wakati akizungumza na mwandishi wa habari hizi.

Alisema upigaji wa fataki hufanywa na baadhi ya watu kiholela na kusababisha wananchi wenye matatizo ya afya kupata mshtuko unaosababisha ugonjwa wa moyo.

Alisema jeshi hilo limebaini siku ya mkesha wanapofyatua fataki hizo na kuchoma matairi barabarani wanaharibu barabara na kusababisha adha kubwa ya madereva kukwepa matairi hayo wakiwa wamebeba abiria hali inayoweza kusababisha ajali.

Kamanda Fungu, alisema mwananchi atakayekwenda kinyume na tangazo hilo atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria na kwamba atakayeruhusiwa kulipua milipuko ni yule aliyepewa kibali maalumu na Jeshi la Polisi.

Kadhalika, watashirikiana na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama pamoja na vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuhakikisha wanadhibiti matukio ya uhalifu.

Pia Kamanda Fungu alisema jeshi hilo litatumia doria za miguu na pikipiki katika barabara zote muhimu ili wananchi washerehekee Sikukuu ya Mwaka Mpya kwa ngazi ya familia katika mitaa kwa amani na utulivu.

Kamanda Fungu alisema jeshi hilo limepiga marufuku disko toto katika kumbi mbalimbali kutokana na sifa za kumbi zilizopo kutokidhi viwango vya kiusalama kwa watoto.

Katika hatua nyingine Jeshi la Polisi Wilaya ya Muheza limedhibiti vitendo vya uhalifu Sikukuu ya Krismasi kwa kuweka ulinzi mkali wa doria.

Doria hiyo iliongozwa na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Muheza OCD Hadija Sokolo, Mkuu wa Upelelezi wilaya, Charles Ntenga, Mkuu wa Kituo cha Polisi Muheza Kuluthumu Bambe, Kaimu Mkuu wa Upelelezi wilaya, Teo Njawa na vijana wao.

# Ridhiwani ataka changamoto urasimishaji makazi zitatuliwe

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, ameagiza ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam kuitisha miamala ya wananchi wa Kata ya Kivule wasiopatiwa hati katika urasimishaji makazi holela.

Ridhiwani alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akizungumza na wananchi wa Kivule, jijini Dar es Salaam alipokwenda kutoa hati ikiwa ni juhudi za wizara kuwapelekea wananchi hatimiliki za ardhi katika maeneo yao.



"Kwa kuwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao waliacha namba zao za simu, basi kamishna itisha miamala ya wale waliolipa na kuwaelekeza ni kitu gani cha kufanya ili waweze kupata hati," alisema.

Katika mkutano huo, wananchi wa kata ya Kivule walimweleza Naibu Waziri kuwa pamoja na kulipa Sh. 160,000 wameshindwa kupatiwa hati na kwamba kumekuwapo mawasiliano hafifu baina ya wananchi na kamati zinazosimamia suala hilo.

Wananchi hao pia walishusha lawama kwa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) kuwa kinachelewesha kukamilisha urasimishaji katika mitaa ya Kivule.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam, Shukran Kyando, Chuo cha Ardhi Morogoro kimefanya kazi kwa zaidi ya asilimia 80 lakini fedha zilizotolewa na wananchi katika urasmishaji ni asilimia 11 pekee.

"Kata ya Kivuke ina mitaa minne na Chuo cha Ardhi Morogoro kimeingia mkataba wa kufanya kazi katika mitaa hiyo kwa ajili ya kumalizia kazi ya urasimishaji lakini zipo changamoto mbili, yaani upande wa kampuni na ule wa wananchi kutolipia zaidi ya viwanja 7,000 ambavyo vimeidhinishwa," alisema Kyando.

Naibu Waziri Kikwete kupitia mkutano huo alikitaka Chuo cha Ardhi Morogoro kupeleka miamala yote iliyofanyia kazi kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam na kusisitiza kuwa taarifa zote zinazokusanywa kuhusiana na urasimishaji, mwenye mamlaka nazo ni kamishna na si kampuni.

"Kama kuna maeneo yamekwama basi kampuni ziongee na kamishna ili kujua namna ya kutatua kero ili kwenda mbele na naelekeza hadi kufikia Februari Mosi, 2023 suala la wananchi wa Kivule kuhusiana na urasimishaji makazi tuwe tumemalizana nalo." Alisisitiza.


## BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD

WE ARE DEALING GENERAL AUCTIONING, DEBT COLLECTION, EVICTION, INVESTIGATION AND REPOSSESSION, STORAGE, COMMISSION AGENCY AND GENERAL BUSINESS.

## NOTICE OF SALE AND INVITATION OF SEALED BIDS FOR SALE OF PROPERTY

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** under the powers contained in the law and Mortgage Deed and other powers enabling us to do so, We **BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD of P.O.BOX 16095 , Dar es Salaam,** duly appointed by **BANK OF AFRICA (T) LTD** to sell the mortgaged property "as they are" by sealed bids. **WE HEREBY INVITE BIDS FROM GENERAL PUBLIC** for the outright purchase of the properties described in the table below

| S.N | PROPERTY DESCRIPTION | LOCATION | Property Registration Owner | Bids Submission Date | Bids Opening Date |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Property held under derivative right on CT no. 146626,plot no. 2362 block "B" | Yombo Area | **JIMMY JIMMY MLIMBILA** | 12TH January 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 12th January 2023 before 12;00 hours at the address below |
| 2 | Property held under derivate right on CT no. 136833,plot no. 2325 block "B" | Yombo Area | **JIMMY JIMMY MLIMBILA** | 12TH January 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 12th January 2023 before 12;00 hours at the address below |
| 3 | Property held under derivative right on CT no. 94381,plot no. 2300,block "B" | Yombo area | **JIMMY JIMMY MLIMBILA** | 12TH January 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 12th January 2023 before 12;00 hours at the address below |
| 4 | Property held under derivative right on CT no. 93995,plot no. 2360, block "B" | Yombo Area | **JIMMY JIMMY MLIMBILA** | 12TH January 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 12th January 2023 before 12;00 hours at the address below |
| 5 | Property held under derivative right on CT no. 94125,plot no. 2302, block "B" | Yombo Area | **JIMMY JIMMY MLIMBILA** | 12TH January 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 12th January 2023 before 12;00 hours at the address below |
| 6. | Property held under Derivative Right on CT no. 93995,plot no.2302 block "B" | Yombo Area | **JIMMY JIMMY MLIMBILA** | 12TH January 2023 before 11:00 Hours at the address below | On 12thJanuary 2023 before 12;00 hours at the address below |

**TERMS AND CONDITIONS:-**

1. Bid must submitted in sealed envelope clearly marked " BID FOR THE PURCHASE OF JIMMY JIMMY MLIMBILA PROPERTY, including full address of the bidder.
2. The successful Bidder shall be required to deposit 25% of the bid price within 7 days from the date of the award and balance 75% of the bid price within 21 days from the date of the award or within such other time as we may prescribe; failure of which the offer shall be revoked forthwith and the 25% down payment shall be forfeited and the next highest bidder who meets the conditions may be awarded, or cancel the sale process altogether.
3. Bids must be submitted and shall be opened on the date and address described in the table above. Bidders are invited to attend opening ceremony event if they so wish.
4. The property is being sold on "AS THEY ARE", the Bank and us shall have no further liability after the sale.
5. The interested parties will be allowed to inspect the property by prior appointment.
6. All the information contained in this advertisement is free from liability.
7. The successful bidder or otherwise shall be notified within a maximum of seven (7) working days after bid opening: either to his physical address or his email address, which shall be sufficient communication.
8. The bank and we shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all or reject any or all the bids without having to assign any reasons.
9. All costs regarding transfer of ownership shall be borne by the successful bidder.
10. All bids shall be addressed to the address below;

**For further information please contact:**
**Visit our office located at Mbezi Beach area**
**Contact us via Email: bilostarcompany@gmail.com;**
**P.O. Box 16095, DAR ES SALAAM,**
**Contact us on the following numbers; 0716943424 and 0719206984**

17209202

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhalifu unaweza kudhibitiwa ushirikiano ukiwapo kwa jamii

**MARA** kwa mara katika siku za sikukuu kunaripotiwa vitendo vingi vya uhalifu, ikiwamo wizi, watu kupigwa au kuporwa vitu vyao.

Lakini katika kipindi hiki cha Sikukuu ya Krismasi, matukio hayo hayajasikika kwa wingi kama ilivyotokea katika miaka ya nyuma.

Kamanda wa wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alitaja sababu ya matukio hayo kutoripotiwa kwa wingi ni jeshi lake kufanikiwa kudhibiti vikundi vya kihalifu maarufu panya road, pamoja kupunguza ajali za mwisho wa mwaka kutokana na ushiriki wa wananchi katika kufichua vitendo hivyo.

Hata kwenye mitaa kwa sasa watu wanaishi na kulala kwa amani kwa sababu wananchi wameona umuhimu wa kuwa na ulinzi shirikishi ambapo kila mwisho wa mwezi huchangishana kuwezesha wanaofanya kazi hiyo.

Pia sasa hivi ukipita mitaa mingi utakuta wameweka vizuizi vya kuzuia magari na watu wasiofahamika kupita bila kujitambulisha wanakwenda nyumba ipi.

Kwa kweli wananchi wakishirikiana na Jeshi la Polisi kufichua watu wanaofanya uhalifu kwenye mitaa yao, hakuna lisilowezekana na wizi na uhalifu hautakuwapo.

Kamanda Muliro alipozungumza na gazeti hili alifafanua kuwa jamii inapaswa kufuta dhana ya kuamini kila mwisho wa mwaka lazima yatokee matukio ya kihalifu na ajali nyingi.

"Tangu Septemba mwaka huu nilisema mambo ya kusema kila ikifika mwisho wa mwaka kuna ajali nyingi au matukio ya kihalifu sasa limefika mwisho, Jeshi la Polisi halitaki watu kuongea mambo ya kufikirika mimi ukiniambia kuna ajali nyingi nitakuuliza hizo ajali ziko wapi? Ukisema uhalifu nitakuuliza hao wahalifu wako wapi?

"Hata wale wanaokunywa pombe na kuingia barabarani hawatofika mbali kwa sababu askari wa usalama barabarani wamejipanga kila kona kitendo cha kusema kila mwisho wa mwaka lazima uhalifu utokee hilo halikubaliki."

Kamanda Muliro anaasa jamii kuwa inaposema hivyo maana yake inahalalisha kwamba lazima matukio hayo yatokee, mambo hayo Jeshi la Polisi haliyataki na hivyo vyanzo ameahidi kushughulika navyo kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zake unaimarika.

Kadhalika, amekemea vitendo vya wananchi wenye tabia ya kutoa rushwa kwa askari akisisitiza kuwa wao ndiyo wanao washawishi askari kujiingiza kwenye tamaa hiyo.

"Mtu asipotoa rushwa askari atapokea nini? Kuna askari wetu wengine ndiyo wametoka mafunzo bado wadogo na wao ni binadamu unapo mshawishi kumpa rushwa maana yake unatuharibia askari wetu na sisi tukikukamata tutakuchukulia hatua za kisheria."


Ameonya ikitokea umeombwa rushwa na askari ni bora uende kutoa taarifa kituo cha polisi. Asisitiza jamii kubadili mitazamo na kwamba mtu wa kwanza kabisa mbaya ni mtoa rushwa ndiyo maana jeshi hilo limegawa namba mbalimbali za kutoa taarifa ili mtu anapoombwa rushwa awaseme na pia wale wanaotoa ili vitendo vya kutoa na kupokea rushwa vikomeshwe.

Alichokisema Kamanda Muliro ni muhimu kikazingatiwa kwa sababu wananchi ndiyo walinzi wa kwanza wa wenzao na wao ndiyo wanaowafahamu wahalifu kwa kuwa wanaishi nao kama si jirani zao kwenye mtaa anaoishi. Umoja ni nguvu na ushirikiano huleta maendeleo na kutatua matatizo mengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Polio ni hatari kwa watoto, wazazi tusijisahau sana kama vile haipo

Na Yasmine Protace

**UGONJWA** wa polio umekuwa na sifa ya kuwaachia ulemavu watoto, pale inapotokea hawajapata chanjo, hata kutoa ulazima wa kimazingira kuhusu kinga hiyo.

Maambukizi ya virusi vya polio ambayo huathiri mfumo wa mishipa, unaweza kumsababishia mgonjwa udhaifu wa ama misuli au kupooza. Kinachotokea ni kwamba, mgonjwa anashindwa kusogeza misuli ya mwili wake katika baadhi ya sehemu.

Pia maradhi hayo ambayo sasa yako katika sura ya kutoweka, ni adimu sana kupatikana kwenye jamii, ikilinganishwa na zama zilizopita hadi katikati ya miaka 1970. Hadi sasa, chanjo na tiba yake imepunguza uwepo wa virusi hivyo katika nchi nyingi.

Polio hutokea zaidi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Watu ambao bado hawajapata chanjo, wako kwenye hatari zaidi ya kuambukizwa maradhi hayo.

Wale wanaosafiri au kuishi kwenye maeneo ambayo bado kuna virusi vya polio wapo kwenye hatari zaidi. Virusi vya polio, kitaalamu inafafanuliwa kuwa vinasambazwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kwa njia nyingi.

Ni maradhi yanayosambaa kwa kukohoa, kupiga chafya au kugusa kinyesi. Mara chache sana watu waliopata chanjo kuambukizwa, huwapata zaidi wale ambao hawajachanjwa dhidi ya maradhi hayo.

Dalili za ugonjwa wa polio ni pamoja na homa, koo kuuma, maumivu ya kichwa na misuli kuuma sana. Baadhi ya watu hupata udhaifu wa misuli.

Inafafanuliwa kwamba maambukizi ya polio hayawezi kutibiwa na kitaalamu inaelezwa kuwa, matibabu ya kawaida hudhibitiwa katika ngazi ya dalili tu.

**Dalili za ugonjwa wa polio ni pamoja na homa, koo kuuma, maumivu ya kichwa na misuli kuuma sana. Baadhi ya watu hupata udhaifu wa misuli.**

Matokeo ya hayo, baada ya maambukizi ya polio dalili hutegemea na kiwango, pia mazingira, ndipo namna inavyoweza kumsababishia mtu ulemavu wa kudumu na hata kifo.

Milipuko ya polio hutokea zaidi katika kipindi cha kiangazi. Watu wenye umri wowote huweza kuathirika na hatari zaidi ni chini ya miaka mitano. Watu ambao hawajapata chanjo dhidi ya polio, wapo hatarini zaidi kuambukizwa.

Hivi karibuni mkoa wa Dar es Salaam, ulikuwa katika kampeni ya kuwataka wakazi kujitokeza kwa wingi kushiriki chanjo ya polio kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, kati ya tarehe Mosi na Nne, mwezi huu.

Ofisa Afya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Katikiro, akafafanua: "Lengo la kutoa chanjo hii ni kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo, hasa baada ya wagonjwa kuripotiwa nchi za jirani za Malawi na Msumbiji na hivyo Shirika la Afya Duniani (WHO) likatoa maagizo kwa kuchukua hatua mapema."

Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Dar es Salaam, Hezron Msongole, alifafanua kwamba, ili kufanikisha ; waratibu waandae timu ya watu 474 ya watoa huduma kwa maeneo yote yenye msongamano wa watu, ikiwamo shuleni na masokoni, pia majumbani na kuwataka wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa kuhakikisha watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano wanapewa chanjo hiyo.

Anasema kuwa polio ni ugonjwa unaoathiri mfumo wa neva na husababisha udhaifu wa misuli au kupooza na huathiri zaidi watoto wenye umri chini ya miaka mitano..

## Mahakama yaelezwa vijana walivyokamatwa wakiingilia miundombinu umeme Soko Kariakoo

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeelezwa jinsi vijana watatu walivyokamatwa, baada ya kuingilia miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kusababisha Soko la Kariakoo kukosa umeme Januari 14, 2022 na kupata hasara ya Sh. milioni 316.9.

Vijana hao wametajwa kuwa ni Erick Mahenzilana, Emanuel Daroshi na Baruani Baruani, wote wakazi wa Dar es Salaam na walifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio na kusomewa maelezo ya awali (PH) na Wakili wa Serikali Caroline Matemu.

Akisoma maelezo hayo, Wakili Matemu alidai kuwa, Januari 14, 2022 majira ya alfajiri washtakiwa wote walikuwa ndani ya soko hilo geti namba tano, wakiwa hapo walikamatwa na walinzi wanaolinda soko hilo.

Alidai kuwa baada ya kukamatwa walipekuliwa na walikutwa na misumeno miwili, spana nane, vichwa vya spana vitano, patasi mbili, bisibisi nne, kipande kimoja cha mnyororo, wembe mmoja wa kulanda, plaizi moja, kipande kimoja cha waya vyote vilikuwa ndani ya kibegi chekundu.

Aidha, washtakiwa walikutwa na nyaya walizoweka katika kindoo cha rangi ya njano, walinzi walichukua vitu vyote na kuviwasilisha Kituo cha Polisi Msimbazi kwa hatua zaidi.

Alidai kuwa, hati ya kuhifadhi mali hizo iliandaliwa na vitu hivyo vilihifadhiwa na Sajenti Nowa mbele ya Shabani Mwenda.

Matemu alidai kuwa soko hilo lilikaguliwa na kubainika kuwapo uhalibifu katika mfumo wa umeme na baada ya kufanyika kwa tathmini na mamlaka husika ilibainika kwamba hasara iliyotokea ni Sh. 316,980,333.78.

Alidai washtakiwa hao waliharibu miundombinu ya umeme kwa kukata waya zilizokuwa zinaelekea katika transfoma na mtambo mkubwa wa umeme.

Baada ya upelelezi wa awali, walifikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili. Washtakiwa wote walikana maelezo hayo isipokuwa kukamatwa na kufikishwa Kituo cha Polisi Msimbazi.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 10, mwakani kwa ajili ya usikilizwaji. Upande wa mashtaka unatarajiwa kuwa na mashahidi wanane na vielelezo vinane ili kuthibitisha mashtaka dhidi yao.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania Limited, Araman Benoite, akielekeza namna ya kuwasha mtungi wa Oryx wakati wa mafunzo ya namna sahihi ya kutumia mtungi wa gesi ili kuepuka madhara yakiwamo kulipuka jana. Kampuni hiyo imetoa mitungi 700 na majiko ya gesi kwa Mbunge wa Viti Maalum Kilimanjaro, Shally Raymond. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waomba kuimarishiwa ulinzi kudhibiti ujambazi

**Na Friday Simbaya,**
RUKWA

WANANCHI wa vijiji vya kata ya Kizumbi mwambao mwa Ziwa Tanganyika, wilayani Nkasi, wameomba serikali kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yao kutokana na vitendo vya ujambazi vilivyokithiri.

Wananchi hao walitoa kilio chao kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga katika mkutano wa hadhara uliolenga kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Walisema kuwa, matukio ya ujambazi ya kutumia silaha za moto yamekuwa mfululizo yakiwamo ya kuwapora wavuvi nyakati za usiku.

Pia, walisema tatizo lingine ni mawasiliano ya simu kupatikana kwa shida na kuomba serikali kwa kushirikiana na kampuni za simu kuimarisha mawasiliano hayo ili kuwasaidia wananchi kutoa taarifa za uhalifu na ujambazi kwa wepesi zinapotokea.

Walimuomba Mkuu wa Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi (JWTZ), kuimarisha ulinzi na usalama ili wananchi wafanye shughuli za maendeleo bila hofu, ikizingatiwa vijiji hivyo vipo mpakani mwa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ziwa Tanganyika ni moja ya maziwa makubwa ya Afrika ya Kati likienea mpakani mwa Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Zambia.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa aliwahakikishia usalama wananchi wa vijiji vya mwambao mwa Ziwa Tanganyika ili kukomesha matukio ya ujambazi yanayotokea mara kwa mara.

"Kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu kila ifikapo nyakati za sikukuu kuwaibia na kuwanyang'anya mali na vifaa vingine vya uvuvi wananchi waishio mwambao mwa Ziwa Tanganyika, wale wote wanaoshirikiana au kuwahifadhi wahalifu hao tutawachukulia hatua kali za kisheria," alisema Sendiga. Aidha, aliagiza nyumba za kulala wageni zote zinazofanya kazi zitambuliwe na kuwe na vitabu vya kusajili wageni wote wanaoingia ili iwe rahisi katika ufuatiliaji wa masuala ya uhalifu.

Aliwaonya watu wanaoshirikiana na mnyororo wa kuwahifadhi majambazi kuacha mara moja. Akaongeza kuwa serikali itawashughulikia.

"Nitoe wito kwa jamii kuendelea kutoa ushirikiano kuwafichua wahalifu katika maeneo yetu...," alisisitiza.

Wakati huohuo, RC Sendiga aliitaka Idara ya Uhamiaji wilayani Nkasi kuwajibika na watu wa mpakani kwa kuhakikisha wanaoingia nchini wanakuwa na vibali.

Alimtaka pia Mkuu wa Wilaya Nkasi kushughulikia suala la nyumba za kulala wageni ili kubaini kama zipo kisheria, zisiwe 'gestibubu' ili serikali ipate mapato yake.

"Mkuu wa wilaya, naomba gesti zote zikaguliwe kuona kama ziko kisheria na ziwe na vitabu vya kuandikisha wageni wote wanaolala kwenye nyumba hizo ili kupunguza matukio ya ujambazi...," aliongeya RC Sendiga.

Mkoa wa Rukwa ni mmojawapo kati ya 31 ya Tanzania wenye postikodi namba 55000.

Unapakana na mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi upande wa Kaskazini, Mkoa wa Mbeya upande wa Mashariki, Zambia Kusini na upande wa Magharibi Ziwa Tanganyika lililo mpaka na Kongo pia.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



**HABARI PICHA**

# MAHAFALI YA 18 YA SUZA KATIKA PICHA



Wahitimu wa Cheti cha Uongozi wa Fedha, wakishangilia baada ya kutunukiwa cheti katika Mahafali ya 18 ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana. **PICHA ZOTE: IKULU**



Wahitimu wa Shahada ya Utabibu, wakila kiapo cha utii na uadilifu wa kazi yao, baada ya kutunukiwa shahada.




Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika hafla ya mahafali hayo.



Wahitimu wa SUZA, wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Hussein Ali Mwinyi.



Wahitimu waliotunukiwa Stashahada ya Teknolojia ya Habari na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.



Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi akimkabidhi zawadi mwanafunzi bora wa Stashahada ya Ofisa Tabibu 2021/22 pamoja na fedha taslimu Sh. 300,000, Ummul-Khayr Sadri Abdulla, katika sherehe za mahafali ya 18 ya SUZA jana.

**HABARI KITAIFA**

## Mashahidi sita kusikilizwa, kesi ya kughushi saini

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashtaka unatarajia kuwa na mashahidi sita na vielelezo sita kwa ajili ya kuithibitishia Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa Seleman Maziku, alighushi ridhaa ya mke wake na kujipatia Sh. milioni 140 kwa njia ya udanganyifu.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Caroline Matemu, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa Mahakama hiyo wakati akimsomea mshtakiwa huyo, mkazi wa Kitunda Mwanagati maelezo ya awali (PH).

Baada ya Matemu kumaliza kumsomea PH Maziku, aliieleza Mahakama kuwa katika kesi hiyo watakuwa na mashahidi sita na vielelezo sita ili kuthibitisha shtaka lao.

Akisoma maelezo hayo, Matemu alidai kuwa Desemba 10, mwaka huu, katika eneo lisilofahamika jijini Dar es Salaam, mshtakiwa bila ridhaa kutoka kwa mkewe Skola Bundala, alisaini ridhaa ya mwenza katika mkopo akionesha kwamba umesainiwa na Skola.

Mshtakiwa alichukua ridhaa hiyo na kuwasilisha katika benki ya Stanbic kama moja ya taratibu za benki kitendo kilichosababisha mshtakiwa ajipatie mkopo wa Sh. milioni 140.

Ilidaiwa kuwa Desemba 18, 2022, Skola alifahamu ubadhirifu uliyofanywa na mume wake, Seleman kitendo kilichosababisha Skola kwenda kutoa taarifa polisi na mshtakiwa kukamatwa.

Pia alidai kuwa sampuli za maandishi na sahihi ya mshtakiwa, Skola pamoja na Wakili Castor Rwekiza, zilichukuliwa na kupelekwa maabara ya uchunguzi wa kisayansi wa maandishi kwa ajili ya uchunguzi.

Matemu alidai kuwa katika uchunguzi huo, ilibainika kwamba saini iliyowekwa katika ridhaa ya mwenza wake iliwekwa na mshtakiwa huyo na kushuhudiwa na wakili huyo.

Baada ya kukamalika uchunguzi wa awali, mshtakiwa alifikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili na wakati wa mahojiano alikiri kukopa mkopo huo katika Benki ya Stanbic.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 23, 2023, kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa mashahidi sita wa upande wa mashtaka.

Mshtakiwa huyo yupo nje baada ya kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho na mmoja wa wadhamini hao kuwasilisha mahakamani hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 70.

# Polisi yataja sababu udhibiti uhalifu

**Na Halfani Chusi**

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amesema jeshi hilo limefanikiwa kudhibiti vikundi vya kihalifu (panyaroad), pamoja na kupunguza ajali za mwisho wa mwaka kutoana na ushiriki wa wananchi katika kufichua vitendo hivyo.

Muliro aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, alipozungumza na Nipashe kwa njia ya simu akitaka jamii kufuta dhana ya kuamini kila mwisho wa mwaka lazima yatokee matukio ya kihalifu na ajali nyingi.

"Tangu Septemba mwaka huu, nilisema mambo ya kusema kila ikifika mwisho wa mwaka kuna ajali nyingi au matukio ya kihalifu sasa limefika mwisho, Jeshi la Polisi halitaki watu kuongea mambo ya kufikirika mimi ukiniambia kuna ajali nyingi nitakuuliza hizo ajali ziko wapi? Ukisema uhalifu nitakuuliza hao wahalifu wako wapi?

"Hata wale wanaokunywa pombe na kuingia barabarani hawatofika mbali kwa sababu askari wa usalama barabarani wamejipanga kila kona kitendo cha kusema kila mwisho wa mwaka lazima uhalifu utokee hilo halikubaliki," alisema.

"Wanaposema hivyo maana yake wanahalalisha kwamba lazima matukio hayo yatokee, mambo hayo Jeshi la Polisi haliyataki na hivyo vyanzo mimi nitashughulika navyo kuhakikisha ulinzi wa raia na mali zake unaimarika."

Aliwaonya wananchi wenye tabia ya kutoa rushwa kwa askari akisisitiza kuwa wao ndiyo wanao washawishi askari kujiingiza kwenye tamaa hiyo.

"Mtu asipotoa rushwa askari atapokea nini? Kuna askari wetu wengine ndiyo wametoka mafunzo bado wadogo na wao ni binadamu unapomshawishi kumpa rushwa maana yake unatuharibia askari wetu na sisi tukikukamata tutakuchukulia hatua za kisheria.

"Na hata ikitokea umeombwa rushwa na askari kwanini usikatae au usiende kutoa taarifa kituo cha polisi? Tunataka jamii ibadili mitazamo mtu wa kwanza kabisa mbaya ni mtoa rushwa ndiyo maana tumegawa namba mbalimbali za kutoa taarifa unapoombwa rushwa, kuwasema wanaopokea tu bila kuwataja wanaotoa huko nikuhalalisha," alisema Kamanda Muliro.




Madereva wa pikipiki maarufu bodaboda jana wakiwa wamepanga foleni katika kituo cha mafuta cha TOP Oil stendi kuu ya mabasi wilayani Muheza, mkoani Tanga baada ya mafuta ya petroli kuadimika katika vituo vingine vya mafuta kwa siku ya pili sasa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Walalamika kuendelea unyanyapaa kwa wenye ulemavu

**Na Julieth Mkireri**

WANAWAKE viongozi wa watu wenye ulemavu na baadhi ya wanaharakati wamesema bado kuna hali ya unyanyapaa kwa kundi hilo hususani watoto, tabia ambayo inaanzia kwenye familia.

Hayo yamebainishwa jana jijini Dar es Salaam katika kikao cha wanaharakati wanaotekeleza mradi wa Disability Rights, Inclusion and Gender Equality (DRIGE) kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la ADD ambao walikutana kujadili masuala ya watu wenye ulemavu na hali ilivyo kwenye jamii.

Katika kikao hicho walibainisha kuendelea kuwapo kwa vikwazo kwenye jamii ambavyo vinawakumba watu wenye ulemavu hususani watoto huku ngazi ya familia ikielezwa kuwa chanzo cha kukithiri kwa unyanyapaa.

Joyce Ambros, mmoja wa wanaharakati walioshiriki kikao hicho, alisema bado kuna tabia ya wanawake wenye watoto wenye ulemavu kutengwa kwenye familia na jamii kuwanyanyapaa.

"Wakati mwingine ukienda kliniki na mwanao huku umembeba wanakuambia kabisa hivi hiyo kliniki mwisho lini? Dhana ya kuroga watoto nayo bado iko kwenye jamii wanaamini mtoto akizaliwa na ulemavu amerogwa," alisema Ambros.

Doris Kulanga mwenye ulemavu wa kuona na kiongozi aliiomba serikali kutenga bajeti na kurejesha utaratibu wa kusafirisha watoto wenye ulemavu kwenda shule na kurejea ili kuwaondolea adha watoto ambao wanatoka kwenye mazingira magumu.

Doris pia aliishauri serikali kupitia Wizara ya Afya kuwa na vyumba maalumu vya kujifungulia watu wenye ulemavu, pia waruhusiwe kuingia na wasaidizi ili kurahisisha wanapohitaji kufikisha ujumbe kwa wahudumu.

Aidha, alipongeza Shirika la ADD kwa kushirikiana na wanaharakati na watu wenye ulemavu katika mapambano ya kukomesha ukatili na unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu.

Kandugu Agustino, alisema familia bado hazikubali kupokea watoto wenye ulemavu, ukatili wa majina ya ajabu hasa wanapoenda kujifungua bado unaendelea, baadhi yao pia wanakumbwa na tatizo la kuzuiwa kuolewa au kuoa watu wenye ulemavu.

Naye Hanifa Mbata, mwanaharakati na mzazi mwenye mtoto mwenye ulemavu, alisema serikali imekuwa ikihimiza watoto wenye ulemavu kupelekwa shule, lakini zipo shule zinaendekeza unyanyapaa kwa kundi hilo.

Lupi Maswanya, mwenye ulemavu wa kusikia alisema mara nyingi kumekuwapo na taarifa za unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu, lakini kwa kundi la watoto imekuwa zaidi.

"Wenye ulemavu bado wanatengwa, wanadharauliwa na hii inatakiwa elimu kwenye jamii na ianzie kwa familia watambue mwenye ulemavu ni sawa na wengine anaweza kufanya vitu kama wengine bila kujali hali yake," alisema.

Alisema, mitizamo hasi kwenye jamii imekuwa ikisababisha watu wenye ulemavu kunyimwa nafasi za uongozi, jitihada za shirika hilo la ADD kwa kushirikiana na wengine zikiungwa mkono zitaondoa mitizamo hiyo na jamii itabadilika.

Waliomba elimu zaidi kutolewa kwenye jamii kuwathamini watu wenye ulemavu na kuwapatia haki ya elimu watoto bila kuwabagua.

HABARI KITAIFA

# TPAWU yalalamikia kiwango mshahara kima cha chini

Na Mwandishi Wetu

CHAMA cha Wafanyakazi Mashambani na Kilimo Tanzania (TPAWU), kimelalamikia kiwango cha mshahara kilichoongezwa katika sekta ya kilimo kikisema ni kidogo na hakimwezeshi mfanyakazi kumudu mahitaji yake.

Hivi karibuni serikali iliongeza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa sekta ya kilimo kuwa Sh. 140,000 kutoka Sh. 100,000 ya awali.

Taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Fred Akondowe, ilieleza kuwa jambo hilo haliko sawa kwa sababu mfanyakazi hawezi kumudu maisha yake kwa mwezi kwa kiasi hicho cha fedha ikiwa ni pamoja na malazi, makazi, chakula, elimu na afya.

Alisema wafanyakazi wengi wa sekta ya kilimo kwa kupitia mikataba ya hali bora za kazi wanalipwa kati ya Sh. 162,000 na Sh. 400,000 kama kima cha chini cha mshahara.

"Mfano sekta ya chai kima cha chini wanalipwa Sh. 175,532, mkonge (Sh. 161,928), miwa (Sh. 278,684), maua (Sh. 304,390), misitu (Sh. 215,000), sekta ya mazao mchanganyiko kima cha chini wanalipwa Sh. 200,307."

Alisema katika tangazo nambari 45/2022, serikali ilitangaza viwango tofauti kwa sekta tatu, kwamba katika tangazo la serikali nambari 196 la mwaka 2013 sekta hizo zilikuwa na kiwango kimoja ambazo ni kilimo, ulinzi wa kampuni ndogo na viwanda, zote zilikuwa na kiwango cha Sh. 100,000.

Alisema katika gazeti la serikali namba 45 la mwaka 2022 serikali imepanga viwango tofauti vya malipo katika sekta hizo, kilimo ikiwa ni Sh. 140,000, ulinzi wa kampuni ndogo Sh. 148,000, viwanda Sh. 150,000.

Alisema vyama vya wafanyakazi kupitia TUCTA vilijulishwa kuwa kutokana na umuhimu na uharaka wa kupatikana kwa kima cha chini cha mshahara, sekta binafsi, kima cha chini cha mshahara kitakachotangazwa kitaanza kutumika Julai, mwaka huu na kitakuwa ni kima cha chini cha mshahara cha mpito.

"Lakini kwenye tangazo imetangazwa kuwa kima cha chini cha mshahara kitaanza kutumika Januari 2023 na hatuoni kama kima hicho ni cha mpito na kama kima hicho sio cha mpito basi utaratibu wa kisheria haukufuatwa na hivyo viwango vilivyopendekezwa ni vya kufikirika."

Aliiomba serikali kurudia kufanya mchakato ikiwamo utafiti na hatua zingine za kisheria zitakazosababisha kupatikana kwa kima cha chini cha mshahara kilichofuata utaratibu wa kisheria.



Waziri Mkuu Kivuli wa Chama cha ACT- Wazalendo, Doroth Semi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya Baraza la Mawaziri Kivuli wa chama hicho Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wakili awasilisha kusudio rufani kupinga hukumu uchunguzi kifo

Na Grace Gurisha

WAKILI Peter Madereka amewasilisha kusudio la kukata rufani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni/ Kinondoni, Dar es Salaam kupinga hukumu iliyotolewa na mahakama hiyo kwa sababu haijaeleza namna utekelezaji wa uchunguzi wa kifo Stella Moses, aliyefia Kituo cha Polisi Mburahati, utakavyofanyika.

Desemba 19, 2022 mahakama hiyo ilitoa hukumu katika shauri la madai namba 3/2020 kuwa ufanyike uchunguzi wa kifo cha Stella aliyedaiwa kujinyonga katika kituo hicho cha polisi, baada ya kubaini kifo chake kilitokea katika mazingira ya kutatanisha.

Madereka alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua anazozifuata baada ya hukumu hiyo kutolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo ambayo ilitoa amri ya uchunguzi wa kifo hicho.

Wakili huyo alidai kusudio hilo aliliwasilisha mahakamani Desemba 27, 2022, huku akisubiri mwenendo wa kesi na nakala ya hukumu ili aweze kuwasilisha nyaraka zingine mahakamani.

Alisema anataka kukata rufani kwa sababu hukumu iliyotolewa haijaeleza namna ya utekelezwaji wa amri iliyoitoa ya uchunguzi wa kifo cha Stella.

Hata hivyo, alidai bado hajapata nakala ya hukumu, akiipata ataisoma ili kujua kama kuna amri zote zilizotolewa katika utekelezwaji wa uchunguzi wa kifo cha Stella.

Katika hukumu ya Hakimu Kiswaga, alisema hakuna ripoti yoyote iliyotolewa ya polisi au ya Mkemia Mkuu wa serikali kuonesha kuwa kuna sampuli zilichukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa mwili wa marehemu Stella.

Pia alisema mahakama haijapata ripoti ya taarifa ya kidaktari ya chanzo cha kifo cha Stella, na kwamba maombi ya mleta maombi yana mashiko kisheria ya kutaka ufanyike uchunguzi huru kujua ukweli wa mazingira ya kifo hicho.

"Mahakama inaamuru ufanyike uchunguzi kuhusiana na kifo cha Stella kilichotokea katika mazingira ya kutatanisha akiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi Desemba 20, 2020 katika Kituo cha Polisi Mburahati."

"Na taarifa hiyo itolewe kwa mahakama na sehemu husika na yeyote aliyehusika achukuliwe hatua za kisheria, kwa hiyo maombi ya mleta maombi yamekubaliwa," alisema Hakimu Kiswaga.

Machi 22, 2022, shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo, alifungua shauri dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam (ZPC), Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni (RPC), Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mburahati (OCD).

Wajibu maombi wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akiomba ufanyike uchunguzi huru ili kujua ukweli wa mazingira ya kifo cha shemeji yake Stella.

# H'shauri Nyasa yakamilisha madarasa kidato cha 1

Na Mwandishi Wetu

HALMASHAURI ya Wilaya ya Nyasa imekamilisha ujenzi wa vyumba 12 vya madarasa vitakavyotumiwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza wilayani hapo na kukabidhi kwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Aziza Mangosongo, makabidhiano yaliyofanyika Shule ya Sekondari Limbo, wilayani Nyasa.

Akipokea madarasa hayo baada ya kukagua kwa niaba ya serikali, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Aziza Mangosongo, alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa, Jimson Mhagama, kwa kusimamia ujenzi wa madarasa 12 wilayani hapo na kukamilisha kwa asilimia 100 kwa viwango tarajiwa.

"Nimekagua madarasa yako vizuri yanapendeza na yanafaa kwa matumizi, nakupongeza sana Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa kwa kusimamia vizuri ujenzi huu wa madarasa 12 hakika unastahili pongezi," alisema.

Kadhalika, alisema kukamilika kwa madarasa hayo kutawafanya wanafunzi 4,452 waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kuwa na miundombinu bora ya kujifunzia itakayowapa wanafunzi hao ari ya kujiunga na masomo ya sekondari, wakiwa na madarasa mapya na madawati mapya.

Alitoa wito kwa jamii kuilinda na kuitunza miundombinu hiyo ili iweze kudumu kwa muda mrefu na kuhakikisha wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2023 wilayani Nyasa wajiunge bila kisingizio chochote.

Awali, akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa vyumba hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Mhagama, alisema halmashauri ilipokea Sh. 240,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hayo ya kidato cha kwanza 2023 kwenye shule sita ambazo ni Luhangarasi (3), Kilumba (1), Limbo (3), Mnika Mbega Kata ya Mbaha (2), Nyasa (1) na Liparamba (2).

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipa miradi ya maendeleo Wilaya ya Nyasa ili kutatua tatizo la upungufu wa madarasa ya kidato cha kwanza 2023.

**"Nimekagua madarasa yako vizuri yanapendeza na yanafaa kwa matumizi, nakupongeza sana Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa kwa kusimamia vizuri ujenzi huu wa madarasa 12 hakika unastahili pongezi," alisema.**



# Mradi wa afya yangu, shule yangu kunufaisha vijana 2,000

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya vijana 2,000 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19, watanufaika na Mradi wa Afya Yangu, Shule Yangu, awamu ya pili, unaotekelezwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la DSW-Tanzania, linalojishughulisha na masuala ya maendeleo ya vijana.

Akizungumza jana jijini Arusha, wakati wa uzinduzi huo awamu ya pili, Mkurugenzi Mtendaji wa DSW, Jan Kreuteberg, alisema wamezindua mradi huo kwa awamu nyingine, kutokana na uhitaji wa vijana wengi wanaohitaji kufikiwa na huduma hiyo.

Alisema mradi utatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili (2022/2024), kwenye shule saba za sekondari katika kata saba ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma na utahusu masuala ya stadi za maisha, afya ya uzazi, makuzi na ukatili wa kijinsia kwa vijana walioko kwenye mfumo rasmi wa shule.

"Tutahakikisha tunaendelea kushirikiana na serikali kwa ajili ya kupanua wigo wa elimu ili uwafikie vijana wengi zaidi na kuna baadhi ya mapendekezo ambayo yametolewa na baadhi ya wadau tutahakikisha tunayafanyia kazi kwa lengo la kuboresha huduma zetu," alisema.

Ofisa Mradi wa Afya Yangu, Shule Yangu, Saumu Rajabu, alisema mradi utafanya kazi kwa karibu na wanafunzi (waelimishaji rika) walimu, watoa huduma za afya, wazazi, viongozi wa serikali na wanajamii.

Saumu, alisema matokeo tarajiwa ya mradi huo, yatalenga katika kuboresha upatikanaji wa taarifa za afya ya uzazi kwa vijana balehe, stadi za maisha, huduma za afya rafiki kwa vijana na usaidizi wa jamii, hivyo kuchangia kufikia ajenda ya kitaifa wa kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe.

Alisema mradi huo, awamu ya kwanza uliweza kuwanufaisha zaidi ya vijana 1,000 kutoka shule tano ndani ya kata tano katika Halmashauri ya Dodoma.

Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji la Dodoma, Upendo Rweyemamu, alisema kupitia mradi huo, umewajengea vijana ujasiri mkubwa wa kuweza kujieleza pasipo kuwa na shida yoyote na kuweza kupunguza mimba za utotoni kwa kiasi kikubwa.

Aidha, wanafunzi walionufaika na mradi huo, Joani Lema na Floriana Joseph, walisema mradi huo, umewasaidia kujiamini katika masuala mbalimbali ya afya ya uzazi na kuweza kuokoa vijana wenzao.



Diwani wa Kata ya Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Salome Mnyawi, akizungumza kwenye uzinduzi wa kwaya ya KKKT Sayuni Mtaa wa Oloshonyokie, Kata ya Naisinyai, alichangia Sh. 200,000 juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Nyanza Group yakusanya mil.4.8/- uuzaji fulana, kalenda

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WANACHAMA wa Nyanza Group, katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara wamekusanya Sh. milioni 4.8 kwenye uzinduzi wa fulana na kalenda zao za mwaka 2023.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Malimi Kija, akiongoza shughuli ya uzinduzi huo alisema wanachama hao wamejitoa kuchangia kiasi hicho cha fedha.

Kija alisema kila mwanachama amechangia Sh. 30,000 kwa kununua fulana na kalenda ila wenye kipato kikubwa baadhi yao wamenunua kwa Sh.500,000, Sh. 200,000 na Sh. 50,000.

"Niwapongeze na kuwashukuru wanachama wote ambao kwa namna moja au nyingine mmeshiriki kutunisha mfuko wetu wa Nyanza Group," alisema Kija.

Alisema katika kutunisha mfuko wao wamepata Sh.milioni 4.1 na ahadi Sh.725,000 hivyo kufikisha Sh.milioni 4.8.

Alisema kadiri miaka inavyozidi kwenda ndivyo umoja wao unavyozidi kupiga hatua na kusema Nyanza Group ni kikundi kikubwa cha kuigwa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mirerani, Isack Mgaya, alisema kikundi hicho kimekaa muda mrefu kwa zaidi ya miaka 20 hivyo wanapaswa kupongezwa.

Mgaya alisema baadhi ya vikundi vingine vimekufa kutokana na uongozi mbovu ila Nyanza wamefanikiwa kukaa muda mrefu bila migogoro.

Hata hivyo aliwataka wanachama hao kujihusisha na mikopo mbalimbali ikiwamo inayotolewa na halmashauri ambayo itawawezesha na kunufaika kiuchumi.

Alisema: "Kwenye halmashauri kuna makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu wanapatiwa mikopo, hivyo undeni vitengo vya namna hiyo ili kujinufaisha kiuchumi.

# Mchimbaji tanzanite atoa msaada vifaa wajawazito

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MCHIMBAJI mdogo wa madini ya tanzanite, Charles Mullo, maarufu kichunga, amejitolea kugharamia ununuzi wa vifaa vya kujifungulia wanawake wajawazito ambao hawana uwezo katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Ili kutimiza lengo hilo, jana alifunga safari hadi kwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera na kisha kumkabidhi vifaa 100 vya wajawazito.

Mullo kwa sasa anafanya kazi kwenye migodi ya tanzanite iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani,

Kabla ya kukabidhi vifaa hivyo Mullo alimweleza Dk. Serera kwamba vifaa hivyo vyote vina thamani ya Sh. milioni 2.8 na vitatumiwa mahususi na wanawake 100, ambao ni wajawazito wasiojiweza.

"Wanawake wote wasiojiweza ambao wanafikishwa katika Kituo cha Afya Mirerani wapatiwe vifaa hivi. Mimi kwangu misaada ya kibinadamu ni zaidi ya ibada. Nimeamua kufanya hivi kwa sababu nilifika hapo na nikaona baadhi ya wanawake wajawazito wanavyotaabika kwa kukosa uwezo wa kununua vifaa hivyo, nikaamua nitoe zaka," alisema Mullo.


Akieleza zaidi namna alivyoguswa na uhitaji huo, Mullo, alisema anatambua kuwa kituo hicho kina uhitaji mkubwa, hivyo wadau wengine wa madini na hasa wachimbaji wadogo, wakubwa na mawakala wa madini, wanapaswa kusaidia.

Baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Serera, alimshukuru Mullo, kwa kutoa vifaa hivyo akisema kuwa vitawasaidia wanawake watakaofikishwa katika kituo hicho cha afya.

Alisema alichofanya mchimbaji huyo ni kusaidia jamii na serikali ambayo inapambana kuhakikisha inaondokana na tatizo la vifo vya kinamama na watoto wakati wa kujifungua.

Awali, Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA) Tawi la Mirerani, Rachel Njau, alimpongeza mchimbaji huyo kwa kutoa vifaa hivyo.

Njau alisema mchimbaji huyo ametumia kiasi cha fedha alichokipata kupitia madini ya tanzanite kurudisha kwa jamii, hivyo kudhihirisha wachimbaji wanavyojitoa kwa jamii.





# Wagonjwa 3,000 wapatiwa huduma Kliniki Afrika Amini

**Na Allan Isack,** ARUMERU

ZAIDI ya wagonjwa 3,000 wanaosumbuliwa na magonjwa mbalimbali yakiwamo ya shinikizo la damu, kisukari, saratani ya mlango wa kizazi, tezi dume, uchunguzi wa macho na vidonda vya tumbo, wamepatiwa matibabu bora katika Kliniki ya Afrika Amini inayotoa huduma za afya mchanganyiko za kisasa na asili.

Kliniki hiyo inayotoa matibabu ya asili na kisasa, iko kwenye Kijiji cha Momela, Kata ya Ngarenanyuki wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu huduma za afya zinazotolewa, Mganga Mkuu wa Kliniki ya Afrika Amini, Baraka Barati, alisema kwa wiki wanaweza kuwatibu wagonjwa zaidi ya 260 na kwa siku wagonjwa 70.

Alisema, wanatoa huduma kwa njia mbili ambazo ni za tiba kwa kutumia miti shamba na kwa dawa za kisasa baada ya kumfanyia mgonjwa uchunguzi kwa kutumia vifaa vya kisasa ili kubaini ugonjwa.

"Wagonjwa wanapofikishwa hapa, wanafanyiwa kwanza uchunguzi wa awali ili kubaini tatizo na kuangalia njia mbadala kabla ya kuleta madhara zaidi," alisema.

Sabina Nasari, muuguzi katika kliniki hiyo, alisema wameandaa bustani ya tiba za asili katika eneo hilo kwa lengo la kuisaidia jamii itumie vitu vilivyoko badala ya kutumia vyakula au dawa za kisasa.

"Katika utafiti wetu tumebaini baadhi ya mboga za majani tunazotumia nyumbani, ikiwamo kabeji, tunaitumia kwa wagonjwa wenye maumivu ya viungo.

"Bustani hii inatusaidia kupunguza gharama kwa kuwa dawa tunaandaa wenyewe, hivyo tunakuwa na uhakika wa kile tanachowapatia wagonjwa kwa kuwa tumefanya utafiti wenyewe," alisema.

Vilevile, alisema katika bustani hiyo kuna zaidi ya mimea ya miti shamba 30, ukiwamo wa mlonge unaotumiwa kwa wagonjwa wenye sukari.

Mkurugenzi wa Kliniki ya Afrika Amini, Dk. Cornelia Frisee, alisema amekuwa na uzoefu wa kufanya kazi kama daktari na mtabibu wa tiba za asili kwa zaidi ya miaka 12 na amefanikiwa kuona wagonjwa wengi.

Alisema katika kutekeleza kazi hiyo ya kitabibu, alibaini wagonjwa wengi wanakwenda hospitalini au kwenye vituo vya afya wakiwa wamechelewa sana kupata matibabu ya magonjwa yanayowashambua yakiwa kwenye hatua za mwisho na inakuwa ngumu kutibika.

"Ninapenda kuwashauri Watanzania kutenga siku moja katika mwaka kwa ajili ya kuangalia afya zao hata kama huumwi au huna dalili za ugonjwa kwa kuwa itakufanya kubaki salama na kutunza afya zao," alisema.

Meneja Uendeshaji wa Kliniki hiyo, Mohamed Abbas, alisema kliniki hiyo iliyoko chini ya shirika lisilokuwa na kiserikali la Afrika Amini Alama, mbali na kutoa huduma za afya, imekuwa ikishirikiana na serikali katika nyanja za elimu ikiwamo kujenga miundombinu ya shule na kufadhili wanafunzi wanaotoka katika familia duni.

Alisema, lengo la kuanzishwa kwa kliniki hiyo ni kutoa huduma bure na kwa gharama nafuu kwa wananchi wenye kipato cha chini.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kulia), akizungumza na baadhi ya viongozi wa Mji Mdogo wa Mirerani kuhusu kuepuka migogoro na kutumikia jamii juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mvua yaharibu barabara mamia ya abiria wakwama

**Na Dege Masoli,** HANDENI

ABIRIA zaidi ya 100 kutoka Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga waliokuwa wakielekea mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, wamekwama kwa saa kadhaa katika eneo la Msete baada ya mvua kuharibu barabara na kusababisha kutopitika.

Magari yaliyokwama yalikuwa yanatoka Songe, Wilaya ya Kilindi, Sunya Mkoa wa Manyara.

Wakizungumza na Nipashe jana baadhi ya abiria waliokuwa wakisafiri kwa siku hiyo walieleza kuwa mvua hiyo imesababisha magari kukwama na kufunga njia katika eneo hilo la Msete kwa zaidi ya saa sita, hivyo walilazimika kusubiri.

Mmoja wa wasafiri hao, Aisha Juma alilieleza Nipashe kwamba: "Sisi tumeondoka Songe saa 12 asubuhi mpaka sasa tupo hapa angalia ni saa ngapi hii, karibuni saa nne. Sasa ilibidi muda huu tuwe Korogwe."

Aidha, Joseph Mpira, aliyekuwa akisafiri na moja ya mabasi kutoka Songe kwenda Tanga, alisema hali ya kukwama magari imetokana na ujenzi wa barabara hiyo ambayo imechimbuliwa kuwekwa lami na kwamba malori ndiyo yaliyofunga njia.

Mmoja wa madereva wa malori hayo, ambaye hakutaka kuandikwa alieleza adha waliyokumbana nayo kwamba baada ya kufika hapo majira ya saa saba usiku walikuta magari zaidi ya 10 yamekwama.

Inaelezwa kuwa malori yapatayo 20 na mabasi nane yalikwama eneo hilo kutokana na kukosa sehemu ya kupita baada ya lori kukwama na kufunga njia, hivyo kuwalazimu kusubiri msaada wa kuvutwa kwa gari hilo na kukaa kwa takribani saa sita.

# Serikali za vijiji, mitaa zapigwa 'stop' uuzaji viwanja kiduchu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI mkoani Arusha, imeagiza serikali za vijiji na mitaa, kuacha kugawa viwanja vya ujenzi wa makazi vyenye ukubwa chini ya mita za mraba 450 hadi 500 ili kurahisisha utoaji wa huduma kwenye nyumba hizo yanapotokea majanga ya moto.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Mkoa wa Arusha, Idrisa Kayembe, alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha kutoa mafunzo juu ya ulipaji wa kodi ya ardhi.

Kikao kazi hicho kilichofanyika jijini Arusha, kiliwakutanisha wenyeviti wa serikali za vijiji na mitaa wa Wilaya ya Arumeru na Arusha.

Kamishna huyo alisema wenyeviti hao wanaowajibu wa kupanga miji katika maeneo yao kwa kuhakikisha wanapogawa viwanja viwe kwenye ukubwa huo na siyo chini ya hapo.

Alisema ukubwa huo utaruhusu nafasi kati ya nyumba na nyumba kwa ajili ya usalama wa nyumba hizo hasa kunapotokea majanga ya moto pamoja na miundombinu ya majitaka, huduma ambazo zinakuwa ngumu kupatikana kwa kukosekana kwa nafasi.

"Tukiwa na nyumba zilizopangwa vizuri ni rahisi mamlaka za serikali kutoa huduma wakati wa majanga yanapotokea kwa kuwa yanasababisha vifo na hasara kwa watu," alisema Kamishna Kayembe.

Hata hivyo aliagiza watu kugawa viwanja vya ukubwa unaoeleweka na visiwe vidogo ili vizingatie michoro ya mipango miji kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanakaa kwenye maeneo yaliyopangwa na kupangika.

Akizungumza kwa niaba ya wenyeviti hao, Mwenyekiti wa Mtaa wa Siara, Simon Mollel, aliwaomba wataalamu wa ardhi kuhudhulia kwenye mikutano ya vijiji ili kutoa elimu ya namna bora ya mipango miji inayoendana na huduma zinazotakiwa kwenye makazi.

"Tunapofanya mikutano ya kujadili masuala ya ardhi, tunahitaji wataalamu wa ardhi, afya, maji, umeme, zimamoto na wa mazingira ili waweze kuelimisha wananchi kufahamu utaratibu wa mamlaka zote, kwa kufanya hivyo tunaweza kupanga miji yetu bila kuchanganyana," alisema.

Alisema endapo kutakuwa na mpango miji itakuwa njia ya kuleta na kuchochea maendeleo kwa mwananchi mmoja mmoja kwa kupatikana kwa urahisi huduma muhimu za kijamii.




Ukurasa 15

**SHULENI HADI MAJUMBANI...**
**Simulizi zenye ukakasi, madhila jinsia yanavyowaangukia watoto kila waliko**



**Ugonjwa wa mtu anawehuka kihisia, anashindwa kuizuia dhamira ngono**

Ukurasa 16

# Akerwa uharibifu mazingira, anuia kupanda miti milioni tano kijijini

• Kila mwezi 2,700; azama mfukoni Mil. 11/-

**Na Mwandishi Wetu**

NI kwamba ameamua kujitosa kuimaliza kazia kuwa mwanamazingira wa ukweli, tena kwa vitendo, Adama Diémé (48), mwanaume raia wa Senegal, amejiwekea dhamira kupanda miti milioni tano katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kwa lugha rahisi ni ajenda ya kupanda miti milioni moja kila mwaka, au kila mwezi miti 2,740, hali kadhalika wastani wa miti isiyopungua 90 kila siku.

Ni wazo la mradi uliomjia pale aliporudi nyumbani eneo la Casamance mwaka 2020, baada ya kufanya kazi barani Ulaya.

Mwanaume huyo alishangaa kwamba vijiji ambavyo vilikuwa na mamia ya miti mikubwa katika ujana wake, ni michache tu sasa imebaki, ikamuuma sana.

Katika baadhi ya vijiji analaumu mtu hawezi kupanda hata mti mmoja, akilalamika wanakata, lakini hawafikirii kuupanda tena. Ni kilio anachosema kinatawala Afrika nzima haya kushuhudiwa jangwa.

Anasema, kando ya eneo kubwa la Mto Casamance, miti hiyo ina uwezekano mkubwa wa kukatwa kwa madhumuni ya ujenzi kama vile nyumba, au kuchoma mkaa.

Diémé, ambaye sasa ni Meneja wa Mradi katika shirika lisilo la kiserikali la huko kwao, huku akiwa mzalendo anayejitolea ukufunzi wa kilimo kwa kinamama kijijini, ameazimia kubadilisha hali aliyoikuta.



Adama Diémé (kushoto), akiwa kijijini kwao na mbegu ya miche ya miti anayotarajia kuipanda. Fulana aliyovaa ni sare ya kampeni hiyo aliyobuni kutumia mafundi cherehani kijijini kwao. **PICHA: MTANDAO**

Akiwa hana akiba kubwa ya mali, anasema alianza kuchangisha pesa ili kutimiza ndoto yake na ametumia Dola za Marekani (Sh. milioni 11.750) za kutoka mfukoni mwake kuanzisha mpango huo.

Amekuwa akifanya kazi kwa kushirikiana na jamii zinazozunguka kufikia wanawake ambao alijua wangeweza kumsaidia kuandaa upandaji kwa wingi miche.

"Unaenda katika kijiji na hakuna wanawake, ni janga," Diémé analamika akiendelea:"Lakini ukienda kwenye kijiji chenye wanawake pekee, ni paradiso wanafanya kazi kwa bidii na wanafanya kazi siku nzima kila siku. Ikiwa unataka kuongoza mradi mzuri anza na wanawake."

Alichokifanya ni kuunganisha mradi wake wa kupanda miti kwa kuwasaidia wanawake kupata ujuzi wa kuwa wakulima wadogo na kuuza mazao yao katika masoko ya ndani.

"Mwanzoni, hatukujua jinsi ya kupanda mbegu na nini cha kufanya ili kukuza mazao," mmoja wa wanawake, Safi Yetou, anamsifu.

"Sasa tuna kila aina ya matunda ya kuuza sokoni na hatumtegemei mtu yeyote. Sote tuna akaunti katika benki sasa na hakuna mtu anayeweza kuniambia ninachoweza au nisichoweza kufanya. Ni vizuri."

Mradi huo wa Diémé unajulikana kama Ununukolaal, jina ambalo katika lugha ya kienyeji linamaanisha "Miti Yetu".

Kuna aina 12 ya miti inayopandwa ikiwamo mitende na limao, kutegemea na hali ya ardhi na mahitaji ya jamii. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, alishapanda zaidi ya miche 142,000 imetunzwa na kuota mizizi.

Mshirika wake, Yolanda Pereñiguez, anayefanya kazi ya ufundi cherehani kijijini, amekuwa muhimu katika kusaidia kupanga fedha kwa kubuni fulana inayouzwa nje ya nchi kwa dola 15 (Sh. 35,000), akiwa na Raymonde Coly, anayefanya kazi katika karakana ndogo yenye cherehani mbili ili kuzitengeneza kutoka kwa nguo za kienyeji, zenye picha ya kipekee ya mbuyu. Kila moja inayouzwa inaweza kulipia miche 15 ya miti.

"Nilichagua mbuyu kwani ni alama ya mti wa Kiafrika," anasema Periniguiz, akifafanua: "Inapendeza kujua kwamba fulana hizi zinakwenda duniani kote, Ulaya na hata Canada kusaidia mradi wa miti."

Miaka 10 iliyopita, viwango vya ukingo wa maji ulikuwa mbali zaidi na kufika kijijini hapo ambako ni kisiwa, isipokuwa katika kilele cha msimu wa mvua. Sasa ni hali ya kukata tamaa na ikiwa inaweza kumaanisha kuwaacha wakazi bila makazi.

"Tumeishi katika kisiwa hiki kwa mamia ya miaka, lakini kama maji yanakuja zaidi tutalazimika kuondoka na kutawanyika kila mahali," Conakry Bassene, kiongozi wa kijiji.

Miti ya mbuyu, ambayo inaweza kuishi ardhini na kwenye maji yenye chumvi au majisafi, sasa imepandwa kando ya ufuo kama kizuizi. Miche hupiga upepo, kwa ahadi ya matunda siku moja na hata kivuli. Miti inaweza kutuokoa," anasema Bassenem, akifafanua "Miti, ndio tumaini letu la maisha."

***Kwa mujibu wa BBC.***

AFYA

# Kibaha wapambana binti asiolewe umri mdogo, ili asidhurike kiafya

**Na Julieth Mkireri**

SUALA la ndoa za utotoni ni kitu ambacho kimekuwa kikielezwa kuwa kikwazo cha baadhi ya wasichana kufikia ndoto zao na badala yake, kufuata matakwa ya wazazi wao.

Kitendo cha msichana kuingia kwenye ndoa akiwa na umri mdogo, kinatajwa kuwa sababu ya baadhi ya familia kutokuwa na uhusiano mzuri wa ndani, kutokana na hali ya kukinzana na baadhi ya mambo yanayowahusu.

Stephen Joseph, mkazi wa Kibaha mwenye vidokezo kuhusiana na ndoa hizo za utotoni anasema kuwakatili walengwa ambao hasa ni watoto wa kike, pia kunasababisha familia kujikita zaidi kwenye kusuluhisha msuguano, badala ya kujielekeza kwenye mengine ya maendeleo.

"Mfano, binti ameolewa akiwa na umri mdogo, akafika mtaani kwake kuna watoto wana umri kama wake wakicheza 'rede' nje na yeye anakwenda, mume wake akimkuta hajafanya baadhi ya majukumu, wanagombana na kwa kuwa umri wake kuna vitu alivivuka, basi atamwambia kama umenichoka nirudishe kwetu bila ya kujua anachofanya si sahihi.


"Haitaishia hapo siku nyingine atarudia, sasa watakuwa na kazi ya kupelekana kwenye vikao vya usuluhishi kwenye familia. Kwa hali hii, hawawezi kujadili masuala ya maendeleo na baadaye umri umeenda sasa, wanakumbuka walichelewa wapi," anasema Joseph.

Maoni yake ni kwamba, ili jamii ikabili hali hiyo, ni vyema taasisi zinazojihusisha na masuala ya watoto zikajikita kutoa elimu vijijini juu ya madhara ya ndoa za utotoni, kwa wazazi na shuleni waliko watoto hao.

Joseph anaeleza namna vituo vya msaada wa kisheria vinavyotakiwa kuchukua jukumu hilo, badala ya kujikita kuelimisha zaidi masuala ya haki kwenye mirathi na majukumu ya huduma kwa wazazi wasiozingatia huduma kwa watoto wao.

Zainab Kassim, mkazi wa Kibaha anashauri namna ya kukomesha uwapo wa ndoa za utotoni kwenye jamii, kwamba serikali inatakiwa kuandaa kampeni maalum, badala ya kuacha kazi hiyo kufanywa na mashirika na taasisi zinazotetea haki ya mtoto.

"Msichana kuozeshwa akiwa na umri mdogo, huu ni ukatili na hili linatakiwa kukemewa kuanzia ngazi ya kijiji, ambako matukio hayo yanafanyika. Tusiyaachie mashirika binafsi peke yake, huu ni wakati wa mtoto wa kike kuthubutu kujua haki zake na kuzipambania," anasema Kassim.



Humphrey Munuo wa Kituo cha Msaada wa Kisheria Kibaha akitoa elimu kwenye moja ya shule zilizoko Kibaha. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

Nipashe ilikutana na Humphrey Munuo wa Kituo cha Msaada wa Kisheria Kibaha, anayeeleza namna wanavyotoa msaada kwenye eneo la ukatili na elimu kwenye mapambano ya ndoa za utotoni.

Munuo anasema katika kituo chao wamekuwa wakitoa elimu kuhusiana na masuala ya ukatili, sheria ya mtoto, mambo ya mirathi, pia sheria ya ndoa inayotolewa kwenye makundi mbalimbali.

Anasema marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1977, tayari wameshatoa mapendekezo yao katika mustakabali wa kumlinda mtoto wa kike. Munuo anaeleza, katika elimu wanayoitoa kwa jamii, ni pamoja na: Ufahamu kuhusiana na mila potofu zilizopitwa na wakati, ambazo bado zinaendelezwa na zimekuwa vikwazo kwa mtoto wa kike.

Munuo ananena kwamba, kituo chao kinaamini kupitia elimu wanayoitoa itasaidia kuleta mabadiliko kwa mtoto wa kike, hususani kuanzia kwa wazazi na walezi wa watoto akiamini kwa kipindi cha mwaka uliopo 2022, wameweza kuzifikia shule mbalimbali za msingi zilizopo katika wilaya ya Kibaha, kwa ajili ya kutoa elimu hiyo na zaidi ya wanafunzi 3,762 wamefikiwa.

"Jamii kupitia makundi mbalimbali tunaielimisha kuhusu madhara ya ndoa za utotoni, kwakuwa ndoa hizi zinafungwa kwa siri, tunawapa uelewa na kuwasisitiza kuwa na ushirikiano na kituo chetu pale, wanapobaini uwapo wa ndoa inayofungwa ambayo inamkatili mtoto wa kike," anasema Munuo.

Lingine analosema, katika kituo hicho wamekuwa wakipokea kesi nyingi zinazohusiana na matunzo ya watoto, anasema wapo wazazi wanakwepa majukumu yao na wengi kuwaachia akina mama pekee suala la malezi na matunzo jambo linaloendelea kumkandamiza mwanamke.

"Katika kesi hizi hasa kundi linaloongoza, ni madereva wa bodaboda ambao wengi wao wamekuwa wakiwapa wanawake mimba na kukwepa majukumu," anafafanua, Munuo, anayedokzea kuwapo kwa kundi la wanawake wanaofika kuomba msaada wa kisheria, kutokana na kutosaidiwa matunzo na waliozaa nao na kwa mujibu wa Munuo, wanawake wenye umri kuanzia miaka 20 hadi 30 wako juu katika kutelekeza watoto kulelewa na bibi zao.

"Kutokana na hali hii tumekuwa tukiyafuata makundi mbalimbali kule yaliko kuwaelimisha haki zao kisheria na moja ya makundi hayo ni madereva boda, mamalishe na wajasiriamali wengine," anaeleza.

"Wapo ambao wameanza kubadilika na kupata uelewa kuwa suala la matunzo kwa mtoto sio hiari ni jukumu lao. Tunaendelea na utaratibu wetu wa kutoa elimu kwenye makundi hayo na kuwapa msaada wa kisheria," anasema.

Katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili, kituo hicho kinashirikiana na mashirika mengine kutoa elimu kwenye jamii, hususani katika shule za msingi na sekondari.

Akiwa mjini hivi karibuni, Mwanasheria wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) Tanzania, Zakia Msangi, anaeleza kwamba uanzishwaji wa madawati kwenye shule na makundi mbalimbali ya jamii, kunasaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Msangi, madawati hayo yataundwa kwa kushirikiana na walimu wa malezi kwenye shule na yatakuwa yakitoa elimu kuhusiana na kupambana na ukatili wa kijinsia, pia kutoa taarifa za vitendo hivyo kwenye vyombo husika, ikiwamo dawati la jinsia na vyombo vingine vya sheria

Msangi anasema, katika shule kutakuwa na wanafunzi wawili vinara watakaokuwa na ujasiri wa kujieleza na wenye usiri, pia kutaundwa sanduku la siri la kutoa maoni.

Mkurugenzi wa Kituo Cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC), Catherine Mlenga anasema, wamekuwa wakipokea wateja wanaofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Mlenga, wamekuwa wakishirikiana na vyombo vya kisheria ikiwamo polisi na mahakama, katika kupambana na vitendo hivyo kwenye ngazi za wilaya na mkoa mzima wa Pwani, huku wakitoa elimu kwenye maeneo na makundi ya kijamii.



Wanafunzi wakijuzwa kuhusu usalama ikiwamo afya ya uzazi. **PICHA: MTANDAO**

AFYA

## SHULENI HADI MAJUMBANI...

# Simulizi zenye ukakasi, madhila jinsia yanavyowaangukia watoto kila waliko

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MIAKA ya nyuma shuleni kulijulikana eneo salama kwa watoto na wazazi wengi walipaamini. Hadi sasa kuna walakini unaojitokeza, kutokana na matukio mengi yasiyo ya kibinadamu, ikwamo ulawiti wa watoto wanapokuwa ama shule au njiani wakirudi nyumbani na imefikia wakati wanafunzi kukutana na unyama huo kwenye mabasi ya shule (school bus).

Mengi yayoripotiwa nchini katika maeneo ya shule; viwanja vya shuleni, vyooni, kwenye mapagala na njiani wanaporudi au kwenda shule.

Jijini hapa eneo la Miyuji kunadaiwa kuwapo mikasa ya watoto saba wenye umri kuanzia miaka mitano hadi 10 walilawitiwa, huku wazazi wakitajwa kuchangia hali hiyo. Mzazi wa watoto wawili, Abbas (siyo jina lake halisi) alikumbwa na madhila hayo, anasimulia alibaini hilo kupitia taarifa ya kuwapo kijana aliyewazidi umri wavulana hao kati ya wanne na watano, akiwachukua na kuwapeleka kwao, hata akawalawiti.

"Pale kwao anaishi yeye, kaka na mama yake na kwa sababu mama yake huwa hashindi nyumbani anarudi jioni, hivyo anawapeleka watoto wale kwao anawaweka mikanda 'CD' za picha chafu za uchi, wanaangalia wakimaliza huwa anawafanyia vitendo vya ajabu... na baadae kuwalawiti," anasimulia Abbas.

"Baada ya kupata taarifa hizo sikuamini, ilibidi niwachukue watoto niwaonye kwa kuwapiga, maana niliwaita nikawauliza hawakusema, nilipowapiga wakasema ukweli kuwa huwa wanafanyiwa vitendo hivyo," anasema

Hussein anaeleza kwamba, akaamua kumtafuta mama wa kijana huyo akamkosa, lakini baadaye alipomkuta, mama huyo alikana kujua lolote kuhusu hilo. Anaendelea kusema: "Mama yule akasema tuite wazazi wa watoto waliofanyiwa vitendo hivyo, wakakusanyika nyumbani usiku wakawa wameongea, wakasema watakutana kwa balozi, sijui mpaka sasa wameongea nini."

"Ukishindwa kumdhibiti mtoto, maana baada ya kufanyiwa kitendo hicho inakuwa hatari, anaweza kuharibika ikawa hata ukimdhibiti, ataendelea maana kimeshamuathiri, lazima atarudia kufanya. Hivyo, wazazi tunaweza kuwapoteza vijana wetu, maana hawi mwanaume aliyekamilika, anaweza kuwa shoga tofauti na hivyo hata nguvu kazi ya taifa inakuwa imepotea," anasema

Kiongozi wa mtaa wanakoishi watu hao, Boniface Kadebe, anakana kuwapo au kusikia kwa aina hiyo ya tukio tangu aingie kwenye nafasi hiyo, huku mzazi huyo anasisitiza kwamba walipohoji watoto hao, wakakiri kutendewa na kulipwa shilingi 500 na hata walipowadadisi namna walivyopokea madhila hayo, wakabaki kimya.

Abbas anasimulia, hata walipofikia hatua ya kuwapa elimu watoto kuhusu madhara ya tukio hilo kuwa ni kinyume na maumbile ya kibinadamu, hivyo kuna walakini mkubwa akaongeza: "Ni sawa na fundi ambaye ametengeneza mlango unaofungika kwa nje, wewe unalazimisha ufungike kwa ndani, hivyo kuharibu bawaba au kuupasua kabisa."

Aidha, kiongozi huyo aliyejipa wasifu wa kijamii, anaeleza namna wanavyopinga mambo yanayofanana na hayo katika eneo lao, akinuia kuhakikisha watoto hao wanataja wenzao, huku akihoji kulikoni watendwa hawakuyasema hayo kwa wazazi wao.

"Wengine wapo chekechea, darasa la kwanza, darasa la tano na kidato cha kwanza. Tulipochukua fimbo wakaanza kutajana, wakasema huwa wanafanyia vyooni, mapagalani au wanapocheza mpira..."anasema

Vilevile, anasema walipowahoji wazazi, walibaini kuwa wapo baadhi hawaishi na waume zao walishaachana na mazingira ya nyumba ni chumba kimoja chenye pazia tu, hivyo wanapoingiza wenza wao watoto huwa wanawaona.

"Sasa anapoingia na mwenzake matendo yanayofanyika watoto wanayaona, hivyo malezi yamechangia kuharibu watoto wale, maana vingine vilisemekana huwa wanachungulia bibi na babu wakiwa chumbani,"anasema

"Tumegundua kuwa hao wazazi wamechangia kuleta mmomonyoko wa maadili na kama ni hatua kali lazima nao wachukuliwe, maana ni chanzo cha tatizo hili," anafafanua.

**KAMANDA OTIENO**

Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma, linasema limeweka mikakati ya kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Akimaanisha hasa kwa wanafunzi wa shule za msingi, ambako kumeshika kasi hivi karibuni.

Kamanda wa Mkoa, Martin Otieno, katika taarifa yake anasema wamepanga kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya vitendo hivyo, ili kuihamasisha jamii ibadilike, akifafanua "tutakwenda katika maeneo ya nyumba za ibada, shule, sokoni, nyumba kwa nyumba na hata katika vyombo vya usafiri kutoa elimu kwa kushirikiana na dawati la jinsia mkoa."

Anaeleza moja ya matukio yanayoripotiwa mara nyingi mkoani Dodoma ni ubakaji, hivyo anatoa wito kwa wananchi kutoa taarifa dhidi ya uhalifu wa aina hiyo na nyinginezo.

Hata hivyo, anaeleza kuhusu tukio la watoto saba kulawitiwa bado hawajapata taarifa rasmi, lakini wanalifanyia kazi kupitia vyanzo mbalimbali.

**KUTOKA KWA WADAU**

Mkazi wa jijini Dodoma, Michael Mwafute anasema, ili kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini, kila mtu anapaswa kujiweka mbali, akieleza; 'Hivi sasa matukio ya ukatili kijinsia yamekithiri sana, kila unaposikiliza vyombo vya habari unasikia mtu kamuua mke wake au kiongozi wa dini kamlawiti mtoto hii yote ni kukosa hofu ya Mungu."

Wakati Dk. Geofrey Chambua, mchambuzi wa Jinsia kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), akiiasa serikali kuchukua hatua kukomesha matukio hayo, Mratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) Taifa John Mwanga anasema, takwimu za uhalifu na usalama barabarani kutoka polisi, kati ya Januari na Septemba mwaka huu, zinabainisha yaliyoongoza ni yahusuyo watoto.

"Matukio ya ulawiti yalikuwa 1,044 ambayo kwa watoto wa kike ni 166 huku wakiume ni 878. Kuwapa mimba wanafunzi ni 1,115, lugha ya matusi ni 1,858 kati yake watoto wa kike ni 1,082 huku wa kiume ni 776,"anafafanua, huku akitaja katika mashambulio 3,100; ya kike ni 1,966 ya kiume ni 1,134; Matukio ya kujeruhi watoto ni 2,141 ambayo kati yake wa kike waliojeruhiwa ni 1,048 huku wa kiume ni 1,093,"anafafanua.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi maalum, Simon Magesa, anasema: "Kuna sheria ambayo inasema kuwa kama mtu akimbaka mtoto chini ya miaka 10 anafungwa maisha, lakini akimbaka mtoto wa zaidi ya miaka 10 ni kifungo cha miaka 30, lakini bado watu wanafanya matukio haya, sasa inabidi tuangalie na tatizo la afya ya akili katika jamii zetu."

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, naye ana maoni kuwa: "Serikali haitamuacha salama mtu yeyote ambaye atabainika kutuharibia watoto kwa kuwafanyia vitendo hivi vya kinyama, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao."

"Kuna mafanikio yamepatikana kwenye utekelezaji wa mpango, hata hivyo ni muhimu kujiuliza kwanini vitendo vya ukatili bado vinaendelea kutokea licha ya jitihada mbalimbali za serikali na wadau," Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum, Dk.Zainabu Chaula, anahitimisha.






Wanafunzi katika picha tofauti za mijumuiko inayowahusu. Ni haki inayoaswa kuendana na ulinzi wao muda wote. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

# Ugonjwa wa mtu anawehuka kihisia, anashindwa kuizuia dhamira ngono

**Na Christina Mwakangale**

NI mara nyingi kwenye redio, mitandao ya kijamii, hata kuona televisheni, taarifa kuhusu ubakaji, ulawiti dhidi ya watoto hutokea kwa ndugu wa karibu na hata familia. Mikasa ya kubaka sasa imetawala kwingi, nchini na hata nje ya mipaka.

Wataalamu wa afya wanawatambua watu hao ni kati ya wanaoshindwa kuzuia hisia zao kimapenzi, hata ndugu wa karibu. Hivi karibuni mkoani Manyara, mtuhumiwa kuhukumiwa kifungo cha miaka 30, baada ya kutiwa mbaroni kwa kosa la kumpa mimba mtoto wake wa miaka 16.

Mtuhumiwa amekiri mahakamani kutenda kosa hilo, akidai kufikia uamuzi huo, kwani hakutaka maana huyo aolewe kutoka jamii ya ambayo hakuipenda. Kimsingi, ni hoja inayoangukia katika kile wataalamu wa afya wanaifafanua kwa ugonjwa unaoitwa 'nymphomania', wagonjwa wanakosa udhibiti wa tabia zao binafsi za ngono.

Ugonjwa 'nymphomania' au kwa Kiswahili uraibu wa kufanya ngono au kujamiiana, unawafanya wanaougua kuwa na matatizo ya hamu ya ngono iliyopitiliza wanakosa udhibiti wa tabia zao binafsi katika hulka hiyo ya ngono.

Shirika la Afya Duniani (WHO), baada ya tafiti nyingi, mwaka 2018 ilitambua kuwapo hulka ya ugonjwa huo wa mhusika anashindwa kudhibiti hisia binafsi.




Bosi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus wa Ethiopia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### TATIZO LILIPO

Vigezo vya uainishaji ugonjwa huo, vinatajwa kuwa ni pamoja na watu kupoteza udhibiti wa tabia zao, hata wanapojitahidi kuachana na tabia hizo za ngono, lakini wanashindwa kuacha. Ni watu wanaokosa furaha na kutokana na uzoefu ulioko na madhara makubwa katika maeneo mbalimbali ya maisha yao, kwa zaidi ya miezi sita.

WHO inaelezea kwamba, ni tatizo lisiloishia kwenye hukumu ya maadili, yaani, ukweli ni kwamba mtu haoni kama ni tabia nzuri au isiyo nzuri kimaadili. Kwa wanaougua, hujitahidi kuacha tabia hizo ambazo hulazimisha mtu kufanya matendo hayo.

"Ngono imekuwa kama wasiwasi kwangu. Kila wakati nateseka na siwezi kuendelea tena na hali hii, kufanya ngono kumekuwa kimbilio langu," anatamka mgonjwa mwenye umri miaka 45, akifafanua ni kawaida yake kuchunguza jinsi wagonjwa wa tabia ya ngono wanavyokuwa na picha za ngono, ukahaba, kuwa na mazungumzo ya ngono kila wakati, ama na mtu moja kwa moja au kwenye mitandao ya kijamii, ili kudhibiti ulimwengu wao wa mapenzi.

Wakati wagonjwa walio na matatizo hayo hawajui jinsi ya kusimamia hisia zao, wao huenda kupata ngono ni namna ya kujipatia utulivu, ingawa kuna utafiti unaendelezwa zaidi kujua mengi ya ziada kuhusu eneo hilo.

Hadi sasa inatajwa kuwa ugonjwa huo unaathiri takriban asilimia 10.3 ya wanaume na asilimia saba ya kinamama, kulingana na marejeo ya kitabu "Compulible Sexual Behavior: A Comprehensive Look. A Guide for Professionals."

### ATHARI ZAKE

Ni namna gani inaathiri? Inaelezwa, ni kwenye njia ya kufikiri na kuelewa ngono ni potofu na inapoteza heshima binafsi, hata kujiamini, hisia ya kutokuwa na uwezo, mabadiliko ya ustawi wa kiroho, adha binafsi, udhalilishaji au dharau, aibu, kujihisi kuwa na hatia na ukosefu wa maendeleo ya utambulisho binafsi.

Kiuchumi, inaangukia kukosa hata ajira, matumizi mabaya ya fedha, ulaghai na udanganyifu.

Uhusiano na wengine; inatajwa ni hali ya mtu kupoteza imani kwa wengine, matatizo katika uhusiano binafsi na wengine, kutengwa na jamii, kushindwa kuwa na upendo kwa wengine, kuvunjika ndoa au mpenzi na kupoteza urafiki. Kitabibu. Kuna kupata magonjwa ya zinaa na uhusiano wa kimwili usiofaa kiafya, magonjwa ya akili na hali mbaya ya afya.

Wengine wanatajwa wanakumbwa na matatizo ya kisheria kama vile kukamatwa na kushtakiwa kisheria kwa jinai kuhusu ngono, mathalani nchini Tanzania kesi mbaya za ngono, tabia ya kutowajibika hata kwa jamii, mkengeuko wa malengo muhimu, kufukuzwa kutoka mashirika, vyama na kuzorota kwa taswira ya umma.



Wenza wakijadiliana jambo, katika mazingira jirani.

### DALILI ZAKE

Ugonjwa huo unaweza kugunduliwa na tabia kadhaa, mojawapo ni kupoteza hamu. Utafiti zaidi kwa mfumo wa neva na jinsi ubongo unavyofanya kazi zimeonyesha kwamba matatizo ya tabia ya ngono yanayoshurutisha yanaonyesha mabadiliko yanayofanana katika ubongo na yanayosababishwa na uraibu wa vitu vingine au tabia.

Hisia za mtu kupata furaha, zinaweza kukosa nguvu kwa kukosekana udhibiti wa ngono, hivyo atakuwa wa huzuni au kero. Pia kwenye maeneo ya ubongo, hali hiyo inatajwa inadhibiti, inapanga, makini na kujali kubadilishwa kama inavyoonekana katika tafiti hizo za karibu.

Lingine linatajwa ni kutokuwa na uwezo wa kujidhibiti katika hisia kama vile kwenye hasira, wasiwasi, utendaji kazi wa kiwango cha chini au masomo na matumizi zaidi ya vilevi kama pombe, tumbaku na hata bangi.

Kuna namna inatajwa, mtu anashindwa kudhibiti hisia binafsi, huku kunakosekana utulivu kwa wanandoa, pia uaminifu na hamu kidogo ya ngono na mpenzi binafsi.

### TIBA IKOJE?

Kitaalamu, inatajwa kuwapo njia za kupata suluhu ni ndefu na inahitaji uelewa, motisha, nguvu, msaada, uvumilivu, mapenzi, msaada na kujitoa kwa namna nyingi.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwapo matibabu tofauti yenye ufanisi yameonyeshwa kuwasaidia watu hao, ikiwa ni pamoja na matibabu binafsi na matibabu yanayotolewa wakati mwingine dawa.

Matibabu hayo husaidia kudhibiti tabia na msukumo, pamoja na kujali afya ya uzazi na kuishi maisha huru. Pia kuna baadhi ya mafunzo yanayoweza kusaidia kumwongoza mtu kuangukia uamuzi sahihi dhidi ya kuwehuka na ngono.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale***

AFYA

# Hili ndilo zao mwani, linavyobeba lishe inayoboresha afya ya mlaji

Na Mwandishi Wetu

KATIKA miaka ya karibuni sehemu nyingi hasa ukanda wa baharini, kumeibuka kilimo cha zao la mwani. Jumapili iliyopita katika gazeti hili kulikuwapo na makala maalum ya kilimo cha zao hilo kilivyoshika kasi katika pwani ya Unguja.

Ila katika ujumla wake, kunabaki ufafanuzi nini manufaa yake? Hapo ndio inapotoa jibu lenye viashiria vingi kiafya kwamba "pamoja na kuwekwa kwenye juisi au supu kwa ajili ya kula, mwani pia hutumiwa katika bidhaa za utunzaji wa nywele, virutubisho vya lishe na vitoweo."

Hivi karibuni katika mitandao ya kijamii, wataalamu wa lishe wamekuwa wakishawishi watu kujumuisha mwani katika milo yao, wakisema una faida nyingi kwa afya. Na baadhi wakiibatiza kama 'super food' kwa maana ya mlo wa daraja la juu.

**JE, MWANI NINI?**

Aina ya mwani wa bahari (Chondrus crispus)' unaoliwa unatajwa uko katika pwani ya Atlantiki, Ulaya, Amerika Kaskazini na pwani ya Afrika.

Inatajwa kuwa na virutubisho vingi, ukitumika zaidi kuandaa vyakula vya kusindika. Majumbani, kunatajwa uwezekano mkubwa kupata mwani katika aina tofauti na si kama kiungo pekee.

Kwa mujibu wa utafiti wa nchini Marekani, zao hilo lina utajiri wa protini na madini kalsiamu, chuma, magnesiamu hata zinki, kiwango cha lishe kikitofautiana kulingana na eneo la kijiografia inakopatikana, jinsi inavyohifadhiwa na kusindikwa.

Ni zao linalopatikana zaidi katika rangi mbalimbali; kijani, njano, nyekundu, zambarau, kahawia na hata nyeusi, huku aina ya kawaida zaidi ni zambarau inapatikana zaidi ukanda wa pwani ya Ireland.

**FAIDA ZAKE KIAFYA**

Inasaidia afya ya tezi; hapo ni kwa maana ya tezi lina jukumu la kutoa homoni za kusaidia kutawala ukuaji wa watu, nishati, uzazi na ukarabati mwili. Tezi linahitaji idadi ya virutubisho ambayo ni iodini na asidi ya amino, tyrosine, virutubisho vinavyopatikana katika mwani.

Afya ya utumbo; nyuzi zake nyingi za lishe ikiwamo katika afya ya utumbo, husaidia kuunda afya ya mtu kupitia uzalishaji asidi ya mafuta yenye mchango mkubwa tumboni.



Mama wa Zanzibar, akiandaa mlo kwa kutumia kiungo cha mwani.

- Inachangia kinga; mwani unamlinda mlaji na magonjwa mbalimbali, kwa kuhakikisha kinga yake inakua na nguvu. Pia husaidia urekebishaji wa kinga na kuboreshaji mwitikio wa kinga kwa walaji. Juisi nzito ya mwani, ina maana kubwa kwa afya ya mnywaji.
- Udhibiti sukari kwenye damu; uchunguzi unaonyesha kuwa mwani kama sehemu ya lishe yenye afya, uwiano wale unasaidia udhibiti wa sukari ya damu na kupunguza hatari ya kisukari cha aina ya pili. Nyuzi nyuzi nyingi katika mwani, pia ina sehemu yake kusaidia kupunguza kasi ya usagaji chakula.
- Inatetea afya ya moyo; ulaji mwani ni mojawapo ya vyanzo bora vya mimea ya asidi ya mafuta ya 'omega-3', ambayo ni muhimu kwa afya na hasa kwa moyo na mfumo wa moyo. Uchunguzi unaonyesha kwamba, mwani unaweza kuboresha usawa wa 'cholesterol' na kufanya kazi kama damu nyembamba, kupunguza hatari ya ugonjwa wa moyo.



Chakula cha mwani katika maandalizi.

Inafaa kuzingatia kwamba, ingawa tafiti zingine huchunguza athari za mwani wa baharini, nyingi hutumia mbadala za mwani. Kwa hivyo, utafiti zaidi unahitajika kufafanua uelewa wetu wa athari mahususi za kiafya za mwani wa baharini katika lishe ya binadamu.

**USALAMA WAKE?**

Mwani wa bahari kama vile wa Zanzibar, ni muhimu hasa kwa wale wanaofuata kwa kiasi kikubwa chakula cha mimea. Hata hivyo, ingawa maudhui ya iodini hufanya mwani kuwa na manufaa kwa afya ya tezi, ulaji mwingi unaweza kuwa na athari mbaya. Kwa sababu hii, Jumuiya ya Dietetic ya Uingereza inapendekeza mwani usiliwe zaidi ya mara moja kwa wiki, hasa wakati wa ujauzito.

Ikiwa unatumia dawa za kupunguza damu kama vile warfarin, daktari wako au mtaalamu wa lishe anaweza kukupendekeza ufuatilie vyakula vyenye vitamini K, kama vile mwani, katika lishe yako ili kuhakikisha unakula kiasi sawa kila mara.

Kirutubisho kingine ambacho mwani inayo kwa wingi ni potasiamu. Dawa fulani hufanya kazi kwa kuinua viwango vya potasiamu katika damu, kwa hivyo ikiwa unachukua mojawapo ya hizi, unapaswa kuwa mwangalifu unapokula vyakula vyenye potasiamu nyingi, kama vile mwani.

Mwani huweza kuloweka na kuhifadhi madini kwa kiwango kikubwa na unaweza kukusanya hatari ya sumu kama vile cadmium, zebaki, na alumini. Utafiti mmoja unaonyesha, hatari ya sumu inaonekana ni chini, ingawa ni bora kutumia mwani wa baharini kama mboga nyingine za bahari kwa kiasi.

***Kwa mujibu Kerry Torrens, ni mtaalamu wa lishe aliyesajiliwa Uingereza (MBANT).***

MAZINGIRA

# Baridi kihistoria yenye mafuriko ilivyoua, Rais Biden abaki mpweke, anakuna kichwa

**Na Mwandishi Wetu**

HADI siku chache zilizopita kumehesabiwa kuwapo takriban vifo 45 vinavyohusishwa na baridi kali, kiwango ambacho haijashuhudiwa kwa miaka 30 sasa, ikiikumba Marekani na Canada. Katika hesabu hiyo, inakadiriwa marehemu 34 ni Wamarekani, huku eneo lililoathirika zaidi likiwa ni jiji la Buffalo, katika jimbo la New York. Awali ilitamkwa waliokufa walikuwa 38.

Vifo vinne viliripotiwa Canada wakati basi lilipoingia kwenye barabara yenye barafu karibu na mji wa Merritt, katika jimbo la Magharibi la British Columbia. Ni kiwango cha maafa ya baridi ambacho hakijawahi kushuhudiwa, kuanzia ukanda wa Kusini mwa Canada hadi kwa majirani wa Rio Grade, nchini Brazil.

Watabiri wanasema, janga la baridi hiyo linatabiriwa kupungua katika siku chache zijazo, lakini ushauri umetolewa kuzuia watu kusafiri, isipokuwa kwa hali ya dharura.

Ni dhoruba iliyosababisha maafa kwa siku kadhaa, hata kuharibu huduma ya umeme, lakini jitihada zimefanikisha kuurejesha. Ni wastani wa wateja 200,000 hawakuwa na nishati hadi Jumapili alasiri iliyopita, kwa mujibu wa Shirika la Habari la Associated.

Ndege nyingi zimekatishwa safari zake na kuzuia watu wengi kufikia familia zao wakati wa Krismasi, ikiitolewa takwimu wastani wa Wamarekani milioni 55 walisalia wanakoishi, wakiahirisha safari ya likizo ya Krismasi; dhoruba ya msimu wa baridi ambayo hutokea, limetatiza usafiri kote Marekani.

Gavana wa Jimbo la New York, Kathy Hochu, mzaliwa wa Buffalo, anatamka: “Hii itaingia katika historia kama dhoruba mbaya zaidi kuwahi kutokea Buffalo.”



Wataalamu wa uokoaji wakipambana kutoa barafu iliyotawala katika maeneo mbalimbali ya mitaa nchini Marekani, kutokana na baridi la kihistoria. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**HISTORIA MIAKA 30**

Ni baridi kali baada ya kipindi cha miaka 30, ikiikumba Marekani, ikifika chini ya nyuzi sifuri. Idara ya Hali ya Hewa, imetahadharisha kuhusu hali mbaya ya hewa kwenye majimbo kadhaa ya nchi. Idara hiyo inasema, baridi inaweza kufikia chini nyuzi hasi 56 na pana wasiwasi mkubwa wa kuharibika miundombinu na kusababisha vifo.

Theluji nyingi na upepo mkali, zimewafanya watu waahirishe mipango ya likizo. Tahadhari ya dhoruba ya baridi zimeshatolewa kwa mamilioni ya watu na watabiri wa hali ya hewa wanasema, baridi ni kali kiasi kwamba sehemu za mwili zinaweza kuganda katika muda wa dakika chache ikiwa mtu anatoka nje ya nyumba yake.

Rais Joe Biden, akizugumza na wananchi, anasema baridi hiyo si ya kawaida na hali ya hatari barabarani, inazidi kuenea wakati ambao Wamarekani zaidi ya milioni 100 walikuwa wanatarajiwa kwenda kwenye shughuli zao za kila siku. Hatima yake, baadhi ya barabara kubwa zikawa hazipitiki kabisa Kaskazini mwa Marekani. Hata hivyo, mamlaka husika ziko katika jitihada kurejesha hali ya kawaida.

Inatajwa, theluji nzito imeanguka na kufunika barabara, hata kusababisha safari za ndege 22,000 zilicheleweshwa na 1,000 kati ya hizo, zilivunjwa, nyingi ni katika viwanja vya ndege vya jimboni Chicago.

Baadhi ya watu waliokosa usafiri wa ndege, waliamua kuendesha magari yao mwendo wa kilometa 1,100 kuelekea makwao kusherehekea Krismasi. Gavana wa New York, sasa anaungana na magavana wa majimbo mengine, kutangaza hali ya dharura, sambamba na hatari ya maafa. Taarifa iliyotolewa, imetahadharisha uwezekano wa kutokea mafuriko, mgando wa barafu na kukatika huduma za nishati.

**RAIS JOE BIDEN**

Rais Joe Biden, mbali na kutangaza hali ya dharura katika majimbo ya New York na New Jersey, ameagiza taasisi za serikali ya Shirikisho za Kupambana na Majanga, kuratibu juhudi za kuwasaidia wahanga kwa kutoa misaada ya dharura inayohusu mafuriko.

Pia ametangaza hali hiyo ya dharura kabla ya ziara yake katika jimbo la Lousiana ambako hapo kabla kimbunga Ida kiliharibu majengo na kuwaacha wakazi zaidi ya milioni moja kwenye giza baada ya umeme kukatika.

“Ujumbe wangu kwa wote walioathirika ni kuwa tuko pamoja katika hili. Taifa litawasaidia,” anatamka Rais Biden, akiendelea; “huo ndio ujumbe niliyoutoa kwa mameya, magavana na viongozi wa taasisi za nishati kwenye eneo hilo, ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na utawala wangu katika siku chache zilizopita.”

Akizungumza katika hotuba yake kwa taifa kuhusu majanga ya kiasili yanayoikumba Marekani, anaorodhesha kimbunga cha Ida, kilichofuatiwa na mafuriko mabaya Kaskazini Mashariki mwa Marekani, pia akiwakumbusha raia wake majanga kama kimbunga hicho cha Lousiana, mafuriko na moto huko California na Nevada, yanachangiwa na mabadiliko ya tabianchi, katika hatua za tahadhari ni muhimu.

**PICHA HALISI**

Mitaa husika, imefurika maji na vikosi vya uokozi vimekuwa vikiendelea kuwasaidia wahanga wa mafuriko baada ya janga hilo. Njia za chini ardhini kama barabara na reli zimefungwa, kutokana na kina cha maji kuongezeka. Mmiliki wa mgahawa wa Manhattan Metodija Mihajlov, anasema hajawahi kushuhudia mvua kubwa kama hiyo.

Vivyo hivyo, safari nyingi za ndege zinatajwa kuahirishwa katika viwanja vya LaGuardia na JFK, pamoja na Newark ambako video zinaonyesha njia ya kuondokea ndege zimefurika maji. Gavana wa New Jersey, Phil Murphy, amewaambia waandishi wa habari kwamba, takriban watu 23 wamekufa jimboni mwake, vifo vingi ni baada ya magari kusombwa na mafuriko.

Watu 13 wamekufa katika jiji la New York, ikiwa ni pamoja na 11 walioshindwa kutoka kwenye makazi yao yaliyoko chini ya ardhi. Rais Biden alitarajiwa kukutana na Gavana wa Lousiana John Bel Edwards na maofisa wa eneo hilo na kuzuru eneo jirani la LaPlace ambalo pia limeathirika pakubwa na maeneo mengine.

Wanasayansi wanasema, mabadiliko ya tabianchi yanachangia ongezeko la matukio mabaya ya hali ya hewa, kama dhoruba kali za tropiki, ukame na joto kali linalochochea kutolea moto msituni. Maofisa wa Taasisi ya Hali ya Hewa nchini Marekani waliripoti kwamba Julai ya mwaka huu, kulikuwa na joto kali zaidi kuwahi kurekodiwa katika kipindi cha miaka 142 nchini humo.

- ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***



AFYA

# Ugumba; tatizo lenye tafsiri tata kuanzia imani hadi kwenye jamii

## •Pata simulizi 'live' yaliyomkuta...

Na Christina Mwakangale

NI ndoto ya wanawake wengi wafikapo umri utu uzima, iwe ameolewa au hajaolewa, kupata mtoto, ingawa matarajio hayo kwa wenye imani tofauti ikiwamo kidini 'ni kudra za Mwenyezi Mungu.'

Ugumba, kimsingi ni tatizo la kushindwa kushika mimba kwa njia ya kibaiolojia na wataalamu wanasema linatibika. Madaktari bingwa wa kinamama na uzazi watatafsiri ugumba ni 'hali ya mwanamke kushindwa kupata ujauzito kwa kipindi cha mwaka mmoja, ilhali upo kwenye ndoa au uhusiano na hatumii njia yoyote kuzuia mimba.

Kukua kwa teknolojia duniani, sasa kunarudisha faraja kwa wanawake waliosubiri ujauzito muda mrefu kwa njia ya kiteknolojia, ikiwamo huduma ya kupandikiza mimba au kitaalamu 'In vitro Fertilization-IVF'.'

Daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake na uzazi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Living Colman, anasema mikasa ya wenza kushindwa kupata watoto zinaongezeka, akitoa takwimu za kliniki, kati ya wagonjwa 10 anaowaona kila siku hospitalini, wastani watu watatu wana tatizo hilo, ambalo kitaalamu analitaja ni ugumba, huku kila mwezi ana wastani wa wagonjwa 90, hali kadhalika kwa mwaka 1,080.



Wenza wakiwa kliniki wilayani Ikungi, mkoani Singida, hatua inayosisitizwa na bingwa, Daktari Living Colman, katika kutatua matatizo ya uzazi.

### TATIZO LILIKO

Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi, (MNH), Dk. Colman anasema ugumba ni hali ya mume na mke, kushindwa kupata ujauzito kwa zaidi ya mwaka mmoja, bila ya kutumia uzazi wa mpango wowote.

"Mzizi wa 'infertility' inategemea na chanzo, kwa mwanamke chanzo kikuu ni hormonal imbalance' (mayai kushindwa kupevuka kwa mpangilio) na hii inaweza kutokana na 'genetics' (urithi), pia ulaji mbaya, sukari nyingi na mafuta, husababisha unene uliopitiliza.

"Pia kupungua sana uzito (anorexia nervosa) inaweza kusababisha ugumba. Mirija kuziba ndio sababu ya pili ya ugumba kwa mwanamke na hii husababishwa na ngono zembe kama nilivyoeleza," anaeleza.

Daktari Colman anasema, kwa mwanaume ugumba unaweza kutokana na kushindwa kuzalisha mbegu kutokana na mambo mbalimbali, ikiwamo ulevi kupindukia, sigara pia kuziba mirija ya kupitisha mbegu inayosababishwa na maambukizi kama ya PID (Pelvic Inflammatory Disease), ambayo ni athari za bacteria.

"Tiba ya ugumba ni kumuona mtaalamu wa afya ya kike (gynecologist), ambaye atafanya vipimo na kugundua tatizo, halafu atatoa tiba husika. Kama ni 'hormonal imbalance' atapewa dawa na ushauri. Kama mirija imeziba atashauriwa apandikize (IVF).

"Si kweli kwamba matumizi ya dawa za uzazi wa mpango ndio chanzo cha ugumba. Ikiwa zitatumika kwa maelekezo ya mtaalamu, husaidia kuzuia mimba kwa muda fulani. Kuwapa watoto dawa za uzazi wa mpango ni kuwapa uhuru wa kufanya ngono zembe, hali inayosababisha kupata maambukizi kwenye uzazi (PID), hivyo kuathiri mirija ya uzazi na kushindwa kupata ujauzito," anaeleza.

Bingwa huyo wa tiba za kinamama, anasema jamii hasa ya mijini hutumia njia za uzazi wa mpango wa dharura (emergency contraceptive pills) maarufu P2, akiitaja njia hiyo si sahihi kwa kuwa, ikitumika kila mara inapoteza maana yake.

Anashauri kwamba, watoto wafundishwe kuepuka ngono za utotoni, ambazo ndio chanzo cha maambukizi kwenye njia za uzazi na kusababisha kuziba mirija na kushindwa kupata mimba.

### SIMULIZI YA VENERANDA

Veneranda ni mkazi wa Ulongoni Ukonga, jijini Dar es Salaam, mjasiriamali ambaye baada ya shughuli zake, muda wa jioni kwa siku tatu za wiki, huamua kushiriki na waumini wenzake kanisani kusali na shughuli zingine. Ni kanisa ambalo haliko mbali sana na mahali anakoishi, akiwa katika makazi hayo kwa takribani miaka 20 alikojenga nyumba yake.

Mama Veneranda Alfred (48), anajihisi ndoto hiyo haijatimia hadi sasa, licha ya kuwashirikisha viongozi wa dini anakoabudu, kuhusu kinachomsibu kwa muda mrefu, akiwataka wamfanyie maombi, apate mtoto.

Anasema ametarajia mtoto kwa takribani miaka 10 bila ya mafanikio, akiona umri unamtupa mkono hajafanikiwa kuitwa mama na anaamua kutumia fedha yake nyingi kupata mbadala wa IVF, ambayo ni mbinu ya kisasa kitabibu, inayowezesha mfumo wa kuunda mimba kiteknolojia hospitalini. Imekuwa maarufu, ikiwamo nchini Tanzania, huku watoto milioni nane duniani, wakikadiriwa kuzaliwa kutokana na IVF, kwa mujibu wa asasi ya European Society of Human Reproduction and Embryology.

"Ninaishi pekee yangu, sina watoto, mara chache au siku za likizo watoto wa ndugu zangu huja kunitembelea au watoto wa marafiki zangu ambao ninasali nao kanisa moja. Kuna wakati huwa najihisi mpweke, nina bahati mbaya," anatamka sentensi ya kinyonge, akiendelea:"Wenzangu ambao nina umri au rika moja, ama nimesoma nao hasa wanawake, wana watoto. Jamii inakutafsiri tofauti, dini nako mtihani."

"Kuna wakati siku tulipotoka kwenye ibada ya Jumapili, mmoja wa muumini mwenzangu, mwanawe mwenye umri kama wa miaka nane, tisa, alimuuliza mama yake swali ambalo nilijihisi vibaya, alimwambia...mama 'tutaenda kwa anti Veneranda, amesema niende.' Mama yake akamjibu utacheza na nani, utamsumbua anti, mtoto wake akamjibu mama yake...nitacheza na watoto wake!"

Veneranda anasema jibu la mwisho lilimfanya ajisikie vibaya, kisha mazungumzo hayo yalikatishwa baada ya mama wa mtoto kuamua kumwondoa mwanawe kisaikolojia, akimwambia akajumuike na watoto wenziwe kucheza na aache maswali mengi.

"Kwa imani ninakoabudu, nafahamu ninachokwenda kukiamua kitanigharimu. Kanisa letu kupata mtoto ni majaliwa ya Mungu na muumini yeyote hutakiwi kutumia njia yeyote mbadala na ukibainika unaweza kuitwa na viongozi wa kanisa au kutengwa. Hivi sasa nimeanza kufanyiwa vipimo na moja ya hospitali binafsi, ili nipandikize mtoto kwa IVF," anasema Veneranda na kuongeza:

"Na mwanzo wa huduma hii ninatakiwa kukaa 'bed rest' (mapumziko) nisifanye kazi ngumu. Kanisani sijaonekana takribani

INANDELEA UK. 20



Dk. Living Colman, bingwa wa tiba za kinamama katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Ugumba; tatizo lenye tafsiri tata kuanzia imani hadi kwenye jamii

INATOKA UK. 19

miezi miwili na sijamtaarifu kiongozi yeyote, watakapofahamu, sijui itakuwaje."

**HUDUMA YA IVF**

Inatajwa mahitaji yanaongezeka na tayari, MHN imeanza maandalizi na maboresho ya kituo rasmi kwa ajili ya huduma hiyo hospitalini, ikiwamo kununua vifaa husika.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma MNH, Aminiel Aligaesha, anasema maandalizi ya utoaji huduma ya IVF yanaendelea hospitalini hapo na yatakapokamilika taarifa itatolewa kwa umma.

Mtaalamu wa kutengeneza Watoto kwa Njia ya Teknolojia (Embriologist) kutoka Hospitali ya Kairuki Green IVF, George Tryphone, anasema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma ya upandikizaji, baada ya kubaini mahitaji ni makubwa, na tayari kwa mwaka huu wameshahudumiwa wanawake 10 na kati yao saba ni wajawazito.

Anafafanua, kati ya hao saba wajawazito, mmoja ana umri miaka 52 na kwamba gharama za huduma ya IVF huwa ni kati ya shilingi milioni 10 hadi 17 kutegemea na ukubwa wa tatizo.

**SIKU YA UGUMBA DUNIANI**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Merck Foundation, Seneta Dk. Rasha Kelej, akizungumza kwenye mkutano wa waandishi wa habari kutoka barani Afrika, ikiwamo Tanzania kwa njia ya mtandao, wakiadhimisha Mwezi wa Kujenga Uelewa kuhusu Ugumba Duniani (World Infertility Awareness Month), nusu ya tatizo la ugumba, huchangiwa na pande zote mbili za jinsia.

Anasema mwezi Juni kila mwaka, ni maalumu kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu tatizo hilo, ili kuondoa unyanyapaa wa umma, akiwa na ufafanuzi kwamba, wanawake wanaokosa watoto na wamo kwenye ndoa, hunyanyaswa na kunyanyapaliwa zaidi na ndugu wa upande wa mume, hasa mawifi, mashemeji na wakwe.

"Tatizo la ugumba hasa Afrika, matokeo ya utafiti yamebaini kwamba asilimia 75 yanachangiwa na tiba isiyo sahihi kwa walioambukizwa magonjwa mbalimbali. Mradi wa 'More Than a Mother and More Than a Father Campaign' unakuja kutoa elimu na kuondoa unyanyapaa," anasema Dk. Rasha.

Prof. Uldapo Ashiru, Rais wa Jumuiya ya Kiafrika inayoshughulikia masuala ya Uzazi (African Reproductive Care Society-ARCS), kutoka nchini Nigeria, anasema ugumba umekuwa tatizo la dunia, huku takwimu za tatizo hilo zaidi likiongezeka kwenye nchi za Afrika, akitaja sababu mojawapo ni msongo wa mawazo.

"Nimefanya kazi kwa miaka takribani 42, zamani kinamama walifika kliniki peke yao kuhusu tatizo hili, lakini sasa hata wanaume wana tatizo. Mwanamke akifikisha umri wa miaka 37 na kuendelea vikwazo vya kutopata ujauzito huongezeka. Sasa Nigeria kuna mfumo ambao unamwezesha mwanamke kutunza mayai yake kwenye benki maalum kama ilivyo benki ya damu.

"Mayai hutunzwa kwa muda mrefu, teknolojia hii inasaidia wanawake ambao kwa sasa hawapo tayari kupata mtoto kutokana na shughuli za masomo, kazi au kuchelewa kuolewa. Atakapofikisha umri wowote akishindwa kupata ujauzito atapandikizwa mayai aliyoyatunza benki, hata akiwa na umri wa miaka 50," anasema bingwa huyo wa kinamama na uzazi," anasema.

Rais wa Shirikisho la Muungano wa Vyama vya Uzazi (International Federation Fertility Societies and Gynaecologist), Dk. Edgar Macanu, anasema tatizo la ugumba, linajitokeza zaidi kwa wanawake kuanzia umri wa miaka 37 na kuendelea, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo za kimazingira au kibaiolojia.




Mama akiwa na mwanawe kliniki wilayani Mvomero, mkoani Morogoro. **PICHA: MAKTABA**


---

## CHEMSHABONGO NA -00 38 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. Nyumba
5. janga
7. mwanaume wa kwanza
8. uchafu
9. safisha mwili
10. maisha ya starehe
12. mtu mwenye afya nzuri
13. Ugwe
14. tamka maneno kimuziki
17. neno la kuitikia
18. Itikadi
19. kifupi cha neno sisi

Chini:
1. ndege mpenda maji
2. toa maagizo uletewe kitu fulani
3. mahali wanapoishi watu
4. utulivu
6. usawa juu ya ardhi
9. gaidi aliyelipua balozi za Marekani
11. sadiki
12. kivuli cha mtu aliyekufa
15. gari kubwa la abiria
16. amu



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

TEMBEA
KETE, VAA
MANDELA
DARI, JAA
BONDE, POMBE
NAMBA, SAA
PANGA, AGA
PAPA, AGO
AJENDA
TAPELI
DEREVA
MBEGE



maoni SMS: 0787 00 97 94

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | A | D | A | | A | B | U |
| U | S | A | F | I | R | I | |
| K | A | M | A | | I | | M |
| A | L | A | S | K | A | | A |
| K | I | S | I | A | | | R |
| U | | C | A | N | A | D | A |
| U | T | U | | I | | | D |
| | A | S | A | S | I | | H |
| | A | | | A | | | I |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | A | B | U | L | I | | |
| U | K | A | L | I | L | I | |
| K | I | B | A | L | I | | N |
| U | L | A | F | I | | | D |
| | I | | I | W | A | P | O |
| K | | I | | A | G | W | A |
| A | | B | A | L | A | A | |
| S | H | A | U | A | | N | |
| A | | | A | | B | I | A |



## Dk. Tulia aahidi kuboresha miundombinu ya machinjio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, ameahidi kuboresha baadhi ya miundombinu ya machinjio mbalimbali yaliyoko jijini Mbeya.

Dk. Tulia ambaye ni Spika wa Bunge alitoa ahadi hiyo jana alipofanya ziara kwenye machinjio mbalimbali zilizoko jijini humo kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakabili.

Alisema atashirikiana na wadau kujenga mazizi kwenye baadhi ya machinjio ili kurahisisha uhifadhi wa mifugo ambayo inasubiria kuchinjiwa.

Vilevile alisema atawasaidia kuingiza umeme kwenye machinjio ya VETA ili kuongeza mwanga ndani ya machinjio hayo na kurahisisha shughuli hizo kufanyika.

"Lakini nawashukuru kwa kuwa mmejichanga mmeanza kuboresha barabara hapa, mimi na wenzangu tutashirikiana kuboresha vitu vikubwa ili kuunga mkono juhudi mlizoonyesha," alisema Dk. Tulia.

Hata hivyo alisema baadhi ya kero zitashughulikia na halmashauri ikiwamo kujenga uzio kuzunguka machinjio ya VETA ili mazingira yake yawe rafiki.

Alisema atawasilisha kero hizo kwenye halmashauri ili zitatuliwe ikiwamo umaliziaji wa ukarabati wa barabara inayoelekea kwenye machinjio ya Veta.

**Vilevile alisema atawasaidia kuingiza umeme kwenye machinjio ya VETA ili kuongeza mwanga ndani ya machinjio hayo na kurahisisha shughuli hizo kufanyika.**

# CCM yakumbusha ahadi ya Hayati JPM ujenzi barabara

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimeikumbusha serikali kutimiza ahadi zilizotolewa na Rais Hayati Dk. John Magufuli ya kuijenga kwa lami Barabara ya Mbambo-Ipinda (kilomita 19).

Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Dk. Stephene Mwakajumilo, alikumbushia ahadi hiyo juzi wakati wa utiaji saini ya ujenzi wa barabara tatu zinazounganisha bandari za Ziwa Nyasa zilizoko wilayani Kyela.

Alisema ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo ilitolewa na Hayati Dk. Magufuli mwaka 2019 wakati alipofanya ziara mkoani humo ya siku tisa mfululizo.

Alisema Hayati Magufuli aliahidi kujenga barabara hiyo baada ya kupita wakati akitokea katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe kwenda Kyela.

Alisema alibaini kuwa barabara hiyo ina umuhimu kiuchumi kutokana na uzalishaji wa mazao mbalimbali katika eneo hilo ambayo yanahitaji kusafirishwa kwenda katika maeneo mbalimbali nchini.

"Mheshimiwa Waziri wewe uliambatana na Hayati Magufuli wakati ule kwenye ziara na alipokuwa anaahidi ulikuwapo, tunakuomba ahadi ile itimizwe ili kuturahisishia usafirishaji wa mazao katika eneo hilo," alisema Dk. Mwakajumilo.

Vilevile Dk. Mwakajumilo aliiomba serikali kuharakisha upanuzi wa Barabara ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kuanzia Igawa wilayani Mbarali mpaka Mji wa Tunduma mkoani Songwe. Alisema barabara hiyo ndiyo roho ya uchumi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na hivyo inatakiwa kuboreshwa ili kurahisisha usafiri na usafirishaji.

Hata hivyo alisema wakati serikali inaanza ujenzi wa barabara za kuunganisha bandari za Ziwa Nyasa, pia inatakiwa kuifanyia upanuzi barabara ya njia panda ya Kasumuu mpaka Kyela Mjini ili iendane na barabara mpya zitakazojengwa.

Pia aliomba itengwe bajeti maalumu ya kuweka taa kwenye barabara mpya ya kuelekea katika Bandari ya Kiwira kuanzia Kyela Mjini ili kuchochea shughuli za kiuchumi katika eneo hilo.

Akijibu maombi hayo, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alisema ofisi yake itatekeleza ahadi zote za serikali ili kufungua fursa za kiuchumi ambazo zipo kwenye maeneo husika likiwamo la Barabara ya Mbambo-Ipinda.

Alisema katika eneo hilo linalopitiwa na barabara hiyo wananchi wanazalisha kakao kwa wingi na hivyo wnatakiwa kuwa na miundombinu mizri ya kusafirishia mazao hayo.

Kuhusu upanuzi wa barabara ya TANZAM, Waziri Mbarawa, alisema michakato yote ilishakamilika na zimebaki taratibu chache ili kuanza ujenzi mapema mwakani.

Naubu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema lengo la serikali kwa sasa ni kuiunganisha nchi kwa barabara za lami katika maeneo yote.

Alisema kwa sasa serikali ipo kwenye michakato ya ujenzi wa Barabara ya Kasumulu-Isongole ili kuziunganisha Wilaya za Kyela na Ileje na kuchochea uchumi kwenye eneo hilo lenye utajiri wa makaa ya mawe.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya (kushoto), akimkabidhi mtungi wa gesi mmoja wa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi ikiwa ni utekelezaji wa kampeni yake ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Naibu Waziri aanzisha kampeni matumizi ya gesi badala mkaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ameanzisha harakati maalumu ya utunzaji wa mazingira kwa kuwahamasisha wananchi kuacha kutumia mkaa na kuni kupikia na badala yake watumie gesi.

Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, anagawa mitungi ya gesi kwa baadhi ya wanawake ili watumie nishati hiyo ambayo anadai ni safi na ni rafiki wa mazingira tofauti na matumizi ya kuni na mkaa ambazo zinachochea ukataji wa miti.

Akigawa mitungi hiyo juzi kwa baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoa, Mahundi alisema matumizi ya nishati hiyo yatasaidia kuhifadhi misitu na vyanzo vya maji.

Kampeni hiyo atakuwa anaifanya kila mwaka kwa kugawa bure mitungi hiyo ya gesi kwa wanawake na kwamba alianza kugawa mwaka jana kwa kugawa mitungi zaidi ya 500 kwa wajumbe wa UWT kama sehemu ya majaribio.

Alisema mwaka huu amegawa mitungi 150 kwa wajumbe wapya wa mkutano huo ambao mwaka jana hawakupata ili kukamilisha kundi hilo kabla ya kuendelea na makundi mengine ya kijamii.

"Tulianza mwaka jana kugawa mitungi hii na nimekuwa nikishirikiana na kampuni mbalimbali ya gesi, lengo langu ni kutaka kutunza mazingira na kuboresha afya za wanawake, nishati hii ni safi na hazina madhara yoyote kwenye mazingira wala kwenye afya," alisema Mahundi.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole, alimpongeza Mahundi kwa kufikiria kundi hilo ambalo alisema ndilo linaloathirika zaidi na matumizi ya nishati za kuni na mkaa.

Alimuomba aendelee kulisaidia kundi hilo ili kuokoa afya zao pamoja na kusaidia kulinda mazingira ambayo yamekuwa yakiharibiwa mara kwa mara.

Mwaigomole ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) alisema matumizi ya kuni ni miongoni mwa shughuli zinazochangia uharibifu wa vyanzo vya maji.

Baadhi ya wajumbe walionufaika na mitungi hiyo walimshukuru Mahundi kwa kuwasaidia huku wakiahidi kuitumia vizuri ili kutunza mazingira na afya zao.

Mmoja wa wajumbe hao, Sophia Mwanahuta kutoka katika Wilaya ya Chunya alisema wilaya yao ni miongoni mwa maeneo ambayo yanakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Alisema zipo shughuli mbalimbali zinazochochea ukataji wa miti na hivyo kwa kitendo cha kugawiwa mitungi kinasaidia kupunguza moja ya shughuli hizo.





# Dodoma, Singida zawezeshwa mbegu za kisasa mtama, alizeti

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KILO 500 za mbegu za mtama na alizeti zimetolewa kwa wakulima wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Singida ili kusaidia kuongeza tija katika mazao hayo nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki baada ya kuwakabidhi wakulima mbegu hizo, Katibu Mtendaji wa Chama cha Wazalishaji wa Mbegu Dodoma (DASPA), Aithan Chaula, alisema ni matumani yao kuwa mbegu hizo zitaleta tija kwa wakulima hao.

Chaula alisema mbegu hizo zimetolewa kwa wakulima na kwenye shule katika kata nane za wilaya ya Chamwino ikihusisha vijiji vya Nzali, Mahama, Msanga, Chamwino, Buigiri, Manchali, Chalinze, Makoja, Muungano Makang'wa, Mlowa Barabarani, Mlodaa na Iringa Mvumi.

Alivitaja vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Singida kuwa ni Mtinko, Ntonge, Mrama, Kijota, Mudidæ, Menya na Madami.

Pia alisema Wilaya ya Chamwino imepata kilo 200 na wakati Singida imepata kilo 100 za mbegu hizo. Kadhalika, alisema kilo 200 zitagawiwa kwenye shule za msingi. Chaula alisema mbegu za mtama zilizogawiwa ni aina ya Masia ambazo hukomaa kwa muda mfupi.

Katibu huyo aliwataka wakulima kutumia vizuri mvua zinazoendelea kunyesha kwa kupanda mazao yanayostawi katika maeneo yao na kupanda katika maeneo yaliyotifuliwa.

Alisema miongoni mwa mambo yaliyochangia kuongeza uzalishaji katika mikoa ya Dodoma na Singida ni matumizi ya mbegu za mazao yanayostahimili hali ya hewa ya eneo husika, matumizi ya matrekta na utifuaji wa mashamba na maofisa ugani kufuatilia wakulima.

Chaula alisema wamekuwa wakisisitiza wakulima kutifua mashamba kwa kuwa hufanya maji yasitembee shambani na kwenda kusababisha maporomoko.

"Watu wengi hawalimi mpaka chini wanalima kwa kuparua. Mvua inaponyesha maji yanapita na kuacha udongo ukiwa mkavu," alisema.

Alisema kilimo cha Dodoma kinategemea mvua, hivyo mwanzo wa msimu wa mvua unakuwa mwanzo wa msimu wa kilimo na hali hiyo itaendelea kwa muda mrefu ujao mpaka pale uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji utakapoimarika.

Hata hivyo, alisema serikali inawekeza fedha nyingi katika kilimo hivyo kila mmoja aone wajibu wa kuunga mkono juhudi hizo kwa kufanya shughuli zenye tija kwa jamii na taifa kwa ujumla.




Baadhi ya wananchi wakinunua bidhaa zinazouzwa kwenye maonesho yaliyoandaliwa na Kampuni ya Kelaf Group ya Dar es Slaam yanayoendelea jijini Dodoma jana. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# DC ahimiza wakulima kutumia vyema mvua

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Shabir Shekimweri, amewataka wakulima kuzitumia vizuri mvua ambazo zimeanza kunyesha kwa kilimo na upandaji miti ya kivuli na matunda kwenye maeneo mbalimbali ili kutunza mazingira.

Shekimweri alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wadau mbalimbali wa maendeleo, wakiwamo viongozi wa serikali, kata, mitaa, wazazi na walezi mara baada ya kukabidhiwa majengo ya madarasa ya Shule ya Sekondari ya Ng'ong'ona jijini hapo yaliyojengwa kwa fedha za UVIKO-19.

Alisema pamoja na mvua hizo kutumika kwenye shughuli mbalimbali kama vile: Kilimo, wananchi wanapaswa kushirikiana na taasisi mbalimbali kupanda miti kwenye maeneo yao.

Mkuu huyo wa wilaya alisema bado kuna maeneo mengi yakiwamo ya taasisi za umma kama vile: Shule na ofisi za majengo ya serikali, hazina miti ya kutosha, hivyo mvua hizo ambazo tayari zinanyesha wahakikishe zinatumika kwa ajili ya kilimo pamoja na uoteshaji wa miche na upandaji wa miti.

Pia aliwataka maofisa elimu kata, wazazi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo kurudisha ajenda ya wanafunzi kuhusu somo la kilimo na kilimo shuleni ambacho kinaonekana kusahaulika hivi sasa ili kujipatia mazao yatakayotumika kwa ajili ya chakula na kuwapunguzia wazazi na walezi mzigo wa kuchangia chakula shuleni.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, aliziomba shule zote za sekondari na msingi kuwa na walimu ambao ni wataalam wa kilimo ikiwemo uoteshaji wa miche ambayo itawezesha maeneo yao kuwa na miti ya kutosha.

Kadhalika, alizitaka shule hizo kulima mazao yanayokomaa haraka kulingana na hali ya hewa iliyopo na chakula kitakacholimwa kitumike kwa ajili ya chakula kwa walengwa ambao ni wanafunzi wenyewe.

# Watakiwa kuacha dhana potofu kuhusu ulemavu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JAMII imetakiwa kutowatenga watoto wenye ulemavu na kuacha dhana potofu kuwa kuzaliwa na ulemavu ni adhabu mbele ya jamii.

Rai hiyo ilitolewa jana na mrembo wa Tanzania mwaka 2022, Halima Kopwe, wakati wa chakula cha pamoja kilichoandaliwa na kituo cha Tumaini Foundation, hafla iliyokwenda sambamba na kuchangisha fedha kwa ajili ya kusaidia kituo hicho ambacho kinalea yatima na wajane.

Kopwe alisema jamii inatakiwa kutowatenga watoto wenye ulemavu na kuondoa fikra potofu kuwa kuzaliwa na ulemavu ni adhabu.

"Jamii inaamini kuzaliwa mlemavu ni adhabu kutoka kwa Mungu. Watoto wenye ulemavu wana kila haki. Tuungane kwa pamoja tuwatie moyo, hata Tumaini Foundation inapojenga shule kwa ajili ya wenye ulemavu pale Gairo mkoani Morogoro, tujitokeze tuwatie moyo," alisema.

Alisema kuwa watoto ni taifa la kesho wanahitaji malezi na kupata elimu ambayo ndiyo msingi wa maisha yake.

"Mwanzoni nilikuwa nikidhani mtoto akiwa yatima ukimpa msaada tu inatosha kumbe sivyo, hawa watoto wana mahitaji mengi na hata kukaa pamoja na kufurahi na wenzao huwaongezea furaha," alisema.

Kopwe alisema alipata fursa ya kutembelea kituo cha Tumaini na watoto wamekuwa wakifundishwa ujuzi, kuchora, kushona na wajane wamekuwa wakishona vikapu na mikeka.

"Tuwape watoto stadi za kazi ili baadae wawe na ujuzi wa kuweza kujiajiri," alisema.

Mkurugezi wa Tumaini Foundation, Tumaini Kivuyo, alisema jamii imeanza kuwa sehemu ya kusaidia maisha ya watoto.

Alisema asasi hiyo ilianza shughuli zake mwaka 2008 wilayani Babati mkoani Manyara ikiwa na watoto 17 waliokuwa wakila majalalani, lakini walipata mfadhili aliyesaidia kituo hicho na hatimaye wakaingia kwenye mfumo rasmi wa elimu.

Alisema asasi hiyo imelenga kuboresha maisha ya watoto wenye mazingira magumu na wajane. Pia alisema kuwa kituo hicho kinahudumia watoto 350 na wajane 300 Tanzania nzima.

"Tunaamini malezi sahihi ni ya familia, tunawasaidia watoto wakiwa kwenye familia na kuhakikisha wanapata elimu na kuendeleza stadi za maisha," alisema.

Alisema wamekuwa wakifanya kazi katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Kagera, Arusha na Manyara na kwamba kwa sasa wanaendelea na ujenzi wa kituo cha watoto wenye ulemavu Gairo na kuwataka wadau kuunga mkono juhudi hizo.

Mmoja wa watoto katika kituo cha Tumaini, Grace Wîston, ambaye anasoma darasa la nne alisema kutokana na uwezo mdogo wa wazazi wake hakuweza kuandikishwa shule lakini juhudi za kituo hicho zilisaidia kuandikishwa shule na kupewa sare na vifaa vingine na sasa amepata fursa ya kupata elimu.

Naye Mkurugenzi wa Diamanda Foundation, Diamanda Kaphipa, aliwataka wenye vituo vya kulea na kutunza yatima kuwa na umoja na mshikamano kwa kuwa lengo ni kuwasaidia watoto wa Tanzania.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Chama Cha Mapinduzi (CCM), Joyce Lyoba, alisema juhudi zinazofanywa na kituo hicho kuhakikisha watoto wanapata elimu ni za kuungwa mkono.



# Ukosefu ajira Zanzibar wafikia 27.4%

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya juhudi kubwa zilizofanywa na serikali kukabiliana na ukosefu wa ajira, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana kimefikia asilimia 27.4 kwa mwaka 2020/21 Zanzibar.

Hayo yalisemwa jana visiwani Zanzibar na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akizindua ripoti ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi ulioandaliwa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

Alisema matokeo yanaonyesha zaidi kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana wa kike ni kikubwa kwa asilimia 40.6 ikilinganishwa na vijana wa kiume asilimia 15.4.

Soraga alisema utafiti huo pia umegundua kiwango cha vijana ambao hawako katika ajira, hawatambuliwi na mfumo wa elimu na hawapo katika mafunzo au kwa jina la kitaalamu wanaitwa (NEET), kimepungua kutoka asilimia 14.6 hadi 14.2.

Alisema hatua hiyo imesababisha kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kuongezeka kwa kasi kubwa.

Pia alisema matokeo ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2020/21 yanaonyesha kuwa na ongezeko la idadi ya wasiokuwa na ajira imefikia asilimia 19.6 ikilinganishwa na asilimia 14.3 ya mwaka 2014.

Alisema kwa mujibu wa matokeo hayo imeonekana kuwa Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa kuwa na ongezeko la ukosefu wa ajira kwa asilimia 26.6 kwa mwaka 2020/21 kutoka asilimia 23.1 ya mwaka 2014.

"Utafiti umebaini kuwa katika Mkoa wa Kusini Unguja na Kusini Pemba, tatizo la ukosefu wa ajira limepanda kwa kasi kubwa ambapo Mkoa wa kusini Unguja umepanda kwa asilimia 12.5 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na asilimia 3.9 ya mwaka 2014, na Mkoa wa Kusini Pemba ongezeko la ukosefu wa ajira limepanda kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 14.0 ya mwaka 2020/21," alisema.

Hata hivyo, alisema umuhimu wa sekta isiyo rasmi katika ajira umeendelea kuonekana ambapo matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa watu wanaojishughulisha katika sekta hiyo imeongezeka hadi asilimia 41.7 kutoka asilimia 37.7 mwaka 2014.

Alisema kukua kwa ajira katika sekta isiyo rasmi kumetokana na serikali kurahisisha mazingira ya watu kujiajiri ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wajasiriamali wadogo kwa kuwapunguzia kodi, kuwapatia maeneo ya kufanyia shughuli zao za kiuchumi na kutoa fursa za mikopo nafuu kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Waziri huyo alisema serikali imejipanga kuandaa mazingira rahisi ya urasimishaji ili shughuli hizi ziweze kukua zaidi.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema matokeo ya utafiti huo yatasaidia serikali na wadau kufahamu hali halisi ya soko la ajira nchini, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango na sera mbalimbali za kukuza ajira na kupunguza umaskini ikiwamo dira ya maendeleo Zanzibar 2050.

Alisema matokeo yaliyotokana na utafiti huo yanawezesha pia kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu nyingine za maendeleo za kikanda na kimataifa ambazo Tanzania imeridhia.

Mwakilishi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Adame Traore, alisema utafiti huo utaisaidia Tanzania katika kukakikisha inaandaa mkakati ambao utasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Pia alisema ILO itaendelea kushirikiana na serikali ili kuzitafutia ufumbuzi changamoto za ajira hasa vijana na wanawake.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga (kulia), akimkabidhi kitabu cha ripoti ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanyakazi ya mwaka 2020/2021, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Masoud, katika hafla ya uzinduzi wa ripoti hiyo iliyofanyika jana hoteli ya Madinatul Bahari Mbweni Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wajasiriamali kuwekewa mazingira bora

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali ya Zanzibar itaendelea kuwawekea mazingira mazuri wajasiriamali ili kuuza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

Hemed aliyasema hayo jana katika hafla ya kukabidhi vifaa vya ufugaji nyuki kwa Wakuu wa Mikoa ya Unguja iliyofanyika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema azma ya serikali ni kuwawezesha wananchi kiuchumi na jitihada nyingi zimechukuliwa kuona wananchi wanakomboka kiuchumi hususan baada ya mlipuko wa janga la UVIKO -19.

Hemed alisema Sh. bilioni 1.4 zimetengwa kwa ajili ya wajasiriamali wa ufugaji wa nyuki.

Pia alisema mradi huo umenufaisha vikundi 85 kwa kupewa mafunzo ya ufugaji wa nyuki na kuwataka wanufaika wa mafunzo hayo kuyatumia vyema mafunzo waliyoyapata.

Hemed alisema mradi huo umelenga kuwasaidia vijana na wanawake kuongeza thamani ya zao la asali na kulipatia soko la uhakika na kuinua hali za maisha ya wananchi wa Zanzibar.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema serikali imejenga vituo viwili vya kusanifu asali Kizimbani kwa Unguja na Pujini, Pemba kwa lengo la kusaidia kuongeza ubora wa asali inayozalishwa Zanzibar.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar, Juma Burhan Muhamed, alisema watawasimamia wanufaika hao kuvitumia ipasavyo vifaa hivyo pamoja na kuhakikisha wanarejesha mkopo huo kwa lengo la kuendeleza wafugaji wingine.

Akisoma risala kwa niaba ya wajasiriamali wenzake, Latifa Faraja Ali, alisema mafunzo hayo ya wiki mbili yamewasaidia kuwaongezea ujuzi pamoja na kujua namna ya kutengeneza mizinga ya kisasa na nta ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa wafugaji wa nyuki.

## Alia watoto ulemavu wasioona kukosa elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRATIBU wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Wasioona Zanzibar (ZANAB), Adil Mohammed, amesema bado watoto wenye ulemavu huo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kukosa fursa za elimu.

Adil aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake, Kikwajuni Zanzibar, baada ya wanachama wa jumuiya hiyo kukamilisha uchaguzi mkuu ambao ulimchagua Fatuma Djaa Chesa kuwa mwenyekiti kwa mara ya pili.


Alisema hali hiyo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na wazazi kukosa mwamko wa elimu kwa kutowapeleka watoto hao shule na kwa waliooshule kutowafuatilia maendeleo yao kielimu. Mratibu huyo alisema watoto hao wanahitaji visaidizi vya kuwafikisha shuleni lakini kupata elimu stahiki kama watoto wengine wasio na ulemavu pamoja na kuwa na mashine ya nukta nundu.

Alisema katika miaka mitano ijayo, jumuiya hiyo imejipanga kutekeleza baadhi ya miradi ukiwamo wa kuwarudisha shuleni watoto wenye ulemavu wasioona walioacha shule ambao wengine wako majumbani ili kupata haki ya elimu.

Kwa miaka mitano sasa, alisema wanatekeleza mradi wa kuwarudisha shule watoto hao kupitia ufadhili wa Shirika la Kimataifa la watu wenye ulemavu la Sweden (SRF).

"Tunatoa pongezi za dhati kwa wafadhili wetu kutoka Sweden SRF kwa kuamua kutusaidia katika kipindi cha miaka mitano. Miongoni mwa miradi ambayo tumeweka kipaumbele kuitekeleza ni pamoja kuwaibua watoto wote wenye ulemavu wa uoni ambao wako nje ya mfumo wa elimu ya lazima huku tukitoa elimu kwa wazazi wenye watoto wa aina hiyo wasiwaweke majumbani kwa sababu fursa za elimu zipo," alisema.

Mratibu huyo alipongeza serikali ya Zanzibar kwa kutumia vizuri fedha za UVIKO- 19 kwa ujenzi wa shule za elimu mjumuisho kwa watu wenye mahitaji maalumu ili kupata fursa na haki ya msingi ya elimu.





# Polisi yabaini utapeli ukodishaji bunduki kampuni za ulinzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limebaini 'utapeli' unaofanywa na kampuni binafsi za ulinzi kwa kukodisha bunduki kwa watu binafsi kinyume cha sheria.

Bunduki hizo licha ya kukodishwa kutoka kwa watu binafsi imeelezwa kuwa zinakuwa hazina risasi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alibainisha hayo wakati wa kikao maalum kati ya Jeshi la Polisi na wamiliki wa kampuni binafsi za ulinzi kilichokuwa na lengo la kupeana maelekezo na kukumbushana wajibu kuhusu ulinzi na usalama.

Kamanda Magomi alisema hatua hiyo imeelezwa kuwa inachangia kuwapo uhalifu kwa sababu wahalifu wakibaini bunduki zinazotumiwa na walinzi hazina risasi ni rahisi kuwavamia.

Alisema licha ya kuwapo na tatizo hilo, lakini bado bunduki hizo zinasaidia katika ulinzi wa wananchi na mali zao.

Alisema askari mmoja analinda raia 1,400 hadi 1,500 idadi ambayo ni kubwa kulinganisha na idadi ya askari polisi walioko.

Magomi alisema Jeshi la Polisi linapenda kuona kampuni hizo za ulinzi zikiwa na silaha zao wenyewe na kuwasihi kuajiri watu waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au mgambo.

Alisema kuajiri mtu asiyekuwa na mafunzo au raia wa kigeni ni kosa kisheria na watakaobainika watashtakiwa.

Mwenyekiti wa Umoja na Kampuni Binafsi za Ulinzi wilayani Kahama, Phabian Ndyanabo, alisema wapo tayari kufuata sheria.

Alisema wamejipanga kuhakikisha kampuni hizo zinafanyakazi kwa kufuata utaratibu uliowekwa na kuahidi kufanya mabadiliko kutokana na upungufu walioelezwa.

Aliongeza kuwa Wilaya ya Kahama ina kampuni za ulinzi 51 na kati ya hizo 34 zina ofisi zinazotambulika na zingine 17 hazina ofisi.

Hivyo, alizitaka kampuni zote ambazo hazina ofisi kuhakikisha wanakuwa nazo ili iwe rahisi kupatikana wanapotafutwa.



Mwendesha bodaboda akipita kwenye daraja lililotengenezwa kwa ajili ya waenda kwa miguu eneo la Majengo jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wafikishwa mahakamani tuhuma kumzika mtoto akiwa hai

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WASHTAKIWA watatu wanaodaiwa kumzika mtoto akiwa hai wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi jijini Mwanza wakikabiliwa na tuhuma za mauaji.

Waliofikishwa mahakamani ni Zawadi Masaga ambaye ni mama mzazi wa mtoto huyo, Elizabert Kaswa dada wa marehemu pamoja na Musa Mazuri ambaye ni mganga wa kienyeji.

Akisoma mashtaka hayo, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Makahama ya Hakimu Mkazi mkoani Mwanza, Fotunata Bubaja, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mwanahawa Changali, alisema washtakiwa hao walitenda kosa hilo Novemba 13, mwaka huu.

Alisema washtakiwa hao wanakabiliwa na kesi ya mauaji namba 7 ya mwaka 2022.

Alieleza kuwa tukio hilo la mauaji ni kinyume cha kifungu namba 196/197 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu na Marejeo namba 16 ya mwaka 2022.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo ya mauaji na walirudishwa rumande.

**Alisema washtakiwa hao wanakabiliwa na kesi ya mauaji namba 7 ya mwaka 2022.**

# Familia yagoma kumzika ndugu aliyefariki kwa sumu ya panya

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

FAMILIA ya Bukindu Bukindu mkazi wa Kitongoji cha Bugogo Kata ya Bukoli wilayani Geita mkoani Geita aliyefariki katika mazingira ya kutatanisha imegoma kuzika mwili wa ndugu yao.

Kijana huyo alifariki dunia baada ya kunywa sumu ya panya na familia yake imegoma kuuzika mwili wake ikitaka ufanyike uchunguzi ili kubaini chanzo cha kifo chake.

Akisimulia tukio hilo, mama mzazi wa marehemu, Shija Antony alisema mtoto wake alikuwa akifanya kazi kwa mfanyabiashara mmoja kijijini hapo.

Alisema juzi kijana huyo aliagizwa na mwajiri kwenda kununua vinywaji na baada ya kufika dukani alitoa Sh. 45,000 na kumlipa muuzaji.

Hata hivyo, baada ya kijana wake kuondoka dukani hapo, muuzaji alimfuata na kumdai fedha kwa madai kwamba hakumlipa.

Aliongeza kuwa kijana huyo alijitetea kwamba alikuwa amelipa, lakini muuzaji hakumwelewa na kuamua kuchukua vile vinywaji na kuvirudisha dukani.

"Kijana wangu ambaye ni marehemu alifika nyumbani akaniambia mama nilipotoka hapa nimetumwa dukani kununua soda, nikafika pale dukani nikampa muuzaji fedha na yeye akanipa viywaji, lakini nilivyoondoka yule muuzaji akadai kwamba sijampa hela akachukua vile vinywaji sasa kwa sababu hiyo mama nimeamua kweli ninywe sumu," alisimulia mama.

Mama huyo alisema baada ya kumweleza hivyo alilazimika kumuita dada wa marehemu ili wamkimbize hospitali, lakini alifariki dunia wakiwa njiani kuelekea hospitali.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Bugogo, George Elias, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kuongeza kuwa baada ya marehemu kununua vinywaji hivyo hakupewa risiti.

Kaimu kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Geita, Ally Kitumbu, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa wanaendelea kufanya uchunguzi.

HABARI KIMATAIFA

# Mahakama Angola 'yambananisha' Isabel Santos tajiri wa Afrika

**LUANDA, Angola**

MAHAKAMA ya Juu ya Angola imeamuru kuwekewa kizuizi kwa mali zenye thamani ya karibu dola bilioni moja zinazomilikiwa na Isabel dos Santos, binti wa rais wa zamani wa nchi hiyo ya kusini mwa Afrika.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Lusa la Ureno, hati ya mahakama iliyonukuliwa Desemba 19, ilisema mamlaka ina ushahidi wa madai ya ubadhirifu na utakatishaji fedha haramu, huku ikiamuru kukamatwa kwa fedha za dos Santos katika taasisi zote za benki.

Lusa ilisema ukamataji huo pia unajumuisha hisa zote za dos Santos katika kampuni ya Angola ya Embalvidro, pamoja na asilimia 100 ya hisa katika kampuni ya mawasiliano ya simu ya Unitel T+ ya Cape Verde na Unitel STP iliyoko Sao Tome e Principe.

Pia ilieleza kuwa jumla ya asilimia 70 ya hisa zake katika MStar na Upstar Comunicacoes za Msumbiji zinapaswa kukamatwa pia.

Aidha, inaelezwa kuwa Dos Santos amekabiliwa na tuhuma za ufisadi kwa miaka, na kwamba mwaka 2019, mahakama hiyo iliamuru kukamatwa kwa mali yake kwa madai ya kusimamia fedha za serikali kwa makampuni ambayo alikuwa na hisa wakati wa urais wa baba yake, ikiwa ni pamoja na kampuni kubwa ya mafuta ya Sonangol.

Ilibainishwa kuwa Baba yake Dos Santos, Jose Eduardo dos Santos, alifariki Julai mwaka huu, na kwamba alitawala Angola kwa takriban miongo minne hadi 2017.

Msemaji wa dos Santos hakujibu mara moja ombi la maoni, na mara kwa mara alikanusha makosa yoyote na aliiambia CNN Ureno mwezi Novemba mwaka huu, kwamba mahakama nchini Angola haziko huru na kwamba majaji walitumika kutimiza ajenda ya kisiasa.

Agizo hilo linakuja baada ya shirika la polisi duniani Interpol kutoa notisi nyekundu kwa dos Santos mwezi uliopita, na kuzitaka mamlaka za kimataifa kumtafuta na kumkamata kwa muda.

***BBC***



Mkutano wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu Haiti. **Picha DW.**

# Putin aweka marufuku uuzaji mafuta nchi za magharibi

**MOSCOW, Russia**

RAIS wa Russia Vladimir Putin amesaini amri ambayo inaweka marufuku ya uuzaji wa mafuta na bidhaa za mafuta kwa mataifa yaliyoweka kikomo cha bei ya mafuta ya Russia, kuanzia Februari moja 2023 kwa miezi mitano.

Kundi la G7 la nchi tajiri duniani, Umoja wa Ulaya na Australia walikubaliana mwezi huu kikomo cha dola 60 kwa pipa moja la mafuta ghafi ya Russia, hatua ambayo ilianza kutekelezwa Desemba tano kwa sababu ya operesheni maalum ya kijeshi ya Moscow nchini Ukraine.

Amri hiyo ya Putin ilieleza kuwa hatua hiyo inaanza kutekelezwa Februari 2023, na inaendelea hadi Julai moja, 2023."

Amri hiyo pia ilisema Rais Putin anaweza kutoa ruhusa maalum kwa usambazaji kwa nchi ambazo ziko chini ya marufuku.

Kundi la G7 lilitoa wazo la kupunguzwa kwa bei mwezi Septemba ili kukomesha Russia kutumia mapato ya mafuta kufadhili vita vya Ukraine.

Ingawa mahitaji ya Magharibi ya mafuta ya Russia yalipungua baada ya uvamizi huo, mapato ya taifa hilo yalibaki juu kutokana na kupanda kwa bei na mahitaji mahali pengine, ikiwa ni pamoja na kutoka India na China.

Inaelezwa kuwa kikomo cha bei kinalenga kupunguza mapato ya mafuta ya Russia, na kwamba inazuia ghafi yoyote ya taifa hilo inayouzwa kwa zaidi ya dola 60 kusafirishwa kwa kutumia meli za mafuta za G7, EU, kampuni za bima na taasisi za mikopo.

Aidha, ilibainishwa kuwa kampuni nyingi kuu za kimataifa za usafirishaji na bima ziko ndani ya G7.

Mwezi huu, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky aliita kikomo cha bei kuwa wazo dhaifu ambalo halikuwa zito vya kutosha kuharibu uchumi wa Urusi.

Waziri wa Fedha wa Russia Anton Siluanov, alisema Jumanne kwamba nakisi ya bajeti ya nchi hiyo inaweza kuwa pana kuliko asilimia mbili iliyopangwa ya Pato la Taifa 2023, huku bei ya mafuta ikipunguza mapato ya mauzo ya nje.

Mafuta kwa sasa yanauzwa kwa takriban dola 80 kwa pipa kutoka kilele cha zaidi ya dola 120, inayoonekana Machi na Juni.

***VOA***

# Taliban yatakiwa kubadili misimamo dhidi ya wanawake

**UN**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) limeshutumu sera za serikali ya Taliban zinazowalenga wanawake na wasichana nchini Afghanistan, huku ikitoa wito wa ushiriki kamili, sawa, na wenye maana wa wanawake na wasichana nchini humo.

Kundi la Taliban limepiga marufuku wanawake kuhudhuria vyuo vikuu na kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) wiki iliyopita.

Baraza la Usalama lenye wanachama 15, lilionyesha kitiwa wasiwasi na vikwazo vinavyoongezeka vya elimu ya wanawake nchini Talban, ikisisitiza kufunguliwa tena shule na kubadili sera ambayo inawakilisha mmomonyoko wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi.

Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres, alisema kwamba vikwazo vya hivi karibuni ni lazima viondolewe.

"Marufuku ya wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu itakuwa na athari kubwa na ya haraka kwa shughuli za kibinadamu nchini, ikiwa ni pamoja na kwa UN," alisema.

Guterres alisema kuwa vikwazo vya hivi karibuni ni ukiukwaji wa haki za binadamu usio na uhalali, na kwamba hatua za kuwatenga na kuwanyamazisha wanawake na wasichana zinaendelea kusababisha mateso makubwa na vikwazo vikubwa kwa uwezo wa watu wa Afghanistan.

Inaelezwa kuwa mashirika matano ya juu yalisitisha kazi nchini Afghanistan baada ya wanawake kupigwa marufuku kuwafanyia kazi, na kwamba Care International, Baraza la Wakimbizi la Norway (NRC) na Save the Children walisema hawawezi kuendelea na kazi yao bila wafanyakazi wa kike.

Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji pia ilisitisha huduma huku Islamic Relief ikisema ilikuwa inasimamisha kazi zake nyingi.

Kundi la Taliban wiki iliyopita lilikamata wanawake watano waliokuwa wakishiriki maandamano katika mji mkuu wa Afghanistan, Kabul, kuhusu kupiga marufuku elimu ya wanawake.

Tangu kutwaa tena udhibiti wa nchi mwaka jana, Taliban wameweka vikwazo kwa haki za wanawake licha ya kuahidi utawala wao utakuwa mpole zaidi kuliko utawala ulioonekana katika miaka ya 1990.

***BBC***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABDULRAHMANI RAMADHANI SHEMSHANGUZO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4970/0203** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **MURIET** mwaka **2019,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/URA/RB/429396/2022**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**JOSEPHAT ALPHONCE RWEYEMAMU** anatangaza kupotelewa na **HATI YA KUSAFIRIA (PASSPORT) (KUIBIWA)** Iliyotolewa kwa namba **TAE 115502** iliyotolewa na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji **23/05/2019**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu

Taarifa ya polisi **IRI/IRI/RB/482396/2022**

Au awasiliane na muhusika kwa simu namba **0752839926**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **SILAJI HUSSEIN LWEZAURA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Hiace lenye namba za usajili **T343BDP.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/492476/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu **namba 0754754730.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba**
**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera**
**Usimamizi wa mirathi Na. 71/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**Rose Andrew Nyamwera wa Bukoba - Kibeta.**

**KATIKA SHAURI YA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA Joyce Andrew Nyamwela.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 30 Mwezi 01 mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:-** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo **tarehe 28 Mwezi 12 Mwaka 2022**

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA BUKOBA MJINI

**HAKIMU**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**MISC.LAND APPLICATION NO.34 OF 2021**
**RICHARD ANSELIMU MUSHI............APPLICANT**
**VERSUS**
**KILIMANJARO CENTRE FOR OPPHANS AND STREET CHILNDREN.........RESPONDENT .**

**NOTICE FOR MENTION,**

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on **21st February,2023 at 9:00 a.m.** before Honourable Judge in charge.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this **1st day of December , 2022**

DEPUTY REGISTRAR

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**J/PCF/54**
**KUITWA SHAURI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo MANGAKA**
**Wilaya ya NANYUMBU**
**MADAI NAMBARI 46 YA 2022**
**MDAI LUKIA ABDU MAMU**

**Mdaiwa MUSTAFA PWIRIRA LILANGA**
**Kwa: 1)............................................**
**2) MTENDAJI WA KIJIJI**
**3) MARATANI**
**4) .......................................**

Kwa kuwa Mdai/Wadaawa amaleta/Wameleta Mdai yake/yao kwamba /Eleza hapa habari za Madai)

**MADAI YA TALAKA**

Kwahiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii ya **MANGAKA tarehe 6/01/2023 saa 2:00 Asubuhi.**

Kwa kujibu madai hayo, kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima kuleta Mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **28 Mwezi 12, 2022**

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA KUKAZIA HUKUMU NA. 13/2022**

**NANZIA LYIMO.................. MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**GODWIN SAMWEL.......................MJIBU MAOMBI**

**<u>WITO/KUITWA SHAURINI</u>**

**GODWIN SAMWEL**
**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro **tarehe 11/1/2023 saa 2:30 Asubuhi** ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Imesainiwa leo **tarehe 21 Mwezi 12 Mwaka 2022**

R. R. KASELE
HAKIMU MKAZI MKUU
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHABANI OMARY CHIKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki (**haojue**) yenye namba za usajili **MC 188 CXB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/491669/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIETHA MARCUS MWINGIRA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA** Hiace yenye namba za usajili **T 942 DCV.** yenye CHASES NAMBA: **RZH1241001822.** Engine No; **2RZE85Z223FT**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/492675/2022**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**SALIM MOHAMED MALIONDO** anatangaza kupotelewa na **HATI YA KUSAFIRIA (PASSPORT)** Iliyotolewa kwa namba **AB 810030** iliyotolewa na Inspecta Jenerali wa Polisi **(IGP) 28/12/2022**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu Taarifa ya polisi **DSM/PHQ/RB/493681/2022**

Au awasiliane na muhusika kwa simu namba **0625336209**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BU



# PENZI LA WEMA, WHOZU CHALI

PENZI la Wema Sepetu na msanii Whozu linadaiwa kwa sasa halipo tena na kila mmoja ameshika hamsini zake.


Wawili hao wanadaiwa kuachana na Wema alianza kuposti snapchat anatamani kufa.

Katika mwendelezo huo huo amefuta picha zote za Whozu ambazo amewahi kuziposti kwenye page yake.

Hii ni dalili tosha wawili hao hawapo pamoja tena na mbaya zaidi Wema amepost video akicheza na mwanaume mwingine.

Mara kadhaa mrembo huyo wa Tanzania aliyeshinda taji katika shindano la mwaka 2006, huweka wazi mahusiano yake ya kimapenzi na anapoachana na mpenzi husika.

# RAPA TORY HATARINI JELA MIAKA 20




RAPA Tory Lanez wa Marekani amepatikana na hatia ya kumpiga risasi mwanamuziki mwenzake wa Hip hop, Megan Thee Stallion, mwaka wa 2020.

Mahakama ya Los Angeles ilimtia hatiani raia huyo wa Canada mwenye umri wa miaka 30 kwa kosa la kutekeleza uzembe wa kufyatua risasi, kushambulia kwa kutumia bunduki na kubeba silaha iliyopakiwa na ambayo haijasajiliwa.

Anakabiliwa na kifungo cha zaidi ya miaka 20 jela.

Megan, rapa mwenye umri wa miaka 27 aliyeshinda tuzo ya Grammy awali alitoa ushahidi alipigwa risasi miguuni baada ya kuondoka kwenye tafrija.

Aliwekwa rumande na anatarajiwa kuhukumiwa ifikapo Januari 27, mwakani.

Akizungumza baada ya kesi hiyo kukamilika, mmoja wa mawakili wa Megan, Thee Stallion aliwaambia waandishi wa habari "majaji wamefanikiwa kufikia ukweli. Nashukuru Megan ametendewa haki."



# HARMONIZE: WANAWAKE WENGI WANANIPENDA

NYOTA wa muziki wa Bongofleva na mkuu wa lebo ya Konde Worldwide, Harmonize, ameibuka na jipya kuhusu wanawake wengi kumzimikia ikiwa imepita wiki chache baada ya kuachana na aliyekuwa mpenzi wake na meneja, Kajala Masanja.

Kupitia Instagram, Harmonize amesema katika siku za hivi karibuni tangu wasikie habari yuko singo baada ya msalaba wake aliosema hadharani ataubeba kumwelemea, wanawake wengi wameanza kumvizia.

Msanii huyo hata yeye alikiri amechanganyikiwa ni kwa nini wanawake wanamfuata kila kona huku akikisia huenda ni kwa sababu ya nyota ya mafanikio yake kila uchao.

"Nimechanganyikiwa katika hili...wanawake siku hizi wananipenda kupita maelezo asikwambie mtu.

"Ni kwa sababu naendelea kupaa kiutajiri au pengine ni kutokana na utanashati wangu," aliandika Harmonize.

# PRISONS KUPATA DONGE NONO IKIMFUNGA SIMBA

**Na Saada Akida**

MAAFANDE wa Prisons wameahidiwa kupokea bonasi ya Sh. milioni 30 endapo watafanikiwa kupata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ahadi hiyo imetolewa jijini Dar es Salaam jana na wadhamini wakuu wa timu hiyo kutoka Mbeya, Kampuni ya Silent Ocean.

Meneja Masoko wa Silent Ocean, Mohammed Kamilagwa, alisema, endapo timu hiyo itapata matokeo ya sare katika mechi hiyo itaambulia Sh. milioni 10 na hiyo imekuwa ni kawaida yao kuwapa wachezaji wao posho wanaposhinda michezo mikubwa.

Kamilagwa alisema mechi zilizopita wamefanya vizuri na wachezaji walipata posho jambo ambalo linawaongezea motisha ya kujituma zaidi katika kila mechi wanayocheza.

"Fedha tulizowaahidi ni kubwa kuliko mechi zilizopita, hii ni kuongeza ushindani katika ligi yetu, kwa juhudi hizi tumeona Tanzania Prisons ni timu sahihi kwetu kuongeza nguvu kwa sababu timu ya umma, lakini inawaongezea wigo mkubwa wachezaji kupata ajira," alisema Kamilagwa.

Katibu Mkuu wa Tanzania Prisons, Rajabu Kifukwe alisema, wadhamini wamekuwa wakijitoa na kuwapa fedha na mahitaji mengine ya timu.

Kifukwe alisema wamejiandaa vizuri na timu tayari imeshafika jijini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo, ambapo anaamini watapata matokeo mazuri yatakayowaweka katika nafasi nzuri kwenye msimu huu.

"Tunawaahidi wadhamini timu inaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Simba, tunatambua ni timu kubwa iko vizuri, tunawaheshimu na tunaenda kuwapa changamoto katika mchezo wetu ujao," alisema Kifukwe.

Naye nahodha wa Prisons, Benjamin Asukile, alisema wamejipanga kuonyesha kiwango cha juu zaidi ya walichokionyesha katika mchezo dhidi ya Yanga.

Asukile alisema, wamekuja kivingine na timu yao haina historia ya kupoteza mechi zote mbili wanapokuja Dar es Salaam kukutana na timu hizo kongwe.




Meneja Masoko wa Kampuni ya Silent Ocean, Mohamed Kamelagwa (kushoto), akitangaza motisha ya Sh. milioni 30 kwa wachezaji wa Prisons endapo wataifunga Simba katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Kulia ni Ofisa Habari wa Prisons, Jackson Mwafulango na Katibu Mkuu wa timu hiyo, Rajabu Kifukwe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kick boxing kuchuana Februari

**Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mchezo wa ngumi na mateke maarufu kama Kick Boxing kwa vijana wenye umri chini ya miaka 16 yanatarajiwa kufanyika kuanzia Februari 25, mwakani kwenye klabu ya Fay Heroes jijini, Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Klabu ya Fay Heroes, Abdul Ally, alisema lengo la mashindano hayo ni kuinua vipaji vya wachezaji chipukizi ambao walikuwa wanahitaji kupata nafasi.

"Tumeamua kufanya mashindano hayo baada ya kubaini vipaji vingi viko mtaani, kuna vijana wengi ambao wanafahamu mchezo huu isipokuwa wanashindwa kutoka kwa sababu hawajui waanzie wapi,"alisema Ally.

Mkurugenzi huyo aliongeza mbali na mashindano hayo, pia klabu hiyo imeandaa filamu maalumu iliyojaa vionjo mbalimbali itakayosaidia kuutangaza mchezo huo.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Wushu Tanzania, Sempai Kapipi, aliliambia gazeti hili wameamua kufanya mashindano hayo baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu jambo ambalo lilirudisha nyuma maendeleo ya mchezo huo.

Kapipi alisema usajili wa wachezaji watakaoshiriki michuano hiyo umeshaanza huku akiongeza pia kutakuwa na michezo mingine itakayoshindaniwa ambayo ni karate, ngumi, judo, wushu.

## Atupele, Banka matumaini Ruvu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutopata ushindi katika michezo 12 mfululizo, mabosi wa Ruvu Shooting wamewaondoa hofu mashabiki wao na kusema watasajili wachezaji wapya katika dirisha dogo ili kusaidia kuimarisha kikosi chao, imefahamika.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, aliliambia gazeti hili jana, tayari wameshanasa saini ya straika mkongwe kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Atupele Green na kiungo, Mohamed Banka ambaye alikuwa akiitumikia Namungo FC.

Bwire alisema pia klabu iko katika hatua za mwisho za mzunguko wa wachezaji wengine ambao watai-saidia timu yao kurejesha makali yake.

"Tunawapa pole sana wale wazee wa mikeka, walikuwa wakitubetia tutaibuka na ushindi, lakini mikeka yao ilikuwa inachanika, sasa nawaambia haitochanika tena, na mashabiki wetu waelewe kipindi cha huzuni sasa kimefika mwisho. Tunajua tatizo letu lilikuwa ni eneo la ushambuliaji, tumeamua kulifanyia kazi," alisema Bwire.

Naye Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Mbwana Makata, alisema tatizo lao litamalizika kwa sababu alilazimika kutumia mawinga kutokana na kukosa washambuliaji wa kati.

## Makocha watakiwa kushawishi chipukizi

**Na Shufaa Lyimo**

MWENYEKITI wa Chama cha Soka Wilaya ya Ilala (IDFA), Kondo Mussa, amewataka washiriki wa kozi ya ukocha ngazi ya awali (Grassroot), kuwashawishi wachezaji kuupenda mchezo wa mpira wa miguu.

Washiriki 22 wanatarajia kumaliza kozi iliyoandaliwa na IDFA Jumamosi na watakuwa na jukumu la kufundisha watoto wenye umri wa kuanzia miaka minne hadi 12.

Kondo alisema kila mshiriki anatakiwa kuyafanyia kazi kwa vitendo mafunzo yote waliyofundishwa ili kuwaendeleza vijana.

"Wito wangu kwa washiriki msikilize na kuzingatia yale mtakayofundishwa, mkayatumie vizuri ili mkatimize malengo yenu, hakuna njia fupi, maendeleo ya mpira yanahitaji rasilimali watu, utaalamu," alisema kiongozi huyo.

Naye Katibu Mkuu wa IDFA, Daudi Kanuti, alisema kozi hiyo inashirikisha makocha wengi vijana na ana imani watafika mbali katika kujiendeleza kwenye taaluma hiyo.

## ZISIKUPITE

### BARCA YATOA MSIMAMO

RIPOTI kutoka Hispania zinadai Barcelona itakataa kumuuza Frenkie de Jong anayelengwa na Manchester United licha ya Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 25 kuwa sehemu muhimu ya mipango ya Xavi. ***(Mail)***

### JUDE AIVURUGA LIVERPOOL

LIVERPOOL hawatasimamisha harakati zao za kumwania, Jude Bellingham licha ya kuizidi kete Manchester United katika mbio za kumnasa Cody Gakpo. ***(Mail)***

### JUDE AITAMANI MADRID

JUDE Bellingham anapendelea zaidi kujiunga na Real Madrid kutoka Borussia Dortmund, licha ya Liverpool, Manchester City na Manchester United kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(AS)***

### DAU LA ENZO HADHARANI

BENFICA imekataa ofa ya euro milioni 100 kutoka klabu ambayo haijatajwa jina kwa ajili ya kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool na Real Madrid, na haitamuuza kwa chini ya euro milioni 120 mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Record)***

### LOCATELLI ANUKIA MADRID

KLABU ya Real Madrid ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 24, ambaye yuko kwa mkopo Juventus kutoka Sassuolo. ***(AS)***

### FOFANA, CHELSEA SAFI

CHELSEA wamefikia makubaliano ya euro milioni 12 na Molde ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye umri wa miaka 20. ***(Fabrizio Romano)***

### MENDY AIKATAA CHELSEA

GOLIKIPA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy, mwenye umri wa miaka 30, amepuuzilia mbali mkataba mpya wa miaka sita hapo Stamford Bridge kwa sababu anaamini klabu hiyo haimwonyeshi heshima ya kutosha. ***(Sun)***

### MUDRYK NJIA MOJA

OFISA Mtendaji Mkuu wa Shakhtar Donetsk, Carlo Nicolini, amethibitisha Arsenal wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhailo Mudryk, mwenye umri wa miaka 21. ***(Calciomercato)***

### JOAO ATAJWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inafikiria kumsajili kwa mkopo mchezaji wa Atletico Madrid, Joao Felix mwenye umri wa miaka 22, katika dirisha dogo la Januari. The Blues hao wanataka kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(Mail)***

### MUDRYK SOKONI RASMI

ARSENAL imetoa ofa ya paundi milioni 55 kwa ajili ya kumnunua winga wa Shakhtar Donetsk na Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhaylo Mudryk. ***(The Telegraph)***

### ARSENAL YAMFUATA RABIOT

KLABU ya Arsenal itajaribu kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake utamalizika Juventus msimu wa joto. ***(Repubblica, via Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD AFUNGUKA KUHUSU NDOTO ZAKE

Mshambuliaji huyo wa United na England asema anahitaji kufunga mabao mengi zaidi ili...

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford anatazamia kupata bao bora zaidi msimu huu baada ya kuongeza idadi yake katika ushindi wa Ligi Kuu England huku akisaidia Manchester United kupata ushindi mnono dhidi ya Nottingham Forest hapo juzi.

Kikosi cha Kocha, Erik ten Hag kilirejea katika mchezo wa Ligi Kuu England kwenye Uwanja wa Old Trafford na kilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 3-0.

Rashford, ambaye alikuwa na msimu mgumu wa 2021-22, alikuwa na wakati mzuri zaidi kwa kuifungia timu yake bao la kwanza kabla ya kusaidia la pili.

Inamfanya sasa kufikisha mabao 10 katika mechi 21 kwenye michuano yote kwa United mwaka huu na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekiri ana lengo akilini.

"Kila fowadi huwa na namba ambayo anataka kujaribu kuifikia," alisema Rashford akiiambia Amazon Prime Sport.

"Kwangu mimi, ni kufunga zaidi ya nilivyowahi kufunga katika msimu mmoja. Nadhani ni 22 au 23. Ninafurahia kile ninachofanya kwa dakika hiyo."

Msimu bora wa awali wa Rashford akiwa na United ulikuwa wa 2019-20, alipofunga mabao 22 katika ngazi ya klabu na timu ilifika nusu fainali ya Kombe la FA, Kombe la EFL na Ligi ya Europa.

Baada ya kuwa na wakati mgumu msimu uliopita chini ya kocha wa muda, Ralf Rangnick, Rashford amefurahia mabadiliko yake chini ya Erik ten Hag na alizungumzia hali ya kuimarika katika kikosi hicho tangu Mholanzi huyo achukue usukani.

"Tunashinda michezo zaidi na nadhani kiwango cha uchezaji kimekuwa cha juu zaidi," aliongeza.

"Nimefurahishwa na jinsi tunavyokuwa kwa sasa na tunatumaini tunaweza kuendelea.

"Ni mawazo tofauti kabisa na msimu uliopita, timu tofauti inayocheza soka tofauti. Tunapaswa kufunga mabao mengi zaidi katika michezo mingi zaidi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,062,0


MECHI KALI
ATLETICO MADRID
VERSUS
ELCHE
1 | 1.26
X | 5.43
2 | 11.06

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAVERTZ AMSIFU POTTER KUWAPA UHURU CHELSEA



**LONDON, England**

KAI Havertz alisifu "uhuru" uliotolewa na Kocha Graham Potter kama ufunguo wa uchezaji wake mzuri baada ya Chelsea kushinda mabao 2-0 dhidi ya Bournemouth, iliyochezwa Jumanne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alifunga bao moja na kusaidia jingine katika ushindi wa 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Stamford Bridge, akifungua ukurasa wa mabao kabla ya kumsaidia Mason Mount kupachika goli la pili.

Huo ulikuwa ushindi wa kwanza kwa Chelsea iliyofanya majaribio sita, lakini Havertz sasa ana mabao manne chini ya Potter katika michuano yote na anafurahia kufanya kazi na kocha huyo wa zamani wa Brighton and Hove Albion.

"Ananipa uhuru wa kufanya chochote ninachojisikia vizuri uwanjani," alisema Havertz akiiambia Amazon Prime Sport.

"Napenda kucheza huru na kuwa ndani ya boksi, ananifanya nijiamini sana.

Potter, ambaye alirithi nafasi ya Thomas Tuchel, Septemba mwaka huu naye aliwasifia wachezaji wake, ingawa alimpoteza Reece James kutokana na jeraha lingine na alikuwa akisubiri kuchunguzwa.

# Sergio mambo magumu Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

HATIMA ya Sergio Busquets katika klabu ya Barcelona imekuwa na mzozo tangu kiungo huyo alipotangaza kustaafu kucheza soka la kimataifa.

Mkataba wa Busquets ndani ya Barca unamalizika mwishoni mwa msimu huu na inaonekana mchezaji huyo ameamua kuondoka Camp Nou ifikapo mwakani na anatajwa kujiandaa kuhamia katika Ligi Kuu Marekani, huku Inter Miami ya huko ikimwania.

Hata hivyo, Kocha Xavi Hernandez hana nia ya kuruhusu Busquets kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu. Kuna maoni Xavi anajaribu kumshawishi kiungo huyo kusalia Camp Nou angalau hadi Januari, mwaka 2024.

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo, inaonekana Xavi haungwi mkono na bodi ya klabu hiyo kuhusiana na wazo la Busquets kusalia Camp Nou hadi nusu ya kwanza ya msimu wa 2023/24.

Wanaamini kuondoka kwa kiungo huyo mkongwe katikati ya msimu kutaathiri upangaji wa kikosi na kulazimu klabu kumtafuta kiungo mpya wakati wa dirisha la usajili la Januari.



078,169/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/12/22 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Crystal Palace | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 02. 31/12/22 | 18:30 | Hapoel Tel Aviv FC vs Maccabi Netanya FC | 2.55 | 3.35 | 2.65 |
| 03. 31/12/22 | 18:30 | Sekhukhune United vs AmaZulu FC | 2.50 | 2.85 | 3.10 |
| 04. 31/12/22 | 19:00 | Bnei Sakhnin FC vs Hapoel Haifa FC | 2.49 | 3.20 | 2.80 |
| 05. 31/12/22 | 20:10 | FC Ashdod vs Hapoel Jerusalem FC | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 06. 01/01/23 | 15:00 | Blackburn Rovers vs Cardiff City | 2.18 | 3.35 | 3.25 |
| 07. 01/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs FC Lorient | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 08. 01/01/23 | 18:00 | Crewe Alexandra vs Tranmere Rovers FC | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 09. 01/01/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Carlisle United | 2.49 | 3.25 | 2.80 |
| 10. 01/01/23 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 11. 01/01/23 | 18:00 | Grimsby Town vs Stockport County FC | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 01/01/23 | 18:00 | Walsall FC vs Mansfield Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 13. 01/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Burton Albion | 2.70 | 3.45 | 2.45 |
| 14. 01/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Sunderland AFC | 2.85 | 3.15 | 2.49 |
| 15. 01/01/237 | 18:00 | Huddersfield Town vs Luton Town | 2.80 | 3.25 | 2.49 |
| 16. 01/01/23 | 18:00 | Colchester United vs Swindon Town | 2.95 | 3.20 | 2.36 |
| 17. 01/01/23 | 20:00 | Hapoel Hadera FC vs Maccabi Bney Reine | 2.40 | 3.15 | 3.00 |

MECHI ZA USHINDI
“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE
“2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 29/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:10 | 2507 | Kazma SC vs Al Salmiyah | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 17:00 | 3017 | Giresunspor vs Gaziantep BB | 2.27 | 3.34 | 2.99 |
| 17:00 | 4202 | Sivasspor vs Galatasaray | 4.28 | 3.78 | 1.73 |
| 17:00 | 4716 | Hyderabad FC vs Northeast United FC | 1.31 | 4.87 | 7.79 |
| 18:00 | 2999 | FAR Rabat vs Wydad Casablanca | 2.81 | 2.81 | 2.57 |
| 18:00 | 4488 | Braintree vs Chippenham Town | 1.67 | 3.78 | 4.26 |
| 18:00 | 5685 | Al Masry Club vs Aswan | 1.75 | 3.14 | 5.38 |
| 18:40 | 5083 | Burgan SC vs AL Qadsia | 6.81 | 5.06 | 1.32 |
| 19:00 | 1705 | Lorient vs Montpellier | 2.01 | 3.54 | 3.39 |
| 19:00 | 3975 | Aris Salonica vs Panetolikos | 1.38 | 4.17 | 8.95 |
| 19:00 | 4522 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.33 | 3.19 | 3.04 |
| 20:00 | 2062 | Gil Vicente vs Santa Clara | 2.14 | 3.20 | 3.40 |
| 20:00 | 2480 | Zamalek vs Ismaily SC | 1.45 | 3.98 | 7.37 |
| 20:00 | 4654 | Besiktas vs Adana Demirspor | 1.78 | 3.89 | 3.89 |
| 20:00 | 5265 | Belenenses vs Leixoes | 2.52 | 3.26 | 2.62 |
| 20:15 | 3686 | Difaa El Jadidi vs FUS Rabat | 2.70 | 2.85 | 2.85 |
| 21:00 | 1324 | Atalanta vs AZ Alkmaar | 1.50 | 4.26 | 5.03 |
| 21:00 | 3746 | QPR vs Luton Town | 2.21 | 3.27 | 3.12 |
| 21:00 | 5311 | Reims vs Rennes | 3.19 | 3.34 | 2.16 |
| 21:15 | 1693 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.63 | 3.23 | 2.63 |
| 22:00 | 1837 | Crewe vs Carlisle | 3.12 | 3.27 | 2.21 |
| 22:00 | 1923 | Nacional Madeira vs Benfica Lisbon B | 2.66 | 3.40 | 2.41 |
| 22:00 | 2450 | GD Estoril vs Boavista | 2.27 | 3.13 | 3.18 |
| 22:30 | 4672 | Sccm Chabab Mohammedia vs Olympique Safi | 2.60 | 2.90 | 2.90 |
| 22:45 | 1093 | Sutton United vs Gillingham | 1.91 | 3.17 | 4.16 |
| 22:45 | 1319 | Northampton vs Swindon Town | 2.08 | 3.22 | 3.47 |
| 22:45 | 1323 | Millwall vs Bristol City | 1.95 | 3.42 | 3.62 |
| 22:45 | 1356 | Barnsley vs Fleetwood Town | 1.67 | 3.62 | 4.85 |
| 22:45 | 1597 | Doncaster vs Rochdale | 2.10 | 3.22 | 3.42 |
| 22:45 | 1667 | Huddersfield vs Rotherham | 2.11 | 3.27 | 3.32 |
| 22:45 | 1692 | Plymouth vs Wycombe | 2.16 | 3.31 | 3.16 |
| 22:45 | 1697 | Barrow vs Tranmere | 2.20 | 3.08 | 3.32 |
| 22:45 | 1883 | Coventry vs Cardiff | 2.06 | 3.32 | 3.42 |
| 22:45 | 3004 | Bradford City vs Harrogate | 1.73 | 3.66 | 4.36 |
| 22:45 | 3041 | Bristol Rovers vs Exeter | 2.40 | 3.17 | 2.87 |
| 22:45 | 3180 | Sheffield Wed vs Port Vale | 1.67 | 3.67 | 4.76 |
| 22:45 | 3238 | Oxford Utd vs Charlton | 1.95 | 3.46 | 3.61 |
| 22:45 | 4221 | Walsall vs Stockport | 3.18 | 3.18 | 2.22 |
| 22:45 | 4325 | Shrewsbury vs Cheltenham | 1.94 | 3.31 | 3.80 |
| 22:45 | 4399 | Blackburn vs Middlesbrough | 2.87 | 3.22 | 2.38 |
| 22:45 | 4731 | Forest Green vs Burton | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 22:45 | 4773 | Portsmouth vs Ipswich | 3.53 | 3.33 | 2.02 |
| 22:45 | 5597 | Peterborough vs MK Dons | 1.83 | 3.57 | 3.97 |
| 22:45 | 5774 | Wigan vs Sunderland | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 22:45 | 5849 | Colchester vs AFC Wimbledon | 2.47 | 3.12 | 2.82 |
| 23:00 | 2168 | Nice vs Lens | 3.14 | 2.89 | 2.43 |
| 23:00 | 2762 | West Bromwich vs Preston | 1.77 | 3.51 | 4.35 |
| 23:00 | 4541 | Marseille vs Toulouse | 1.49 | 4.49 | 5.58 |
| 23:15 | 3890 | Blackpool vs Sheffield Utd | 3.95 | 3.61 | 1.82 |
| 23:30 | 2189 | Atletico Madrid vs Elche | 1.26 | 5.43 | 11.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# NTIBAZONKIZA KUIVAA PRISONS, SIMBA IKITAMBULISHA MASHINE

**Na Adam Fungamwango**




Kiungo wa Simba, Saido Ntibazonkiza.

WAKATI kiungo mpya, Saido Ntibazonkiza, anatarajiwa kuanza kutumikia timu yake ya Simba kesho katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Prisons, klabu hiyo huenda ikatangaza mchezaji mpya iliyemsajili kwenye dirisha dogo ambalo limefunguliwa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanatarajia kukamilisha taratibu zote muhimu kesho na mambo yakienda vyema, Ntibazonkiza atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoshuka dimbani kuwakabili Maafande wa Prisons.

Ahmed alisema mchezaji huyo yuko tayari kuongeza nguvu katika kikosi cha Simba na wanaamini ujio wake utawasaidia.

“Siku hiyo uwanjani itakuwa ni kama sherehe kwa wanachama na mashabiki wa Simba, tunakwenda kuuaga mwaka 2022, kwenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwenda kupongezana Wanasimba, kukosoana na kuulizana kuanzia kwenye timu yetu na hata maisha ya kawaida kama wanadamu, “ alisema Ahmed.

Aliongeza klabu hiyo inaendelea na mchakato wake wa kusajili na huenda pia kesho wakatambulisha mchezaji mpya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

“Mwenyekiti wa Bodi (Salim Abdallah) ameniambia analifanyia kazi hilo, likiwezekana atanijulisha kwa hiyo Ijumaa itakuwa ni mechi fulani hivi ya Wanasimba na baada ya hapo wakazi wa Dar na Tanzania Bara hawataiona tena timu kwa sababu itaelekea Zanzibar kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi,” alisema kiongozi huyo.

Aliongeza wanachama na mashabiki wa Simba wasikaririshwe majina ya wachezaji wanaodaiwa wanasajiliwa na badala yake wasubiri taarifa rasmi ya klabu.

“Tunaendelea na usajili wa wachezaji wapya, wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi, wanatakiwa kukaa wakisubiri mchezaji yoyote atakayekuja kuisaidia timu na siyo jina la mtu au lazima aje mchezaji fulani,” alisema Ahmed.

# YANGA, FEITOTO, MOSHI MWEUSI

INATOKA UK. 32

Shirikisho Afrika.

Nyota wanaotajwa kuwindwa na Yanga ni kiungo wa Geita Gold FC, Kelvin Nashon pamoja na kumrejesha kikosini aliyekuwa mshambuliaji wao, Yacouba Songne ambaye kwa sasa yuko fiti baada ya kupona majeraha yaliyokuwa yanamsumbua.

Hata hivyo inadaiwa Geita Gold FC wameanza kuweka vikwazo katika usajili wa Nashon kutokana na tayari imeshapoteza wachezaji wengine wawili wa kikosi cha kwanza ambao ni George Mpole aliyesajiliwa FC Lupopo ya DRC na Saido Ntibazonkiza, aliyetua Msimbazi.

Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, alisema klabu yao ina mipango ya kusajili wachezaji wapya zaidi ya wawili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao na hatimaye kufikia malengo.

Haji alisema wamepokea mapendekezo kutoka katika benchi la ufundi lililoko chini ya Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi, ambalo limeainisha aina ya wachezaji wanaowahitaji.

“Tutasajili wachezaji kulingana na mapendekezo ya benchi letu la ufundi, lakini kuna wachezaji ambao walikuwa majeruhi wamerejea, watakuwa sehemu ya kikosi cha Yanga.

Huu ni wakati wetu Yanga kuweka alama kwenye mashindano ya kimataifa, mfumo wetu ni ule ule mchezaji tunayemsajili lazima awe bora sana au zaidi ya yule ambaye tunaye,” alisema kiongozi huyo.

Katika hatua nyingine, Yanga imewasilisha barua rasmi kwa uongozi wa Azam FC ikitaka kuwasajili nyota wake wa kimataifa, James AkamiNko na Kipre Junior.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, amethibitisha klabu yao kupokea maombi hayo na itatoa majibu ya upatikanaji wa nyota hao huku akiongeza, pande hizo mbili zimefanya mazungumzo.

# MGUNDA AENDELEA

INATOKA UK. 32

Aigle Noir ya Burundi.

Azam itacheza mechi yake ya kwanza Januari 3, mwakani dhidi ya Malindi wakati Simba itavaana na Mlandege na siku inayofuata Yanga wakawakabili KMKM na Chipukizi itawaalika Aigle Noir.



Michezo
Alhamisi Desemba 29, 2022
Nipashe




UKURASA 29

## Rashford afunguka kuhusu ndoto zake

# YANGA, FEITOTO, MOSHI MWEUSI

## •••Jangwani sasa yamgeukia Nashon, yapiga hodi Azam...

**Na Saada Akida**

SAKATA la kiungo Mtanzania, Feisal Salum 'Feitoto' dhidi ya klabu yake ya Yanga limeendelea kugubikwa na sintofahamu baada ya nyota huyo kudaiwa kugomea mazungumzo kumrejesha katika kikosi cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara yaliyokuwa yanaendelea, imeelezwa.

Mazungumzo hayo yanadaiwa kuhusisha vigogo kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, lakini hadi jana jioni hakuna makubaliano yaliyofikiwa huku Feitoto hajulikani alipojificha.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema wawakilishi wa Yanga walifanya kikao na nyota huyo kwa ajili ya kufikia makubaliano ya kuboresha mkataba ili asalie ndani ya klabu hiyo, lakini kikao hicho hakikuzaa matunda.

Chanzo chetu kiliendelea kusema Feitoto hajaripoti kambini kama wachezaji wengine walivyoingia ili kujiandaa na safari ya kuelekea Turiani, mkoani Morogoro kuwafuata Mtibwa Sugar na inaelezwa hapatikani katika namba ya simu yake inayofahamika.

Chanzo hicho kiliendelea kusema baada ya Feitoto kuendelea kushikilia msimamo wake, pia nyota huyo kutoka Zanzibar inadaiwa amepanga kusafiri kwenda mapumzikoni nje ya Tanzania katika kipindi hichi ambacho Ligi Kuu Bara itasimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Jumapili.

"Msimamo wa Feitoto unawapasua vichwa viongozi wa klabu, mazungumzo hayajafanikiwa, imetumika nguvu kubwa lakini bado hakuna dalili nzuri, bado hajarejea kambini, kikosi chetu tayari kimeingia kambini Avic Town," kilisema chanzo chetu.

Kilisema kutokana na sintofahamu hiyo, benchi la ufundi limemwondoa kwenye mipango yake mpaka pale suala lake litakapomalizika.

"Hayuko kambini na viongozi bado wanaendelea na kuhakikisha wanafanikiwa kumshawishi, wanataka akubali kukaa mezani na kuzungumza kuhusu maboresho ya mkataba, aachane na uamuzi wa kuuvunja mkataba uliopo, hii itakuwa ni mara ya pili baada ya juzi kuwagomea," kiliongeza chanzo hicho.

Wakati huo huo Yanga imeanza mazungumo ya kusajili nyota wawili wapya ili kuongeza nguvu katika kikosi chao ambacho Februari mwakani kitaanza kusaka matokeo chanya kwenye hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa ya Kombe la

INAENDELEA UK. 31




Nyota wa Azam FC, James Akaminko, ambaye ameingia katika rada za Yanga. **PICHA: MTANDAO**

## Mgunda aendelea kuzichanga karata

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI imepangwa kuanza dhidi ya Mlandege katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yatakayofanyika Zanzibar, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema anahitaji kufunga 'hesabu' za mwaka kwa ushindi ili kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba inatarajia kuikaribisha Prisons katika mechi ya raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema wachezaji wake wanaendelea vyema na mazoezi na kila mmoja akili yake imeelekea katika kuvuna pointi tatu muhimu kwenye mchezo huo.

Mgunda alisema anafahamu mechi dhidi ya Prisons haijawahi kuwa nyepesi, hivyo kila mchezaji amejipanga kupambana kuhakikisha wanapata matokeo bora na hatimaye kufikia malengo.

Alisema amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya michezo iliyopita na sasa kuitazama mechi iliyoko mbele yao ambayo ni muhimu kwa wakati huu.

"Leo (jana) tumeanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu wa Ijumaa dhidi ya Tanzania Prisons, ni mchezo unaotarajiwa kuwa na upinzani mkubwa, mechi ngumu na inayohitaji akili pia," alisema Mgunda.

Kocha huyo aliongeza kikosi chake kitashuka dimbani kwa tahadhari lakini wakiongeza umakini katika mashambulizi ambayo yatasaidia kuwapa mabao mengi.

"Malengo yangu ni kushinda mchezo huo, nimewaandaa vizuri wachezaji, najua mchezo utakuwa na ushindani, lakini tukiwakamata mapema, tutajiweka mahali salama, ninaamini watafanya kile ambacho wanakionyesha kwenye mazoezi," Mgunda alisema.

Wakati huo huo katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yatafanyika kuanzia keshokutwa, Simba ambao ni mabingwa watetezi imepangwa katika Kundi C pamoja na Mlandege FC na KVZ zote za Zanzibar.

Kundi A linaundwa na timu za Azam FC, Malindi na Jamhuri wakati mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Singida Big Stars na KMKM ziko Kundi B na Kundi D linaundwa na Namungo, Chipukizi na

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >